**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake. |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |

| | |
|---|---|
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 79.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA NNE**

**Kikao cha Tano - Tarehe 27 Januari, 2015**

*(Kikao kilianza Saa 3.00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Mwenyekiti, (Mahamoud Muhammed Mussa) alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 74**

**Uharibifu wa Mazingira Maeneo ya Uchimbaji Vifusi**

*(Mjumbe aliyeuliza suali hili ameliondoa)*

**Nam. 19**

**Mamlaka ya Naibu Kamishna wa TRA Zanzibar**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub –** Aliuliza :-

Kwa kuwa Maamuzi ya Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambaye yupo Zanzibar hayana uzito kwa bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia Zanzibar ambapo ushuru wa bidhaa hizo hukadiriwa upya mara zinapoteremshwa Tanzania bara. Na kwa kuwa, kiutendaji TRA bado inachukulia Zanzibar kuwa miongoni mwa nchi za nje, ambapo Mheshimiwa Waziri anafahamu vizuri suala hili kwa vile ameshakua Naibu Waziri wa Fedha Bara.

(a) Je, kuna ulazima gani kwa TRA kuwa na Afisa mwandamizi wa cheo cha Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Zanzibar mwenye watumishi wengi chini yake, wakati kazi wanayofanya ya kuzikaguwa na kuzifanyia tathmini bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia Tanzania Zanzibar haitatambuliwa na Mamlaka husika Tanzania Bara.

(b) Je, Serikali haioni kuwa utaratibu wa kuichukulia Tanzania Zanzibar kuwa nchi ya kigeni unakiuka Katiba ya nchi na hati ya Muungano.

**Mhe. Waziri wa Fedha –** Alijibu :-

Mhe Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 19 lenye kifungu (a) na (b) kwanza naomba nitoe maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, Mmalaka ya Mapato Tanzania (TRA) ni taasisi ya Muungano iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria Na. 11 ya mwaka 1985. Mamlaka ya Mapato Tanzania pia ina ofisi yake Zanzibar. Kazi ya msingi ya TRA – Zanzibar ni kukusanya mapato ya Muungano yanayotokana na kodi ya Mapato, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977.

Aidha, naomba nilielezee Baraza lako tukufu kuwa, Kodi itokanayo na ushuru wa Forodha inasimamiwa na Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya 2004, na kwa mujibu wa Sheria hiyo, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni moja kati ya sehemu ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki imeweka utaratibu wa uwekaji thamani bidhaa zinazotoka nje na ndani wa nchi wanachama wa Jumuiya hiyo. Hata hivyo, kwa kuwa Zanzibar ni Kisiwa, hutumia viwango vya Ushuru/Kodi moja, kunaweza kuathiri shughuli za Uchumi wa Zanzibar. Hivyo, Serikali imeweka utaratibu wa viwango vya kodi tofauti kwa bidhaa kama zilivyoainishwa katika Sheria ya Ushuru wa Forodha wa bidhaa zinazoingizwa Zanzibar kwa madhumuni ya Soko na matumizi ya ndani ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kuna tofauti ya viwango vya Kodi, bidhaa itakaposafirishwa kwa madhumuni ya kuingia katika soko na matumuzi ya Tanzania Bara, TRA wameweka utaratibu wa kuitoza tofauti ya kodi kulingana na viwango vya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakilishi lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(**a**) Mhe. Mwenyekiti, kuna umuhimu kwa Zanzibar kuwa na Afisa Mwandamizi wa cheo cha Naibu Kamishna kwa madhumuni ya kusimamia ukusanyaji wa mapato yatokanayo na Kodi ya mapato, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa kwa lengo la kuimarisha shughuli nyengine za uchumi wa Zanzibar. Tathmini za kodi kwa bidhaa zinazotoka Zanzibar kwenda katika soko la Tanzania Bara inalengo la kuweka uwiano uliosawa kwa soko la Tanzania Bara.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Serikali haioni kama *TRA* inaichukulia Zanzibar kama Nchi za Kigeni kwani utaratibu wa kutoza tofauti ya kodi uko katika nchi nyingi duniani zenye Muungano kama wetu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza suali moja la nyongeza.

Tanzania inatokana na Tanganyika na Zanzibar ndio maana ikaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, vigezo vilivyotumia Tanzania na hapa karibu TRA ni vimoja, *formular* ni moja. Lakini Zanzibar kwa nini ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tathmini ya ongezeko la kodi hufanyika Zanzibar wakati mzigo umepitia Zanzibar kwenda Tanzania bara. Utaratibu huu umeishusha hadhi ya Zanzibar, na inaonekana kama uliyechukua *cocaine.*

Je, Naibu Waziri katika sehemu ya Jamhuri ya Muungano ameliona hilo wananchi wa Zanzibar wanavyoteseka muda mrefu na suala hilo.

Hivi juzi tu kulikuwa na makontena mangapi tumeshuhudia baada ya kelele za muda mrefu baadae ndio ukapatikana ufumbuzi, na bado kuna mizigo ya Wazanzibari imekwama; kuna magari yameandikwa *transite* Zanzibar.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mjumbe uliza suala.

**a)** **Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Je, unatoa kauli gani kuhusu suala hilo kwa wafanya biashara.

b) Kwa kuwa Tatizo hili ni la muda mrefu sana na limeathiri maendeleo ya biashara, huoni imefika wakati viongozi wakuu wa nchi akiwemo Rais wa Zanzibar na Rais wa Jamhuri ya Muungano, kukaa pamoja kutatua kadhia hii.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Kwanza nawapa pole sana wafanyabiashara wa Zanzibar ambao wanapata usumbufu wakati wa kuleta mizigo yao kutoka Tanzania Bara, kutoka nje kupitia bandari ya Tanzania bara, hilo si jambo la kawaida hata kidogo na sisi Wizara ya Fedha Zanzibar huwa hatulipendelei.

Nachukua maelezo ya mwenzangu Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub na nataka nimuahidi kwamba katika vikao vyetu vya mashirikiano baina ya wizara ya Fedha ya SMT na Wizara ya Fedha ya Zanzibar, suala hili tutaendelea kulizungumza ili mizigo inayokuja Zanzibar kupitia bandari ya Dar es Salaam basi isipate usumbufu; ije zake moja kwa moja kwa taratibu ambazo tumeziweka kwa pamoja. Kama ni nchi moja ni kwamba huu utakuwa ni utaratibu ambao hautaleta tija kwa wafanya biashara wa Zanzibar na wafanyabiashara wa Tanzania bara.
Ni vyema tukawafanya wafanya biashara wakafanya biashara zao kwa ufanisi zaidi ili tuweze kupata ile tija ambayo tumeikusudia.

Lakini la pili, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub ametaka viongozi wakuu wa nchi wakae pamoja ili kuondoa tatizo hili, nataka nimhakikishie tu kuna kamati ya pamoja ya kero za Muungano, ambayo inaongozwa na Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watendaji wakuu wawili; Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamo wa Pili wa Rais, ni wajumbe wa Kamati hiyo.

Wacha nilifikishe kwao kwanza likishindikana wao watakuwa na wajibu wa kulielekeza kwa viongozi wetu Marais wawili. Lakini mimi naamini kwamba nikilifikisha kwao watalifanyia kazi na nitaanza kulifikisha kwa Makamo wa pili wa Rais kwanza.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kuuliza suala moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba atakaa na mwenzake wa Tanzania bara - Waziri wa Fedha wa Tanzania bara kulizungumza suala hili, na alizungumza kwa viongozi wa kitaifa kukaa katika vikao vyao kulizungumza suala hili.

Mimi nataka nimwambie tu kwa kuwa mazungumzo ya suala hili yamekuwa ni ya muda mrefu haoni kuna haja ya kutafuta njia mbadala kutatua tatizo hili?

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Kukwama kwa makontena na mizigo ya wafanya biashara wa Zanzibar pale Dar es Salaam ni jambo jipya na hili ndilo ambalo Mheshimiwa Jaku alinitaka tuanze kulitatua, ili mizigo ile itakapokuja kutoka nje kwa ajili ya Wafanya biashara Zanzibar isikwame pale Tanzania bara.

Kero nyengine zinazoendelea zipo zinaendelea na tunajaribu kuzizungumza lakini kwa hili ambalo nimekuwa nimemjibu Mheshimiwa Jaku, ni jambo ambalo limeibuka hivi kribuni na tumeanza kulitatua. Tumelifanyia kazi yeye ni shahidi; kulikuwa na makontena kule yalikuwa yamekwama tukaingilia kati Makontena hayo yamekuja Zanzibar. Kwa hivi sasa ni jambo jipya limeanza kuongeza kero za muungano.

Kwa hivyo, kama nilivyosema kwamba nitajaribu kukaa na wenzangu ili tuweze kuona kwamba tunalitatua tu tusiongeze zile kero za Muungano. Sasa na haya mengine ya zamani tutaendelea kuyazungumza ili kuweza kuyatatua, kwasababu kila tukiendelea sisi ni binaadamu, tuko *dynamic,* matatizo yatakuwa matatizo yatakuwa, lakini tutafute njia za kuyapunguza matatizo yetu.

**Mhe. Subeit Khamis Faki**: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza suali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Mheshimiwa Waziri ni mazuri sana lakini mtu hujifunza kutokana na makosa ya nyuma yanayotokea. Wafanya biashara wetu wa Zanzibar kulipa mara mbili, halafu wakifika kule wakalipa tena kama mfano wa kukomolewa, tulipofuatilia mimi nimefuatilia pamoja na wewe Mhe. Mwenyekiti, tulikwenda Tanzania Bara mimi na wewe kwa sababu nilikuwa na gari yangu mimi mwenyewe binafsi, lakini tatizo walilotueleza watu hao wa TRA Bara, walitueleza nyie mnakaa viongozi mnazungumza mkishamaliza mazungumzo lile mnalofikia mnasema tu kwenye redio, lakini hamuwapi kwa maandishi.

Sasa je, Mheshimiwa Waziri baada ya mazungumzo yenu mtakapofikia muafaka mtafanya vipi ili kuwapa maandishi watu wa TRA, ili waone kama suala hili limepata ufumbuzi, wasije wakarudia tena, kama mnazungumza ya kawaida tu hatimae mkayaacha kwenye meza.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** TRA ni watekelezaji waamuzi na waongozaji ni Mawaziri wanaosimamia sekta husika, wajibu wangu ni kumuandikia Waziri muhusika Wizara ya Fedha na yeye ana wajibu vile vile wa kuwaita watu wake wa TRA walioko Tanzania Bara, na mimi kama kawaida yangu watendaji wa TRA mara kwa mara nakaa nao na kama kutakuwa na ulazima basi wa kuweka rekodi ya maandishi basi nitafanya hivyo.

**Nam. 124**

**Kodi ya Mafuta Kupelekwa Wizara ya Afya**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Aliuliza **:-**

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijauliza suala ambalo katika masuala mengi niliyoleta Baraza la Wawakilishi limenipa uchungu na hisia na limenikosesha usingizi hata wakati mwengine kula kwa baadhi ya wakati ni hili, naomba nifanye marekebisho Serikali kwa nia njema ilianzisha uchangiaji wa shilingi 30 badala ya 30 tukasema tuweke 100.

Serikali kwa nia njema ilianzisha uchangiaji wa Shs. 30/- kwa kila mwananchi anaenunua na kutia mafuta ili kuweza kuboresha miundombinu ya barabara zetu.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa fedha hizo kupelekwa Wizara ya Afya, ili kuweza kusaidia Bohari Kuu katika suala zima la upatikanaji wa dawa.

(b) Ni kweli Serikali hawajaliona tatizo hilo mpaka kufikia Mwakilishi kuleta suala hilo Barazani.

(c) Ni kipi bora katika maisha ya mwanadamu ama barabara au maisha yake.

**Mhe. Waziri wa Fedha – Alijibu** :-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 124 lenye kifungu (a), (b) na (c), kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Serikali inatoa shilingi mia moja (100/-) kwa kila lita ya mafuta ya Petrol na Disel inayonunuliwa na mwananchi na sio shilingi thalathini (30/-) kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Muwakilishi. namshukuru Mheshimiwa Muwakilishi amefanya masahihisho sasa hivi. Fedha hizo ni kwa ajili ya kuimarisha miundo mbinu ya barabara zetu.

Aidha, katika kuimarisha huduma za afya, Serikali inaongozwa na Dira ya Maendeleo 2020, *MKUZA* II pamoja na malengo ya Melenium.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha afya za wananchi zinaimarika, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuongeza vituo vya afya na kuvipeleka karibu zaidi kwa wananchi kwa lengo la kuwapatia huduma kwa urahisi zaidi.
(ii) Kulifanyia matengenezo Bohari Kuu la Madawa.
(iii) Kuongeza bajeti ya ununuzi wa madawa kutoka Tshs. Bilioni tatu (3) mwaka 2012/13 hadi Tshs. Bilioni 4.2 mwaka 2013/2014
(iv) Kukiimarisha Chuo cha Afya kilichopo Mbweni ili kiweze kutoa wahudumu wengi zaidi na walio bora.
(v) Kuongeza kwa fedha zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya wagonjwa wanaokwenda nje kutibiwa, kutoka shilingi Tshs 833,000,000/= mwaka 2011/12 hadi Tshs 1.8 bilioni 2012/13 na kufikia shilingi bilioni 2.8 mwaka 2013/2014.
(vi) Serikali kuanzisha Mfuko maalum wa Afya kwa Wilaya kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma za afya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa kwa heshima kubwa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti**,** Serikali inaona umuhimu mkubwa wa kuimarisha sekta ya afya ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa dawa na ndio maana inatumia fedha nyingi kila mwaka kwa ajili ya kuimarisha sekta ya afya.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Mwakilishi wa Wananchi ni wajibu wake wa kikatiba wa kuiuliza Serikali, ili yeye mwenyewe na wananchi wake wapate majibu muafaka kutoka Serikalini. Hata hivyo, Serikali imeona umuhimu wa afya kwa wananchi wake tokea mwaka 1964 na ndio maana gharama kubwa ya afya ya wananchi inabebwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub kwa kuiuliza Serikali.

(c) Mhe. Mwenyekiti, naomba ifahamike kuwa maisha ya mwananchi ni mjumuisho wa mambo mengi ikiwemo afya, makaazi pamoja na miundombinu. Ili maisha ya mwananchi yaweze kuwa bora na kuimarika siku hadi siku, huduma zote hizo zinahitajika. Hivyo, Mhe. Mwenyekiti, barabara ni sehemu ya maisha ya mwanadamu na ndiyo maana inahitajia kuwa na barabara zilizo bora zaidi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kwa dhati kabisa katika Mawaziri waliokuwa makini kwa ahadi kwa kuzifuatilia sio kwa mdomo tu na kwa vitendo, nimeshuhudia ahadi tatu Waziri huyu kuzifuatilia, nikupongeze kwa dhati na kuna msemo unaosema wala sio matusi, mgema akisifiwa tembo hulitia maji.Kwa hivyo naomba uendelee na uzi huu huu baada ya maelezo hayo nikuulize suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la ukosefu wa dawa limeongezeka zaidi katika kipindi cha muda mrefu, tatizo hilo limetokana na nini, na ukweli kama ulivyozungumza kutakuwa na kuzuia Miswada ya kibajeti tangu kutokea tatizo la ubadhirifu wa fedha za *ESCROW account* nini ukweli juu ya tatizo hili.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub na nitajitahidi mgema akisifiwa tembo hulitia maji, nitajitahidi nisilitie maji.

Mahitaji ya dawa yanaongezeka siku hadi siku na hii ni kwa sababu idadi yetu tunaongezeka siku hadi siku, kuongezeka kwa idadi ya watu hakuendani na ongezeko la fedha ambazo tunazoziweka kwa ajili ya matumizi ya madawa. Nataka niwambie tu Mhe. Jaku Hashim Ayoub tutashirikiana na Sekta ya Afya tuweze kuona kwamba na sisi mwaka hadi mwaka tunaongeza mahitaji ya dawa katika hospitali zetu pamoja na vituo vyetu vya afya kwa kuongeza bajeti ya madawa.

Mhe. Jaku, ametaka kujua kuhusu habari ya masuala ya *Escrow Account* na matatizo yametokea Tanzania Bara sote tumeyasikia, sisi Zanzibar hayatuhusu. Wafadhili wamesimamisha misaada yao kwa sababu ya tatizo hilo na wamesimamisha pia mpaka Zanzibar, ingawa sisi halituhusu. Lakini tunaendelea kuzungumza na wafadhili kupitia kwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje pamoja na Waziri Mkuu. Matumaini yangu na matarajio yangu kwamba suala hili kwa kuwa limekwisha basi wataruhusu fedha zao, ili zije katika maendeleo ya nchi yetu.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri wa Fedha swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri fedha hizi zinazotozwa shilingi 100/= kwa kila *litre* ya mafuta mwananchi anaponunua, nia yake ni kuongezea miundombinu ya barabara. Sasa namuuliza swali Mhe. Waziri.

a) Mnakusanya kiasi gani cha fedha hizi kwa mwaka makadirio yenu mnayokusanya.

b) Je, hizi fedha zikishakupatikana zinakarabatiwa barabara au zinajengewa barabara. Kama zinajengewa barabara, zinajengewa kwa kiwango cha lami au ni kwa kifusi. Kama ni kwa kifusi hatuoni kama kifusi baada ya mwaka mmoja tu kinaondoka na tunatumia fedha hizi mara kwa mara, si bora kujenga barabara hata kama ni moja lakini ikawa ya lami ili fedha hizi tukazitumia vizuri.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, Makisio ya fedha kwa ajili ya matumizi kwa mfuko wa barabara yanategemeana na makisio yanayotokana na uingizaji wa mafuta ambao mwananchi mmoja mmoja anatumia katika shughuli zake mbali mbali.

a) Katika mwaka huu makisio yetu tunatarajia kuwa bilioni nane.

b) Mhe. Mwenyekiti, kazi ya fedha hizi ni kukarabati barabara. Lakini mfuko umeruhusiwa kujengwa barabara kwa kiwango cha lami isiyozidi kilomita moja. Hata hivyo pale ambapo wanapoanza kwa kiwango cha kifusi lengo na nia ni kuiwekea lami katika siku za baadae.

**Nam. 86**

**Mpango wa Kusafirisha Wagonjwa Tanzania Bara**

**Mhe. Ali Salum Haji –** Aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya Muhimbili wameanzisha tiba za mafigo na moyo na kuanzisha upasuaji wa kisasa wa tundu ndogo.

Je, Wizara ina mpango gani wa kupeleka wagonjwa hao Tanzania Bara badala ya kuwapeleka nje ya nchi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya -** Alijibu:-

Asante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaaliwa kuwa tumeamka, wenye afya na uzima.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 86 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida utaratibu wa Rufaa kwa Wizara ya Afya ni kuwapeleka wagonjwa katika hospitali ya Rufaa iliyo karibu nasi kwanza kabla ya kwenda kwengine kokote. Hospitali hiyo ya Rufaa kwa kwetu hapa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Hospitali ya Muhimbili. Wagonjwa wanapelekwa kwa huduma ambazo hazipatikani hapa kwetu Zanzibar. Kabla ya kupelekwa wagonjwa hao kwengine kokote basi huanzia pale Muhimbili na hapo hupata rufaa nyengine ambayo Bodi ya Madaktari huikalia na kuamua wapi kwengine kwa kupelekwa kwa zile huduma ambazo hazitolewi pale Muhimbili.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Muhimbili ndiyo ambayo Wizara imefugiana nayo mkataba rasmi kwa kuwapeleka wagonjwa wetu wote wa rufaa kwanza. Aidha, wagonjwa wengine huenda nje ya nchi moja kwa moja kwa pesa zao wenyewe binafsi pasi na kupitia utaratibu maalum wa ushauri wa Bodi ya Madaktari ambayo ipo chini ya Wizara ya Afya, utaratibu ambao umewekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Bodi ya Madaktari walioteuliwa ndio wenye mamlaka ya kuamua mgonjwa kupelekwa Rufaa ya Muhimbili kwanza na baada ya kupata majibu hayo Bodi hiyo hiyo huamua apelekwe wapi mgonjwa huyo. Hata hivyo, kuna baadhi ya Wafadhili ambao wanawapatia msaada wa matibabu katika nchi zao moja kwa moja wagonjwa hao mfano Israel na India basi wao huwa na taratibu maalum ya kuomba kupitia kwa wawakilishi wa nchi hizo hapa Zanzibar.

**Mhe. Nassor Salum Ali:** Asante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Katika majibu yake mama Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba mbali na wale ambao wanapata fursa ya kwenda kufanya matibabu nje ya nchi kwa uwezo wao wenyewe, lakini kuna wafadhili ambao husaidia kuwapeleka wananchi katika matibabu haya.

a) Je, niwafadhili gani ambao husaidia wananchi wetu kuwapeleka katika matibabu hayo.

b) Na ni wangapi ambao hupata kupelekwa katika matibabu kwa mwaka.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba wafadhili hawa huwa wanakuja mara kwa mara na hubadilika kila mwaka. Kwa hivi sasa wafadhili tuliokuwa nao ni *Lions Club* ya Tanzania ambayo huchukua wagonjwa mara nyingi wa matatizo ya moyo, *(Save a Child Hearts)* hii ni Jumuiya isiyokuwa ya kiserikali kutoka nchini Israil inaitwa *(Save a Child Hearts)* yaani "Okoa Moyo wa Mtoto". Wao pia huwa wanachukua watoto wadogo wenye matatizo ya moyo kwa wingi sana.

Mara nyingi Zanzibar huwa inapata nafasi zaidi ya 30 mpaka 40 kuwapeleka watoto hao kwenda kupata matibabu ya moyo.

Pia, zimekuwepo Jumuiya nyengine za watu binafsi kina Shekhe Suleiman Yahya Al-Alawi pamoja na Jumuiya yake kutoka Oman ambayo pia imeshawahi kutoa misaada mbali mbali katika kuwapeleka wagonjwa nchini India kwenda kupata matibabu. Kwa hivi sasa ni Jumuia hizo tatu ambazo tunafanya nao kazi kwa karibu sana, lakini kila baada ya muda hutokezea Jumuia mbali mbali kuangalia makundi mbali mbali ya wagonjwa, hususan watoto na hususan huwa wanatizama maradhi ya moyo zaidi. Asante.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi kuuliza angalau swali moja dogo sana la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Zanzibar ni nchi na kwa kuwa tunayo hospitali yetu ya Mnazi Mmoja ambayo karibuni tukijaaliwa bi-idhini Lahi, tunategemea iwe Hospitali ya Rufaa. Na kwa kuwa *SUZA* sasa hivi kwa mujibu wa maelezo tuliyopewa tayari wameanzisha *faculty of medicine,* jambo ambalo tunaweza tukazalisha madaktari wengi sana katika fani mbali mbali ikiwemo hiyo ya *curdiac* na mambo mengine huko.

a) Je, ni sababu gani za msingi ambazo hadi leo hii hatujaleta hichi kitengo cha mambo ya figo na moyo pale Mnazi Mmoja na badala yake kutegemea vijinchi vyengine kupeleka wagonjwa wetu.

b) Kuendelea kuwapeleka wagonjwa wa moyo katika Hospitali za nchi za jirani wakati Hospitali ya Muhimbili tunayo pale, huku si kurudisha nyuma Wazanzibari na kuteremsha thamani ya nchi hii.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Asante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimfahamishe Mhe. Pamoja na Waheshimiwa wote kwamba katika digirii zote duniani, shahada iliyokuwa ghali kuliko zote ni shahada ya *medicine* hata *masters,* katika *masters* zote ulimwenguni basi *masters* ya *medicine* ni ghali zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa aelewe kwamba gharama za kuendesha kozi hizo za *medicine* ni kubwa sana na mpaka sasa hivi Zanzibar ina fahari ya kuzalisha watoto au vijana 40. Madaktari wetu wenyewe ambao kwa mara ya kwanza kabisa wamesoma hapa Zanzibar na kufaulu mitihani yao na sasa kuwa madaktari ambao wanafanya kazi kama *intern* katika hospitali zetu mbali mbali na wengine wanafanya *intern* katika Hospitali, ambazo zipo nje ya mji pamoja na hizo alizozitaja Mheshimiwa kama Muhimbili wapo, KCMC na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, pili ni kweli hii kozi nzima ya *Matanzas University of* Cuba imehamishiwa kule SUZA hivi sasa. Uwezo uliokuwepo wa kuendesha *faculty* ni kati ya wanafunzi 40 na 50 kwa mwaka, bado haujapatikana uwezo wa kufanya *full leg pecult* ya *madicine,* kwa hivyo bado uwezo wetu uko hapa. Lakini *ratio* hii ya madaktari 40 mpaka 50 inapunguza sana takwimu za mahitaji ya madaktari Zanzibar, yaani *ratio* ya madaktari kwa wagonjwa inaongezeka kwa kiwango kikubwa sana kwa hawa 40, kila wakimaliza mitihani yao. Kozi hiyo naomba niseme kwamba inaendelea na hivi sasa inaendelea vizuri pale SUZA.

Kuhusu suala la Mafigo naomba nitoe taarifa rasmi kwamba mradi wa ORIO ambacho ni kile Kiwanda cha madawa kilichokuwepo pembeni ya hospitali. *ORIO* wanatoa asilimia 50 yaani Serikali ya Uholanzi pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatoa asilimia 50. Mkataba huo Mwenyezi Mungu akitujaalia unatiwa saini mnamo tarehe 11 mwezi wa 2. Naamini kamati ile ya ustawi wa jamii itashirikishwa kikamilifu na kualikwa katika ghafla hiyo ya utiaji saini. Katika kutia saini huko wale watajenga ....... *unit* nzima, yaani magonjwa ya watoto, *unit* nzima itakuwa ghorofa ya kwanza.

Lakini pale chini patakuwa na *unit* nzima kazi yake ni mambo ya *diagnosis* na mambo ya figo.

Tayari tumeshakubaliana nao upande wa mashine, baadhi ya mashine zipo tayari hapa Zanzibar na baadhi ya vifaa vyengine vitakuja. Kwa hiyo *unit* ile itakuwa *at list* baadhi ya maradhi bado hatutoweza kufanya ile *replacement* ya figo zima lakini *at list* mambo ya *diagnosis* na wagonjwa watakuwa hawana haja ya kwenda nje kutibiwa.

Mradi huo utachukua muda wa mwaka mmoja na nusu mpaka miwili kumalizika, kwa hivyo tutarajie mambo ya mafigo tutakuwa tunafanya hapa hapa Zanzibar.

**Nam. 87**

**Huduma za Afya kwa Mtandao**

**Mhe. Ali Salum Haji -** Aliuliza:-

Kutokana na kukua kwa taaluma za I.T wenzetu Tanzania Bara wameanza kutoa huduma za afya kwa mtandao, kuanzia usajili wa wagonjwa, matibabu na uwekaji wa kumbukumbu za wagonjwa.

Je, ni lini Zanzibar tutaanzisha mfumo huo ili kutoa huduma bora na kuweka kumbukumbu vizuri za wagonjwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 87 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu uliopo wa uwekaji kumbukumbu za wagonjwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja ni mfumo wa kutumia majadala *"manual system"*. Kutokana na kukua kwa Teknologia ya habari na mawasiliano (ICT), Wizara ya Afya imeona ipo haja ya kutumia mfumo wa kielectroniki katika kuweka kumbukumbu za taarifa za wagonjwa katika hospitali za Serikali. Matumizi ya kieletroniki yalishaainishwa kwenye Mpango Mkakati wa III wa Sekta ya Afya – *Health Sector Strategic Plan III (HSSP III 2013/14 – 2018/19)* na Mpango Mkakati wa Mfumo wa Taarifa za Afya – *Health Information System Strategic Plan (HISSP 2011/12 – 2015/16).*

Mhe. Mwenyekiti, Wizara tayari imeshafanya upembuzi yakinifu kwa hospitali ya Chake Chake kwa mukhtadha wa matumizi ya kieletroniki. Aidha, hospitali ya Kivunge na Makunduchi wameanza kuweka kumbukumbu za wagonjwa kwenye *computer* ingawa na mfumo wa zamani wa mabuku bado unaendelea kutumika yaani wanatumia *parallel system*.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia mradi wa *e-government phase II,* serikali inakusudia kuwa na mfumo madhubuti na wa kisasa wa usajili. Usajili huo utajumuisha matibabu pamoja na utunzaji wa kumbukumbu za wagonjwa. Hata hivyo, kuna baadhi ya vitengo katika hospitali ya Mnazi Mmoja wao tayari wameshaanza kutumia mifumo yenye kujitegemea ya kielektroniki, vitengo hivyo ni kama ifuatavyo:

- Kitengo cha Macho tayari wana mfumo wao wa kielektroniki ingawa bado wanaendelea kutumia na mabuku kwa sababu wanafanya *parallel system.*

- Maabara kuu wana *system* pale inaitwa *(Laboratory information System – LIS*). Bahati nzuri mimi mwenyewe binafsi nilishuhudia nikenda kusoma pale, mfumo huo unafanya kazi vipi na kama Wawakilishi watakuwa wanakwenda Hospitali watakuwa wanaona kuna *barcode* zinatoka, zinakuwa zinabandikwa kwenye chupa moja kwa moja, siku hizi na kuna *barcode reader,* kwa hiyo huwa zinasomwa moja kwa moja.

- Katika mifumo hii yote ya kielektroniki, mfumo unaoongoza ni wa *laboratory* mpaka hivi sasa. Kitengo cha meno pia na wao wana mfumo wa kielektroniki wanautumia unaitwa *(Easy dental)* na sehemu ya mapokezi ya wagonjwa wa nje, pia wanamfumo wa kuchukua taarifa mbali mbali ya maradhi mbali mbali ambayo huwa inatusaidia sisi kuyafanyia kazi pamoja na wafadhili wetu wa maendeleo ambao wanafuatilia kwa karibu.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutengeneza mfumo shirikishi *(Intergrated)* Wizara imefanya mazungumzo na kampuni tofauti zinazofanya kazi ya uwekaji wa taarifa kwa njia ya kisasa *"electronic medical record system"*. Kampuni hizo:

- Kampuni *Z-TECH*, tayari tumeshafanya mazungumzo nao na Mwenyezi Mungu akitujaalia Ijumaa tunafanya kikao maalum cha kufanya tathmini ya mifumo mbali mbali ambayo imeshawasilishwa.

- Kampuni ya *MESO,* kutoka South Africa.

- Kampuni ya *VECNA* kutoka Marekani,

- *CARE, All see EMR* na;

- *COSEKE* ya hapo Dar-es-Salaam, ambayo wao pia walifanikiwa kufanya mfumo mzuri wa Kielectroniki pale Hospitali Kuu ya Rufaa ya Muhimbili.

  Kampuni hizi zote zina uzoefu katika masuala haya. Aidha, Wizara imefanya majadiliano na WHO ambayo tayari wameonesha nia ya kusaidia katika eneo hili la *"electronic medical record system"* katika hospitali zetu tukianzia na MMH yaani Mnazi Mmoja Hospitali.

  Tunatarajia Mwenyezi Mungu akitujaalia kabla ya Oktoba mifumo hii itakuwa tayari tumeshaiweka kwenye sehemu yake ikiungana na hii mifumo ambayo ipo hivi sasa.

  **Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa maelezo mazuri na jitihada za serikali zinazoenesha kuelekea katika mfumo wa IT.

  Kwa kuwa wenzetu na mfumo wa kimatibabu kuanzia *registration* mpaka matibabu ni mfumo wa mambo ya IT. Lakini pia kuna mfumo mzima wa malipo kwa wale wanaochangia nao kulipa katika mfumo wa kimtandao na wenzetu Tanzania Bara wamefika pahala katika mfumo huo; wamemalizia mpira mpaka wameweka Benki pale ya NMB katika hospitali.

  Je, Wizara yako nayo ina mpango gani wa kuhakikisha kutumia mfumo wa kimalipo katika njia za kimitandao na kuweka Benki kulipia baada ya kulipia hospitali, ili kuweza kubana ile michango ya wananchi inayotolewa ili baadae irudi kuwasaidia wananchi wenyewe.

  **Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Asante Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze kwa swali hilo zuri sana, kwa kweli taaluma yake ameithibitisha maana baada ya kujadili mifumo ya kimatibabu pamoja na mifumo ya kuweka taarifa, hatua ya pili ni mifumo ya kifedha ambayo tunataka kwenda. Kwa sababu sera yetu bado matibabu ni bure. Kwa hivyo hatukuchukua mfumo ule wa fedha uwe mwanzo, tumechukua mfumo wa mwanzo ni matibabu pamoja na taarifa za mgonjwa yaani *patients and medical records system.*

Hatua ya pili ndio hiyo *financial integrated management system* ambayo wenzetu Wizara ya Fedha wameshaanza wao tayari, wapo hatua ya mbele. Tunaweza kuunganisha pia mifumo hii. Inaweza kuungana nao kwa sababu wao baada ya kulipa mgonjwa au kwa zile huduma za *fast-track* au huduma binafsi, kama pale Mapinduzi Kongwe basi fedha zile huwa zinaingia moja kwa moja Serikalini. Hiyo itakuwa ni hatua ya pili baada ya kumaliza hatua ya awali.

Lakini tunayapokea maoni hayo na tutawachukua wenzetu hawa mabenki mbali mbali ambao na wao tayari wana mifumo yao tuwakaribishe ili siku moja na wao wawekeze pale hospitali. Tukiona kuna ATM tofauti au mashine tofauti za mabenki ambapo wagonjwa wanaweza kupata huduma moja moja pia za fedha si jambo baya ni jambo zuri sana.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini vile vile nimuombe sana alipokuwa akijibu swali la msingi aligusa hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo ni hospitali ya kimbilio la wanyonge wengi. Mheshimiwa kabla ya kutafuta makubwa ningekuomba kabisa ni lini

utakagua vyoo vya hospitali ya Mnazimmoja kuona hali halisi kutokana na vyengine *bulb* havina, na vinasababisha hatari kujigonga watu kwenye ukuta.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nilithibitishie Baraza lako tukufu wewe Mwenyekiti pamoja na wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi kwamba jana na juzi zote mbili hizo na ushahidi upo na wafanyakazi wa hospitali wanajua tulikagua vyoo na vyote viko katika hali nzuri. Sasa ninachokuomba Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu lilikuja suala la *X - Ray* jana mimi pamoja na Katibu Mkuu pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali tumekwenda kuzipitia *X - Ray* zote pamoja na zile *TB Unit* na mimi mwenyewe nilijitolea pia nipigwe *X - Ray* ya kifua ili niangalie kifua changu kiko katika hali gani, zote hizo zinafanya kazi.

Taarifa zinazotolewa zinakuwa si sahihi, wakati mwengine kama *film* imekwisha taarifa inatoka hapa kwamba *X - Ray* haifanyi kazi. Kwisha kwa *film* na kufanya *X - Ray* kazi ni masuala mawili tofauti. Ni sawa sawa na *printer* kuisha *tonner* haina maana ile *printer* haifanyi, inatakiwa mtu uchukuwe *tonner* ubadilishe ifanye kazi.

Kwa hivyo ninachokuomba Mhe. Mwenyekiti, ili kumridhisha na mjumbe namualika tufanye ziara mimi na yeye Mhe. Jaku kwenye vyoo vyote, tuchukuwe na *camera* zetu tupige picha ili aweze kuthibitisha wapi hapafanyi kazi, wapi panafanya kazi na pale tutakuwa na uongozi wa hospitali nitauchukua, Katibu wa Hospitali atakuwepo na Mkurugenzi Mkuu Mnazimmoja nitahakikisha yupo na Katibu Mkuu wa Wizara ili hizi taarifa ziwe zinatoka kwa usahihi kabisa. Lakini jana nilipotembelea mpaka *maternity* nilikwenda jana na vyoo vya huko niliingia mimi mwenyewe viko katika hali nzuri na visafi.

**Nam. 26**

**Bwawa la Kumwagilia Bonde la kinyakuzi**

**Mhe. Salma Moh'd Ali -** Aliuliza:-

Katika bonde la Kinyakuzi kuna bwawa la uhifadhi wa maji ya umwagiliaji, kwa bahati mbaya bwawa hilo baadhi ya siku humwaga maji na kuwaharibia wakulima kilimo chao.

Je, Serikali inalijua suala hili na Waziri ameshawahi kwenda kuwatembelea, na kuna hatua zozote zilizochukuliwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Salma Mohammed Mwakilishi wa Viti Maalum swali lake namba 26 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Bwawa la Kinyakuzi ni la zamani na linahitaji matengenezo makubwa. Bwawa hili lilifanyiwa matengenezo mwaka 2009 kupitia fedha za mradi Shirikishi za Uwezeshaji wa Maendeleo ya Kilimo PADEP. Karibu na kingo za bwawa hilo pana miti na mizizi yake imepitia katika kingo hizo inapasua na kuacha mianya ambayo hupitisha maji.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inalifahamu suala hili, kwani uongozi wa Wizara ya Kilimo na Maliasili nikiwemo mimi mwenyewe Naibu Waziri, Mkurugenzi wa Umwagiliajimaji na Wahandisi na viongozi mbali mbali wa Wizara walitembelea bwawa hilo kwa azma ya kuona na kufahamu tatizo liliopo. Aidha, kinachohitajika ni kulijenga upya tuta hilo kwa kulisogeza mbele ya hapo lilipo ili kuikimbia mizizi ya miti iliopo karibu yake ambayo husababisha matundu yanayovujisha maji, kuongeza kina cha tuta kufikia mita moja na nusu na urefu wa tuta kufikia mita 30.

Wizara inatarajia kulimaliza tatizo hilo wakati wowote pale hali ya fedha itakaporuhusu.

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa nyuma ya Bwawa hilo kuna wakulima wanaolima na kwa kuwa wakulima hao hupata hasara kubwa kwa kuingiliwa na maji katika mashamba yao pale linapojaa bwawa hilo. Je, Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima hao kwa kuwapa konde nyengine.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ni kweli katika bwawa hilo nyuma kuna wakulima ambao wanalima na wanaathirika na maji na maji huathirika wakati wa mvua zinapokuwa nyingi na bwawa lile linapofungwa wakati watu wa mbele hawatumii maji yale, maji yale hupanda nyuma na kuathiri. Mhe. Mwenyekiti, konde za kilimo cha umwagiliaji maji tofauti na konde za juu. Konde za kilimo za umwagiliaji maji kila mmoja anamiliki pahala pake natulipokwenda katika ziara kulifatia suala hili kuna baadhi ya watu ambao walikuwa wakilima pembeni humu hao wameondoka. Lakini kuna baadhi ambao hao waliokuwa wakilima nyuma kila mmoja kamiliki anapolima ni hapo hapo kuondoka mwenyewe hataki, hili linakuwa tatizo.

Tatizo la kulitatua wakulima hawa ni kuujenga ule ukuta kwa sababu maji yanapopanda yanakiuka tuta la pili ambalo yanaingia sehemu ya konde za nyuma. Ni kujenga huu mtaro wa tuta ili wapate kunufaika wale waliokuwa nyuma wanaingiliwa na maji.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii na mimi napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali lifuatalo. Kwa kuwa amekiri kuwa bwawa hili linavujisha maji na linatoa maji hasa mvua inapokuwa kubwa na kuharibu mazao ya wakulima wa eneo hili. Je, Mheshimiwa ni mara ngapi mumetoa ushauri kwa wakulima hawa juu ya kadhia hiyo.

(b) Ni kiasi gani cha fidia ambacho mumewafidia wakulima hawa baada ya kuharibikiwa na mazao yao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Mwenyekiti, ushauri wa suala hili ambalo la kuharibikiwa mazao mimi mwenyewe nilipofanya ziara nimekwenda nikakaa na wakulima tukatoa ushauri, ambao wanaharibikiwa na maji haya tukakaa na wataalam pamoja na nina imani na bado unatolewa ushauri kwa sababu hili tatizo lipo ni tatizo endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu fidia bado hapajatolewa fidia kwa sababu huu uharibifu unapokuja kutokana na suala hili hatujapata rasmi kwamba kuna watu ambao wanaharibikiwa total, kwa sababu tatizo la pale linapokuja baadhi ya maji yanapojaa. Maji yale yanapojaa na hufungwa lile bwawa lina milango yake, yanapofungwa yanapomwagika upande wa pili endapo hawa huku hawayataki yale maji ndipo linapotokea lile tatizo, hatujapata tathmini hasa kwamba kuna watu ambao wameharibikiwa *totally* na vipando vyao.

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kunisaidia kunipa nafasi hii na mimi nikauliza swali moja lenye (a) na (b) la bwawa hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa bwawa hili la Kinyakuzi ni bwawa linalotegemewa na wakulima wengi wa bonde hilo, lakini wakati wa kipindi kama hiki cha Kaskazi maji yake yanakuwa ni madogo sana hayawatoshelezi wakulima kuweza kumwagilia vizuri vipando vyao. Je, Wizara yako italiondosha lini tatizo hili kwa sababu wakulima wanasema mbele yake kuna kijiinuko kwa hivyo Kaskazi maji hayendi vizuri. Je tatizo hili Wizara yako italiondosha lini.

(b) Kwa kuwa bwawa hili katika mazingira lilipo hili bwawa linakuwa wakati wa masika kama ulivyoeleza kama maji yake hujaa na kweli na limefanya nyufa nyingi na kukatika na maji yakaingia katika vilimo vya wakulima wengine. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri utawaambia nini wakulima walio katika maeneo hayo kuepukana na kadhia hiyo. Lakini kama ulivyosema kwamba Wizara yako imo katika kulitatua ni lini hasa maana bado hatujapata jawabu rasmi kwamba muda fulani tatizo hili litatuka.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kipindi kama hiki bwawa pana kilima ambacho kinachosababisha maji yale hayendi na hicho kijilima ni moja katika hilo tatizo ambalo linasababisha kuwa maji hayo hayendi. Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili tumeliona na tatizo hili ambalo ni kitu ambacho kimoja kinachukua pamoja jumuiko ya hilo bwawa lenyewe, tumesema kwamba katika bajeti inayokuja kwa sababu kazi ya pale si ndogo ni kazi kubwa, tatizo huondoka kwa kujengwa tena lile bwawa.

Bajeti inayokuja tutazingatia mpango huu ili kuondosha lile tatizo na wakulima wa pale tunawaambia wafanye subra kwa hili. Kuna tatizo linaweza kuondoka kwa macho, kuna tatizo haliwezi kuondoka kwa kuona linaondoka kwa fedha kwa hivyo sisi tutakapolitia katika bajeti tukipata fedha ndipo tutakapoondosha tatizo hili.

**Nam. 56**

**Utafiti wa Samaki Bahari ya Hindi**

**Mhe. Saleh Nassor Juma -** Aliuliza :-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara inayohusiana na mambo ya uvuvi, imefanya tafiti za kina katika kujua kiwango cha maji na aina mbali mbali za samaki wanaopatikana katika maeneo tofauti ndani ya Ziwa Nyasa, tafiti ambazo zimesaidia sana kuongeza kipato kwa wavuvi wadogo wadogo pamoja na kuchangia uchumi wa nchi.

Kwa kuwa Wazanzibari walio wengi wamewekeza katika sekta ya uvuvi na kwa kuwa bahari ya Hindi ina samaki wakubwa na wengi zaidi ukilangnisha na ziwa Nyasa.

Je, ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafanya tafiti kama hizo ili wavuvi wadogo na wakubwa waweze kujiongezea kipato pamoja na kupunguza umasikini.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mwakilishi wa kudumu wa Jimbo la Wawi Mhe. Saleh Nassor swali lake nambari 56 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeshafanya tafiti katika miaka ya nyuma za kutambua aina na wingi wa samaki na maeneo yao wanaopatika. Hata hivyo, tafiti hizo zinahitaji kufanyiwa mara kwa mara kupitia mradi wa *Swiofish* unaotarajiwa kuanza Machi, mwaka huu Wizara yangu imekusudia kufanya utafiti wa kujua wingi wa samaki hasa wale wanaohama kutokea nchi moja kwenda nchi nyengine pamoja na aina nyengine mbali mbali za samaki. Tafiti hizi itawezesha wavuvi kujua maeneo muhimu yenye samaki wengi zaidi na wawekezaji kuweza kuwekeza katika sekta hii kwa lengo la kujiongezea kipato na kusaidia uchumi wa nchi hii.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Serikali ndio kwanza ina mpango wa kufanya tafiti na kwa kuwa wavuvi wa Vitongoji, Jambiani, Kiwengwa, Makunduchi bado wanaendelea kuvua samaki wengi sana na hulazimika kuvua samaki katika kile kipindi cha *season* ya Kaskazi wanavua kwa wingi sana kiasi ambacho soko linajaa na kulazimika kuwauza kwa bei ndogo sana, ambayo na kuwaongezea kipato lakini hakiwapunguzii umaskini vile vile.

Sasa swali, wakati tafiti bado hazijafanyika je, ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein itaweza kujenga *marketing board* ya kuweza ku-*stabilize* bei ya wale samaki na hatimaye wavuvi hawa wakaweza kupanga ule mpango wa MKUZA wa kujiongezea kipato na kujipunguzia umaskini.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein katika ziara yake ya juzi ya kwenda Comoros ilihakikisha moja kuweza kuzungumza na wadau wetu na kuanza kujenga kiwanda kikubwa hapa, ili kuweza kuwafaidisha wananchi wa Zanzibar kuweka bei na watauza pale pale kwenye Kiwanda cha kusindika. Na hata hivyo MMU tayari inakaribia kuwekwa *sign* kwa hivi sasa.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri, swali langu dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inafanya jitihada za kuhamasisha wavuvi na kuandaa miradi mbali mbali na wavuvi wameanza kuhamasika na wanavua sana lakini zao la samaki ni zao ambalo haliwezi ku-*survive* kwa muda mrefu katika mazingira ya kawaida.Na Serikali yetu imejitahidi kuweka *cold room* ya kisasa pale Malindi lakini tulisikia fununu kwamba kuna jitihada nyengine za kuweka *cold room* nilitaka kujua tu, ile *cold room* ambayo ilikuwa inatarajiwa kujengwa upya na ya kisasa pale Malindi iko katika hatua gani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Mwenyekiti, nasema tu mradi huu tunataraji Machi utaanza kazi kujengwa katika diko lile kubwa na vifaa hivyo ulivyovitaja ni moja kati ya Serikali iliyovitilia mkazo, na suala hilo litaweza kuondoka mara tu baada kukamilika ujenzi ule na ujenzi utachukua miezi minane.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kama wamefanya utafiti na anategemea kwamba mwaka huu kuendelea kufanya tena utafiti. Na kwa kuwa nchi yetu ina samaki katika bahari, kuna samaki wengi ambao wanahitaji kufanyiwa kazi, na kwa kuwa bahari inaweza ikaongeza kipato katika nchi yetu na kutoa ajira zaidi pamoja na kuwa ipo kwa wananchi wetu. Mheshimiwa na kwa kuwa bajeti zilizopita zote Mheshimiwa walitwambia kwamba wanataka kuanza uvuvi wa bahari kuu na akatuahidi kama wanataka kuanza kwa boti mbili za majaribio. Na pia tuliahidiwa kama wanataka kujenga kiwanda cha kuzalisha boti hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, namuuliza Mhe. Naibu Waziri ni lini hasa wataanza uvuvi wa bahari kuu ili wananchi wapate ajira. Na je, ule mradi wa kujenga maboti umekufa au bado upo, na je, ni lini watasaidiwa wavuvi wetu wa Kojani, Micheweni ambao kwamba wanazalisha zaidi samaki hasa ukilinganisha katika upepo wote wa Kaskazi mwaka huu wametoa samaki wengi zaidi, ni lini watawasaidia wavuvi hao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Mwenyekiti, nimezungumza katika jibu langu la msingi kuwa serikali hii inayoongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein ilifanya ziara kule Comoros na kuweza kuzungumza na wadau mbali mbali. Moja katika hayo tulizungumza na haya maboti ili tuweze kupata nchini Sri Lanka, lakini vile vile serikali imechukua muda mrefu ilikuwa sio kupata bora boti, lakini tulikuwa tunasema tupate boti imara na za kuwezesha katika kipindi kirefu. Sasa mipango hii baada ya mazungumzo kukamilika mara tu tutaweza kufanya hivyo vitu na havitokuwa na muda tena kwa sababu tayari *MOU* imeshatiwa saini na tunategemea wakati wowote tunaweza tukaanza.

Lakini kuwasaidia wananchi hawa wa kwake aliosema serikali imejitahidi kwa kupitia mipango mbali mbali, lakini kitu kinachoonekana nacho hata wavuvi wakisaidiwa wanataka kusaidiwa tena, lakini kama wizara itakuwa na nafasi na uwezo utaruhusu basi tutaweza kuwasaidia baadae.

**Nam. 27**

**Uteuzi wa Mawaziri na Watendaji Wakuu**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub –** Aliuliza:-

Uwajibikaji wa Serikali yoyote duniani unategemea kuwepo viongozi na watendaji wenye sifa na uwezo wa kufanyakazi hasa katika kusimamia suala zima la uwajibikaji. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imekuwa ikipata viongozi wake na bado maeneo mengi ya utendaji yamekuwa na mapungufu ya kiutendaji na uwajibikaji.

(a) Je, Serikali inatumia vigezo gani vya kuchagua mtu kuwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu au Mkurugenzi.

(b) Kama sifa na vigezo vinazingatiwa katika kufanya uteuzi wa viongozi hao kwa nini upatikanaji wa huduma kwa wananchi umekuwa na mashaka na kusababisha malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wa Unguja na Pemba.

(c) Kwa nini suala la uwajibikaji katika Ofisi za Umma linaendelea kuzorota na kusababisha malalamiko kutoka kwa wananchi, watendaji wakuu wakiwemo na viongozi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma** – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 27 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya hapo nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza yeye pamoja na muasisi, kwa kweli wanalifanya Baraza letu lijiandae kwa maswali kila siku.
Pili naomba sasa kuchukua nafasi hii kutoa kwanza kabla ya kujibu swali lake Mhe. Mwakilishi jirani yangu Wilaya ya Kusini.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba uwajibikaji wa serikali nyingi duniani unategemea kuwepo kwa viongozi na watendaji wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi ili waweze kusimamia ipasavyo uzalishaji na utoaji wa huduma kwa wanachi. Hata hivyo, sikubaliani na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba bado maeneo yetu mengi ya utendaji yamekuwa na upungufu wa kiutendaji wa uwajibikaji.

Ukweli wa mambo ni kwamba serikali imepiga hatua kubwa sana katika kuandaa na kutekeleza mipango ya kitaifa na kimataifa, na kuweka mifumo mbali mbali ya kuhimiza na kuendeleza utendaji na uwajibikaji katika sekta ya umma. Miongoni mwa mipango hiyo, ni pamoja na mpango wa pili wa kupunguza umasikini (MKUZA II), malengo ya Milenium, Sera ya Utumishi wa Umma, Miundo ya Utumishi, Mipango Mkakati, Mipango Kazi na kadhalika. Ufuatiliaji uliofanywa wa mipango na mifumo hiyo unadhihirisha wazi kwamba utendaji na uwajibikaji wa taasisi zetu umeongezeka zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba sasa kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 27 kama ifuatavyo:-

a) Kwa mujibu wa vifungu nambari 42, 47, 50 vya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 (Toleo la 2010), Mamlaka ya uteuzi wa viongozi katika ngazi za Mawaziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu iko moja kwa moja chini ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, mamlaka ya uteuzi kwa Mkurugenzi pia iko chini ya Mhe. Rais kama vifungu nambari 53(a) na (b) vya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 (Toleo la 2010) na vifungu nambari 54 (1), (5) na (6) vya Sheria ya Utumishi wa Umma nambari 2 ya mwaka 2011 vinavyoagiza.

Katika kuifanya kazi hiyo, na kwa mujibu wa Katiba, Rais anateua Waziri kutokana miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kwa kuzingatia uwiano wa viti vya majimbo, wa vyama vya siasa vilivyomo ndani ya Baraza la Wawakilishi. Uteuzi wa Naibu Waziri nao unafanywa na mamlaka ya uteuzi kwa kushauriana na Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa uteuzi wa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Mkurugenzi, pamoja na kwamba uwezo wa kitaaluma na uzoefu wa utendaji unazingatiwa, lakini bado uteuzi wa watendaji hawa ni maamuzi ya Mamlaka ya Uteuzi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ni kweli kwamba sifa na vigezo vinazingatiwa katika kufanya uteuzi wa viongozi hao kwa mujibu wa Katiba na Sheria zilizopo. Kwa hivyo, si sahihi kusema kwamba upatikanaji wa huduma kwa wananchi umekuwa na mashaka. Katika hili, serikali haina taarifa ya malalamiko hayo ambayo Mhe. Mwakilishi ameyataja kutoka kwa wananchi wa Unguja na Pemba. Naomba kumshauri Mhe. Mwakilishi tukutane ili anipatie hayo maeneo ambayo upatikanaji wa huduma umekuwa wa mashaka na malalamiko, kwa ufuatiliaji zaidi na kwa hatua zinazofaa.

(c) Kama nilivyoeleza katika jawabu langu la (b) si sahihi kusema kwamba uwajibikaji katika Ofisi za Umma unazidi kuzorota. Napenda kusisitiza tena kwamba ofisi yetu haina taarifa hizo za uzorotaji wa utendaji. Bado naomba Mhe. Mwakilishi tushirikiane ili atupe taarifa maeneo gani ambayo yamezorota na tuchukue hatua za kufaa.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza niendelee kumshukuru Mhe. Waziri kwa kuliona hilo baada ya rafiki yangu Mhe. Saleh Nassor Juma Mwakilishi makini wa Jimbo la wananchi la Wawi nikiwemo mimi Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni kwa kuuliza maswali mengi Barazani. Nikushukuru sana Mhe. Waziri kwa hilo na niombe Mawaziri na Manaibu Waziri huu ni wajibu wetu kikatiba, na wala hatumkomoi mtu, mengi mawaziri mnakuwa hamuyaoni ni kama kukumbushana msije mkataba kujenga chuki baina yetu. Baada ya maelezo hayo Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo tu.

Kwa kuwa uwajibikaji wa utumishi wa umma wa viongozi ndio nguvu kazi ya Taifa, tokea kwa uteuzi wako Mhe. Waziri umekutana lini na watumishi ili kuwakumbusha wajibu wao.

La pili kwa kuwa tatizo la urasimu limekuwa kero kubwa la upatikanaji wa huduma za jamii, lini serikali itaweka utaratibu kuweka angalau masanduku ya maoni katika sehemu za jamii zinazotolewa kwa ajili ya wananchi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma:** Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kawaida kwa mawaziri kufanya mazungumzo, kufanya ziara na kukutana na watumishi waliochini ya wizara zao, na hilo ni moja katika jukumu letu kuhakikisha kwamba tunafuatilia katika maeneo hayo na tunasikiliza shida zao na matatizo yao.

Suala la kimsingi ni kwamba sisi kama mawaziri tunaosimamia wizara zetu, tunamuakilisha Mhe. Rais katika utekelezaji wa kazi zetu za kila siku, na tunaendesha shughuli zetu kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi. Kwa hivyo la msingi ni kwamba tuhakikishe kwamba utendaji katika maofisi yetu unakwenda kwa ufanisi mzuri na wananchi wanapata zile huduma muhimu ambazo tunazihitajia.

Sasa siwezi kumwambia kwamba nimefanya lini ziara hiyo kwa sababu sina kalenda hapa itakayosema ziara hiyo, lakini tunafanya kama wanavyofanya mawaziri wengine na nadhani tukitizama vyombo vya habari tunaona jinsi mawaziri wanavyochacharika huko na kufuatilia taarifa mbali mbali katika mawizara yao.

**Nam. 52**

**Kuimarisha Vilabu vya Soka Nchini**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** - Aliuliza:-

Mchezo wa mpira wa miguu soka au kabumbu ni moja katika mchezo unaopendwa sana na Wazanzibari walio wengi. Kwa kuwa timu za Zanzibar kwa sasa zinavunja moyo kwa kiasi kikubwa wapenzi wake baada kufanya vibaya siku hadi siku kutokana na kushindwa kupata fedha za kusajili wachezaji wa kulipwa (*professionals)* kutoka nje ya nchi kama ilivyo timu nyengine za nchi jirani.

(a) Je, tatizo hili ni kutokana na uwezo mdogo wa *ZFA* kusimamia soka hapa nchini.

(b) Ni lini Serikali itaondoa sababu ya timu zetu kufanya vibaya kwa kuvitaka vyombo au taasisi za fedha kutoa mikopo kwa timu zetu na hatimae kuweza kuajiri wachezaji wa kimataifa.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, tatizo halitokani na uwezo mdogo wa *ZFA* kusimamia soka hapa nchini, lakini kinachosababishwa ni utashi wa watu binafsi wanaotaka kurejesha nyuma maendeleo ya soka nchini, kwa kusababisha migogoro ndani ya uongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar, wao wakiwa si viongozi wa mpira wa miguu wanaokubalika na wadau wa soka nchini.

(b) Jukumu la kuzifanya timu zetu kufanya vizuri na kusajili wachezaji wa kulipwa liko kwa uongozi wa vilabu vya timu husika na kwa ushauri wa chama kinachosimamia mpira wa miguu (*ZFA*). Serikali husaidia pale inapoona kuna upungufu. Kuna haja ya wapenzi wa michezo kuipa nafasi *ZFA* kutekeleza wajibu wake badala ya kuisakama na kuifanya ipate ugumu wa kusimamia mpira wa miguu kwa kuibua migogoro isiyokwisha. Ushauri wangu tuiachie *ZFA* ifanye shughuli zake ipasavyo izidi kujenga imani kwa watu na hizo taasisi za fedha ambazo kikiamini chama hicho zitakuwa tayari kutoa misaada na mikopo kwa chama hicho na timu zetu.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Waziri, kwa kuwa jana tuliambiwa tusitaje vyeo lakini nitamtaja, ingawa ni mkwe wangu Mhe. Waziri, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Waziri napenda kumuuliza swali dogo la nyongeza. Serikali katika suala zima la soka haiwezi kujivua, kwa kuwa wajibu wa serikali ni pamoja na kuleta maendeleo, yakiwemo maendeleo ya mchezo huu wa soka au kabumbu. Na kwa kuwa serikali za jirani hapa ziliingilia kati katika kuinua maendeleo likiwemo soka, kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Aliweza yeye mwenyewe kuleta *coach* kutoka nje na soka akamleta *coach* Marcio Maximo hapa na soka la Tanzania likaanza kuinuka kuanzia pale.

a) Je, kwa mnasaba huo ni lini serikali yetu kupitia japo wewe Mhe. Waziri itaweza kuleta *coach* wa kimataifa aliye na kiwango kama kile cha Marcio Maximo ili kuja hapa na kuweza kufundisha timu yetu ya Taifa na hatimae soka letu likaja juu.

b) Kitendo cha *ZFA* kusema wao sio wanaofanya huu mchezo wa mpira wa miguu kusinyaa, kusema sio wao mbali ni vijana ambao wako nje kutokana na utashi wao, wakati wao ndio wenye dhamana kitendo cha kusingizia watu wa nje kwa utashi wao wakajivua wao katika jukumu hili la kudhalilisha soka katika nchi hii huko si kushindwa kazi Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti, sisi tunaamini kwamba mjenzi wa nchi ni mwananchi mwenyewe, na kwamba bado tunaamini kwamba katika nchi yetu tuna wenzetu ambao wana ujuzi mzuri sana wa ukocha wa kuzifundisha timu zetu, na bado *ZFA* yenyewe haijaona umuhimu wa kuiambia serikali kwamba inahitaji kocha kutoka nje. Sasa wakati wote ambapo cha Chama cha Mpira wa Miguu kwa kushauriana na klabu zenyewe zikiona umuhimu huo basi wizara ipo, serikali ipo tutashauriana na itatafuta kocha popote kutoka nje.

Pamoja na hayo katika kuangalia kwamba tunaibua vipaji vya vijana wetu, tuliwahi hapa kuleta *coach* kutoka Misri akawa anazifundisha timu zetu ndogo ndogo. Kwa hiyo, Mheshimiwa bado kwamba sisi kama serikali kwa kushauriana na kushirikiana na *ZFA,* tuko tayari wakati wowote haja ikiwapo kuona kwamba tunaleta ma-*coach* kutoka nje kama ambavyo alifanya Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala lake la pili kwamba *ZFA* isikwepe jukumu. Ninachosema ni kwamba *ZFA* inajitahidi na inajitahidi sana, uongozi uliopo wa *ZFA* kwa kweli umefanya mambo makubwa ambapo uongozi uliopita haikuwahi kufanya. *ZFA* muda mrefu siku za nyuma ilikuwa hauna hata kipando cha kuendelea na shughuli zao, miaka hii miwili iliyopita imenunua gari mbili kwa fedha zao wenyewe, imenunua pikipiki kumi kuhakikisha kwamba watendaji katika ngazi tofauti wanaweza kuzitembelea timu na kuzipa ushauri moja kwa moja. Haya mambo huku nyuma hayakuweza kufanyika.

Kwa hiyo, tunachozungumza ni kwamba *ZFA* wanajitahidi sana, na kwamba bado tunawashauri kuwa walio nje ya *ZFA* waipe nafasi *ZFA* ifanye jukumu lake badala ya kuisakama na kuitafutia mbinu za kushindwa au kupata ugumu wanapofanya shughuli zao.

**Mhe. Nassor Salum Ali:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja lenye (a) na (b) la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, mbali na majibu ya Mhe. Waziri ambayo mimi naweza kusema kwamba funika kombe mwanaharamu apite.

Mhe. Mwenyekiti, katika majibu ya Mhe. Waziri amesifu viongozi wa *ZFA* kwa kuweza kununua magari, kununua vespa ndio maendeleo ya viongozi wa *ZFA*. Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha sana kwa sababu maendeleo ya mpira wa miguu kutokana na mafanikio ya timu zetu za mpira wa miguu, ikiwemo timu ya Taifa na vilabu vyetu ambavyo hushiriki katika mashindano ya kimataifa, sio kununua vyombo vya kupanda na vyenginevyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wachezaji wa zamani ambao kuna Mzee Mkweche, kuna Abdul Majham, kuna Nassor Machoto na wengine kina Bausi na wengine hao ambao nadhani wangeweza kusaidia kutoa ushauri ili kukuza…

**Mhe. Mwenyekiti:** Uliza swali.

**Mhe. Nassor Salum Ali:** Je, wizara imefanya mikakati gani kushirikiana na Baraza la Michezo na *ZFA* yenyewe kufanya mikakati ya kuinua soka letu la Zanzibar, sio kutegemea kununua vipando vya kuweza kutumiwa kwa *ZFA*.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti, moja katika maendeleo ya taasisi ni kuona kwamba taasisi ina nyezo ya kufanyia shughuli zake. Huwezi kuwa na taasisi ambayo haina jengo, haina uwezo wa kufanya shughuli, haina hata kipando. Haiwezi kuwafikia wadau wake ukasema hiyo taasisi ina maendeleo, kwa kweli itashindwa kufanya shughuli zake. Kwa hivyo, la msingi kwanza taasisi yenyewe ni kujijenga na kuweza kuwafikia na kuwakagua wadau wake. Kwa hiyo kilichofanywa *ZFA* hivi sasa jambo la mwanzo ni kuhakikisha kwamba taasisi hii inajiimarisha.

Suala la kuzungumza na wazee wa zamani, mimi mwenyewe nishazungumza nao si mara moja wala mbili na ushauri wao bado tunaufanyia kazi, na huwa tunakutana kila mara kuona kwamba ni vipi ushauri wao unaweza ukatusaidia katika zama za sasa. Zama za zamani ambazo Mzee Mkweche alivyokuwa akicheza mpira zimebadilika na zama za kileo. *Techniques* zimebadilika sana, hawezi kuchukua *techniques* za Mzee Mkweche na Mzee Mashoto enzi hizo ukazileta leo katika uendelezaji wa mpira wa miguu; tunachukua yale ambayo tunaweza kuyafanyia kazi na tunayafuata. Lakini bado nasema kwamba walio nje ya *ZFA* wakae upande wawaachie *ZFA* ifanye kazi zake kwa mujibu wa katiba iliyopo.

**Nam. 93**

**Mpango wa Kujenga Skuli za Serikali za Kisasa**

**Mhe. Nassor Salim Ali -** Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuinua sekta ya elimu kwa wizara kujenga skuli mpya za kisasa kwa Unguja na Pemba na nyengine kuzifanyia ukarabati katika azma yake hiyo, wizara ilikuwa na mpango wa kujenga majengo ya kisasa na ya ghorofa katika skuli ya Mwembeshauri.

a) Je, mpango huo wa kujenga majengo mapya ya kisasa ya ghorofa katika skuli hiyo bado upo.

b) Je, kama upo unatarajiwa mpango huo kuanza lini.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 93 ambalo lenye sehemu (a) na (b).

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) imetekeleza mradi mkubwa wa Uimarishji wa Elimu ya Lazima ambapo skuli 21 za sekondari zimejengwa. Kampasi ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa huko Mchanga Mdogo, Pemba na skuli 6 za Sekondari zimefanyiwa ukarabati mkubwa katika sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba. Mbali ya utekelezaji wa mradi huo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Mfuko wa *OPEC* umekusudia kujenga Skuli 10 za ghorofa. Mradi huu ulichelewa kuanza kutokana na kutokamilika kwa taratibu za kisheria kuhusu makubaliano ya mkopo.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, nina furaha kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa sasa hivi taratibu zote za kisheria zimekamilika na mradi huo umetangazwa rasmi kuanza utekelezaji wake kuanzia tarehe 12 Januari 2015. Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mpango wa kujenga skuli za kisasa ya ghorofa katika eneo la Skuli ya Mwembeshauri, Unguja upo.

(b) Utekelezaji wake utaanza hivi karibuni kwa kutoa matangazo ya zabuni elekezi ya ujenzi ambao ndio utakaoandaa michoro na usimamizi wa ujenzi.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wizara husika kwa kuweza kujenga majengo mbali mbali na kufanyia ukarabati kama maelezo ya Mhe. Naibu Waziri alivyoeleza.

Mhe. Mwenyekiti, mpango wa ujenzi wa skuli ambao Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba utaanza karibuni, swali langu ni kwamba, pale Skuli ya Mwembweshauri ambayo iko katika Jimbo la Rahaleo, Shehia ya Mwembeshauri, Wadi ya Rahaleo. Mheshimiwa maeneo yale ambayo yamezunguka Skuli ya Mwembeshauri kuna mabanda mengine ambayo yamejengwa ya uwekezaji.

Je, kutokana na majengo yale ambayo yako ndani ya skuli ile, wizara ina mpango gani ili kuhakikisha kwamba hayo majengo ambayo yatajengwa ya kisasa, ya ghorofa itaanzia wapi na itamalizia wapi, na yale mabanda yalioko pale yatakuwepo au yataondoshwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kusema skuli hizi zijengwe wapi na wapi wizara ilitembelea maeneo yote ambayo imelenga kujenga skuli hizi. Tulikaa na Kamati ya Skuli ya Rahaleo tukaona ile kadhia ya mabanda ambayo yapo pale na tulionana na baadhi ya watu ambao wamejenga yale mabanda. Kwa ufupi nataka kumwambia Mhe. Mwakilishi kama kuna mabanda ambayo yataathirika na mradi ule. Skuli ile ikijengwa kuna mabanda ambayo yataondoka pale na ambayo Kamati ya Skuli wenyewe ndio wameridhia kuwepo pale ni miradi yao wamekodisha na wanapata pesa za kuwaendeleza.

Kwa hivyo, yale ambayo yataingia katika ujenzi wetu tabaan yataondoka na yale ambayo hayatoingia katika ujenzi wetu hatuna haja ya kuondoa, kwa sababu Kamati ya Skuli wenyewe kwa kushirikiana na walimu waliopo pale ndio ambao wametaka mabanda yale yawepo katika maeneo yale.

**Mhe. Farida Amour Mohammed:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri ambayo amekiri katika swali lake la msingi kama wana lengo la kujenga skuli 10 za kisasa za ghorofa. Sasa kuna tetesi kuwa skuli hizo mpya za ghorofa za kisasa zitajengwa Mkoa wa Mjini Magharibi.

(a) Je, tetesi hizo ni kweli. Kama ni kweli si ubaguzi wa kunyima haki wilaya nyengine.

(b) Kuna vigezo gani vinavyotumika katika kujenga skuli hizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, skuli hizi 10 ambazo tumekusudia kujenga tutajenga kwa Unguja na Pemba. Lakini kwa Unguja ni kweli tetesi alizosikia kama tumekusudia skuli hizi kuzijenga katika Mkoa wa Mjini Magharibi, kwa Unguja ni skuli sita na kwa Pemba zitajengwa skuli nne katika Wilaya zote za Pemba. Tutajenga Kizimbani kwa Wilaya yake ya Wete, tunajenga Micheweni - Ndugu nkitu, Chake Chake na Mwambe, Mkoani.

Kwa Unguja kama ambavyo nilisema tunajenga kwa Mkoa wa Mjini Magharibi na hii ni kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi ambao tunao katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Wastani wa darasa moja kwa skuli zetu hizi ni wanafunzi 70. Kama mnakumbuka Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika bajeti yetu tuliyoelezea kama tuna mradi maalum kwa ajili ya Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo Mheshimiwa kwa ufupi Wilaya ya Magharibi wanafunzi wa msingi ni 71,275, kwa mjini ni 35,295. Kwa Wilaya ya Wete ambako pia tutapeleka ni 24,000.

Kwa hivyo, ukitizama hizi wilaya tatu tu ambazo nimezitaja kiujumla ni karibu asilimia 45 na zaidi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe mnapozungumza maneno yanakuwa yanaingia kwenye *hansard* yanaingiliana na majibu ya waziri, sasa wale watu wa *hansard* wanakuwa hawafahamu vizuri. Tunaomba tumsikilize Mhe. Naibu Waziri anapotoa majibu. Ahsante Mhe. Naibu Waziri tuendelee. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Narudia kusema kwamba Mheshimiwa skuli hizi zaidi ujenzi wake unategemea na mahitaji ya skuli ambazo tunazo na mahitaji ya skuli ni zaidi katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa sababu kila darasa lina wanafunzi takriban 70 ambao wanaingia kwa darasa moja tofauti na skuli nyengine ambazo wanaingia mkondo mmoja tu, kama skuli za Wilaya ya Kusini. Lakini kuna skuli kwa mfano Skuli za Mwambe, Mkoani ambako skuli hizi tunazipeleka wanaingia mara tatu kwa siku. Kwa hivyo, ndio tukaamua Mwambe pia kupeleka skuli hizi.

Vile vile, nilikuwa natoa takwimu halisi za wanafunzi ambao tunao katika Mkoa wa Mjini Magharibi na ndio tukaamua kuwa ni lazima skuli hizi kwa Unguja zote tuzipeleke katika mkoa huu ili kuondokana na msongamano mkubwa ambao tunao katika skuli za mkoa huu.

Kwa hivyo, ukitizama wilaya hizi tatu tu ni asilimia 45 na zaidi ya wanafunzi wetu ambao tunao na ndicho kigezo ambacho tuliona ni lazima tukichukue au tukifuate kutokana na idadi ya wanafunzi ambao tunao katika wilaya husika. Ni hivyo Mheshimiwa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa toka jana maswali yetu ni mengi na muda unakuwa unakwenda zaidi, naomba kutumia Kanuni ya 39(3) kama ambavyo kiti kinavyopewa uwezo kuongeza dakika 15 ili tumalizie maswali yaliyobakia. Katibu.

**Nam. 67**

**Tatizo la Maji Mkoa wa Mjini Magharibi**

**Mhe. Ali Salum Haji** – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu maeneo mengi ya Mkoa wa Mjini Magharibi yamekuwa yakipata maji kwa zamu na maeneo mengine kukosa kabisa huduma hiyo.

(a) Je, wizara imefikia wapi kumaliza tatizo hili.

(b) Na ni muda wa kipindi gani tatizo hili litamaliza kabisa ili kuondoa usumbufu kwa wananchi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 67 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Mjini inaendelea kuimarika siku hadi siku, ingawaje kuna maeneo mengine yanapata maji kwa muda mrefu na kuna baadhi ya maeneo yanapata maji kwa mgao kwa vipindi tofauti na maeneo machache yanakosa huduma hiyo kabisa. Hata hivyo, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imekuwa ikiendelea kulitafutia ufumbuzi suala hili kwa kuwa na mpango wa uimarishaji huduma kwa muda mrefu ambao ni uchimbaji wa visima pamoja na ulazaji wa mabomba katika maeneo tofauti, ikiwemo Mradi wa Chumbuni na Welezo kupitia programu ya usambazaji maji mijini na uimarishaji wa miundombinu ambao utafanya kazi ya ubadilishaji wa mabomba chakavu katika maeneo ya Mji Mkongwe na Ng'ambu ya zamani.

(b) Kama nilivyosema hapo juu, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea kuimarisha mradi mkuu chini ya Ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*). Kumalizika kwa mradi huo mwaka 2017 wananchi wa maeneo hayo watapata huduma hiyo kwa uhakika zaidi.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, nataka niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na majawabu ambayo siku zote imekuwa ni hayo kwa hayo jitihada zinaendelea, visima vinaendelea kuchimbwa, mambo mazuri yanakuja, lakini baada ya kupunguza kasi ya tatizo tunaongeza kasi ya tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu kama nilivyokuwa nimeuliza swali mama tulikuwa tunapata maji kwa zamu katika siku mbili mpaka tatu, lakini tuna takriban miezi mitatu Shehia ya Mikunguni na Shehia ya Kwa Alamsha, sasa hivi baada ya kupata zamu kwa muda wa siku tatu wanapata maji kwa zamu si chini ya wiki mbili mpaka tatu na wakati mwengine inafika mpaka mwezi katika kipindi cha miezi mitatu.

(a) Nataka Mhe. Naibu Waziri anieleze ni sababu gani iliyopelekea shehia hizi baada ya kupata maji kwa zamu ya siku tatu kufikia hadi wiki mbili mpaka tatu.

(b) Katika suala la miradi kuna mradi wa Michamvi, nataka kujua tatizo la kusuasua kwa mradi ule hadi leo haujakamilika. Nakushukuru.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri ni kwamba jitihada za wizara yangu katika kutatua matatizo ya maji ni kubwa sana na wala sio majibu hayo kwa hayo.

Kwa sababu tunaongeza upatikanaji wa maji kila siku Unguja na Pemba. Tuna miradi mingi ya upatikanaji wa maji mipya ambayo tayari imeshakamilika na mingine tumeshakabidhiwa. Tatizo la mjini tunalijua na ndio maana katika tatizo la mjini tuna mradi wetu wa *IDF12* ambao ni Mradi wa *ADB* uliochimba visima katika maeneo ya Wilaya ya Magharibi, pamoja na kukagua mabomba machakavu yaliopo katika mji huu yanayosababisha kupotea kwa maji.

Kwa hivyo, jitihada zinaendelea na tunategemea kwamba mradi huu ukikamilika wa *IDF12* ambao sasa hivi tayari umeshaanza tatizo la maji kwa mjini litakuwa limeondoka.

Amezungumzia matatizo ya Kwa Alamsha ambako wanapata matatizo ya maji na sehemu nyengine yanakwenda badala ya kuwa siku tatu sasa hivi wanasema wanachukua mwezi mzima wakati mwengine hawajapata maji.

Nashkuru kwa kupata taarifa hiyo kwake na mimi nitajaribu kuangalia kwa nini suala hili linatokea katika maeneo hayo na tutarekebisha. Lakini hata hivyo, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge kwamba wanapoliona hili tatizo la maji katika maeneo yao wanajitahidi na wao kulitatua kwa kuchimba visima vifupi na kuweka matangi kuwasaidia wananchi kupata huduma ya maji.

Hata hivyo, tutashirikiana na Mhe. Mwakilishi kuona kwamba kuna tatizo gani linalosababisha katika maeneo hayo kukosekana kwa maji katika kipindi kirefu namna kama hii, kama ni ubovu wa mabomba au kitu chengine chochote tutashughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, swali lake la pili ni kwamba hatupendi sisi Wizara ya maji kuona kwamba wananchi wa nchi hii wanalalamika katika upatikanaji wa maji. Hatupendi kuona hali hiyo na ndio maana tunajitahidi kusimamia miradi na tulitaka hasa kwamba katika mwaka huu tatizo la maji tumelipungusa katika nchi yetu Unguja na Pemba, na ndio maana tumeanzisha miradi mbali mbali.

Anapozungumza suala la michango ni kwamba kuna maeneo hapa Unguja na Pemba ukichimba visima chini unakuta maji ya chumvi, Michamvi kulikuwa na visima lakini kilikuwa kina maji ya kunywa mazuri ya kwanza baadae yamebadilika na kuwa ya chumvi. Michamvi tumeanzisha mradi wa kutengeneza maji ya chumvi kuyageuza kuwa maji ya baridi na tunafanya *desalination* huo maradi umechukuliwa na Wajarumani na wameondoka kidogo kwenda kwao kwa ajili ya mwaka mpya, maana wenzetu hawa mwaka mpya wanapenda kutumia kwao pamoja na *X-mas* lakini wakirudi mradi wa Michamvi utaendelea na ndio tunategemea kwamba baada ya muda mfupi kama tutafanikiwa, kwa miradi hii katika kisiwa cha Uvi ambapo nako ukichimba maji yanapatikana ya chumvi.

Hivi sasa wamechimba visiwa pale wemepata maji ya chumvi wanayatengeneza yanakuwa maji ya kunywa na watu wanapata maji ya kunywa. Kwa hivyo, halkadhalika na Chwaka pale tuna mradi kama huo na Pemba nako kuna mradi huo na Michamvi tunaendelea nao mradi kama huo, baada ya muda mfupi Wajarumani hawa wakirudi tutaendelea na mradi kama tulivyoingia katika maeneo mengine.

Hata hivyo jitihada za kusambaza maji katika maeneo hayo kutoka katika maeneo ambayo yako mbali kidogo na maji yabaridi nazo hizo zitaendelea ili kuondoa matatizo ya maji katika maeneo yetu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, bado maji tatizo kubwa na nataka kumuuliza Mhe. Waziri ile miradi ya Japan imefikia hatua gani mpaka hii leo na tatizo hilo limekuwa la muda mrefu na wananchi wanaendelea kukosa maji ikiwemo Shehia ya Pete, Muyuni angalau la Michamvi limetafutiwa ufumbuzi kidogo. Lakini bado wananchi wanaendelea kuteseka baada ya kushughulikia kilimo wakirudi ni kutafuta maji, imekuwa wananchi wetu bado wimbo huu wa Taifa unaendelea.

Tukiachia hapo maeneo ya Mjimkongwe kuna mahoteli makubwa sasa hivi yanajengwa ikiwemo Serena ile unakuta magari kwa magari yanapeleka maji, tatizo gani la Mjimkongwe mpaka muda huu kukosa maji?

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, maji ni bidhaa muhimu sana. Lakini vile vile wananchi wakawa na shukurani tunapotatua matatizo ya maji katika maeneo yao, inaweza ikatokea maeneo fulani maji yameshaimarika kabisa na watu wanapata maji ya uhakika kabisa, hatupati suala la kushukuriwa kwamba pale nimetatua tatizo la maji. Lakini kila mara tunapata maswala katika maeneo ambayo tunahangaika nayo na kunakuwa na matatizo ya maji na tunahangaika nayo ili kutatua matatizo yale.

Kwa hivyo, tunawambia kwamba sio wimbo wa taifa ni kwamba maji ni bidhaa adimu na inahitajika kwa kila mtu, kwa maisha ya siku kwa siku kwa sababu kila kitu kinakuwa kwa sababu ya maji. Kwa hivyo, tunajua kwamba jitihada ya kutafuta maji kwa ajili ya wananchi lazima ziwe kubwa na ndio maana mkazo wetu mkubwa wizara hii hivi sasa tumeweka kwenye maji zaidi, ili yapatikane maji zaidi kuliko mambo mengine yote, hivi sasa kwa sababu ndio kitu muhimu kusema kweli.

Kwa hiyo, sio wimbo wa Taifa wa kila siku huu, Mhe. Jaku Hashim Ayoub akubali kwamba pamoja na kuwa kuna miradi ya Japan imeanzishwa katika nchi hii lakini bado watu siku hizi wote wanataka kutumia maji yanayotoka katika mifefreji, au mabomba kwa jina la wenzetu Watanzania Bara. Visima vina matatizo na vimeshabadilishwa na hii Tabia ya Nchi. Utakuta karibu kijiji kizima nyasi zimekauka. Hivi sasa maji lazima twende chini sana, tupate maji ya uhakika.

Kwa hiyo, tatizo hilo lipo. Kuna tatizo la ma- *pamp*, mabomba, kuna tatizo la umeme ambayo hayo yote tunayashughulikia kwa wakati mmoja. Kwa hivyo, nyimbo ya Taifa kuna maeneo yameshafanikiwa sana. Sasa hivi ya maji hawana matatizo lakini hatujapa kuambiwa kwamba tumefanikisha katika suala hilo. Kunako matatizo ya maji tunawaambia wananchi kwamba tutaendelea kwenda kwenye matatizo ya maji na tutapambana mpaka tuwapatie maji, ahsante sana.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Hii miradi ya Japan imekufa njiani au bado inaendelea ili wananchi wapate kujua.
**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Nachukuwa mfano wa mradi wa Japan ulioko Welezo. Mradi huu ulikuwa upate maji sio pale pale kutoka kisima cha Welezo lakini kulikuwa kuchimbwe visima vyengine vilishie katika matangi yale. Kwa bahati baadhi ya visima vya kulishia katika matangi yale havijapatikana mpaka sasa hivi kutokana na uwezo wetu wa bajeti yetu inavyokwenda na bajeti tunapitisha humu humu.

Kwa hivyo, ile miradi ipo na inasaidia kwa kiasi fulani lakini inakosa maji kutokana na upingufu wa visima ndio maana tumeanzisha miradi mingine mingi, tumechukuwa mradi wa Rasilhema ambapo tunachimba visima 50 Unguja na Pemba, ili kutatua matatizo ya maji. Tuna mradi wa visima kwa Wachina ambapo utaanza kesho kutwa, tutachimba visima kwa ajili ya kujaza matangi yetu ambayo tunayo.

Hivi sasa *alhamdulillah!* Tuna matangi mengi sana tukipata maji sasa hivi, maana tangi unalo lakini kama halina maji watu watakuwa hawapati maji. Kwa hivyo, mradi wa Japan una uwezo mkubwa wa kukushanya maji ulioko pale Welezo lakini lazima tupate visima vya kujaza mle yale matangi ili yaweze kuwafikia wananchi. Mbali na hili tatizo la miundo mbinu linaloshughulikiwa na huu mradi nilioutaja wa *IDFL*.

**Nam. 54**

**Kazi za Vibarua kutopatiwa Wazawa**

**Mhe. Saleh Nassor Juma -** Aliuliza**:-**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar moja kati ya mipango yake mikubwa ni kupunguza umasikini na kuongeza kipato kwa wananchi wake, sambamba na kutengeneza ajira kwa vijana.

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hutangaza tenda kwa Makampuni mbali mbali ya ndani na nje ya nchi, pale inapokuwa na miradi mikubwa mbali mbali kama vile ya ujenzi wa barabara, viwanja vya ndege pamoja na majengo ya taasisi mbali mbali za Serikali.

Ni sababu gani za msingi zinazopelekea baadhi ya Makampuni ya nje ya Zanzibar vibarua wake wengi hata kwa zile kazi zisizohitaji taaluma kuwatoa Tanzania Bara pamoja na Kenya.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano -** Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekitia, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 54 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inajukumu la kusimamia miradi ya ujenzi katika sekta ya usafiri na Mawasiliano, ikiwemo miradi ya ujenzi wa barabara, viwanja vya ndege na bandari. Baadhi ya miradi

hiyo hutekelezwa na wakandarasi wazalendo na mengine hutekelezwa na wakandarasi kutoka nje ya nchi kulingana na taratibu za zabuni kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Manunuzi ya Serikali.

Mhe. Mwenyekitia, kwa mujibu wa mikataba na makandarasi Wizara haina uwezo wa kuwalazimisha kuajiri wafanyaka kutoka Zanzibar tu. Hata hivyo Wizara huwashauri wakandarasi wetu kuajiri zaidi wananchi wetu hasa kwa zile kazi ambazo wanauwezo wa kuzifanya kama vile vibarua na nafasi nyengine za chini za kitaalamu. Kwa kiasi kikubwa tunashukuru wakandarasi wengi wameweza kutekeleza kwa vitendo ushauri wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano mradi wa ujenzi wa barabara tano za Kaskazini Pemba zilizofadhiliwa na *MCC*, na kutekelezwa na kampuni ya *H-Young* kutoka Kenya ambapo mkandarasi aliajiri jumla ya wafanyakazi 249, kati yao wafanyakazi 205, sawa na asilimia 82.3 ni wazalendo na wafanyakazi 44 tu, sawa na asilimia 17.7, ndio wageni.

Mhe. Mwenyekiti, mradi wa barabara mbili za Kaskazini Pemba, Wete – Gando na Wete – Konde unaotekelezwa na kampuni ya kizalendo ya *MECCO*, Kampuni hadi kufikia January 2015, ilikuwa na wafanyakazi 71, ambao wote ni wazalendo. Mradi wa ujenzi wa njia za kupitia ndege na eneo la maegesho ya ndege katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Abeid Amani Karume uliotekelezwa na kampuni ya *SOGEA* Satom ya Ufaransa ulikuwa na wafanyakazi 278, amabpo 14 tu ndio wageni kutoka nje ya Tanzania 264 ni wazalendo wa nchi hii. Mhe. Mwenyekiti, Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kuwa katika miradi hii imekuwa ikiajiri wazalendo zaidi kuliko wageni hasa kwa nafasi zile za vibaru na kazi za chini zisizokuwa za wataalamu, kama vile masharti mengine yanavyoekeza.

## HOJA ZA SERIKALI

### Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu Namba 2 ya mwaka 1996

**(Kusomwa kwa mara ya Pili)**

**(Majadiliano yanaendelea)**

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuuchangia mswada huu. Baada ya kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze kwa pongezi Mhe. Waziri.

Nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu lakini pia nimpongeze kwa usimamizi wake katika wizara yake katika kuona namna gani anaweza kuinusuru nchi hii katika masuala mazima ya kimazingira. Imani yangu ile nishani aliyopewa ya mwanamke jasiri ataitumia vyema katika kutekeleza majukumu yake katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mswada ni mzuri na una mambo mengi ambayo yamejipanga katika kuonesha kwamba unaondosha kabisa tatizo la mazingira katika nchi yetu. Lakini napenda niseme kwamba pamoja na mswada huu mzuri ambao tunategemea baada ya muda mfupi utakuwa sheria bado niombe serikali kutafuta namna ya pekee katika kuelimisha na kuwataka wananchi wake kusimamia sheria ipasavyo. Kwa sababu kinachoonekana kwa Zanzibar tatizo sio sheria, tatizo ni usimamizi wa sheria pale inapokuwa tayari katika utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu tu kabla ya kufanya marekebisho ya sheria hii tayari tulikuwa na sheria za kimazingira sheria ambazo zilikuwa zinaeleza masuala mbali mbali katika kuchukuwa hatua kwa yale makosa ambayo yalikuwa yanafanyika.

Moja ya kifungu cha sheria kulikuwa kuna kifungu cha wanaochimba mchanga pasipo na kufuata utaratibu wa sheria basi panapobainika yale magari hutaifishwa. Lakini nataka niamini kwamba tangu sheria ile imetungwa hakuna hatua ambazo tumeziona zimetekelezwa na magari huwa yanakamatwa na urasimu au umimi na udugu ndio unaopelekea kutokutii sheria na matokeo yake kuharibu ya kuchafua mazingira ya nchi hii.

Sasa namuomba kwa dhati kabisa Mhe. Waziri pamoja na hekima zake alizokuwa nazo, kama anataka kupitisha sheria hii kufatilia kwa kina watendaji katika maeneo ya Wilaya ambapo magari huwa yanatoka mashamba kuja

mjini, ili watendaji wale watekeleze ipasavyo zile sheria ambazo tunakuwa tunazipitisha ili kuweza kulisaidia suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka nimsaidie Mhe. Waziri aje anisaidie kwamba katika mswada huu nimejaaribu kuangalia kadiri ya uwezo wangu lakini sijaona pahala ambapo pamewekwa adhabu kwa taka za hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna kitu ambacho ni hatari kwa mazingira ya afya za binadamu basi ni taka za Hospitali. Kwa sababu taka zile moja kwa moja wingi wa mataka ya Hospitali inakuwa ni sumu kwa wanaadamu. Sasa tunakuwa tunashuhudia na tumeshazungumza mpaka kwenye vyombo hivi, hata Hospitali yetu ya Searikali imeshafika pahala huzitupa taka zile kwenye mazingira yasiyokuwa salama katika eneo ya nyuma ya Mapinduzi mpya, sasa tukajaribu kuzungumza tukapiga kelele lakini tunashukuru kwamba tatizo lile limepata ufumbuzi.

Tukiachilia kwenye Hospitali za kiserikali pia tuna Hospitali binafsi ambazo wanakuwa wanazichukulia taka za Hospitali, kama ni taka za kawaida kwa sababu wa wepesi wa kwenda kuzitupa wanapewa watoto hawafikishi katika maeneo husika, na hazina utaratibu na taka zile matokeo yake zinaathiri afya za wanaadamu.

Sasa ningemuomba Mhe. Waziri katika Mswada huu wa Sheria ajaribu kuangalia pahala gani ambapo ataweka adhabu na adhabu hii, hata kama kwa Hospitali iwe kali zaidi kuliko adhabu ya taka ngumu za kawaida kwa sababu taka hizi ni hatari kwa afya za wanaadamu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo sasa nataka niingie katika baadhi ya vifungu mbali mbali ambavyo nimejaribu kuviangalia na nimeona kuna mapungufu kwa mawazo yangu na naomba Mhe. Waziri ajaribu kulichukuliwa hilo.
Suala la kwanza Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 323, kifungu cha 5(3) hapa nilikuwa nataka niweke msisitizo tu baada ya kupitisha mswada huu na kuwa sheria Mhe. Waziri atafute namna ya pekee ya kutoa taaluma kwa wananchi katika kulifanyia kazi. Kwa sababu kifungu hiki Mhe. Mwennyekiti, kinazungumza kwamba kila mtu ana haki ya kutoa malalamiko kwa taasisi husika au kuchukuwa hatua ya kisheria dhidi ya mtu anayetaka kusababisha uharibifu au uchafuzi wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu ni kizuri lakini tatizo bado nataka kuzungumza kwamba Wazanzibari wengi wamekuwa na muhali katika kuchukuwa hatua za kisheria pale matatizo yanapojitokeza. Hili sio katika masuala ya kimazingira lakini huwa tunalizungumzia hata katika suala la unyanyasaji, mara nyingi watu wanakataa kwenda kutoa ushahidi pale yanapojitokeza masuala ya unyanyasaji. Hofu yangu kwamba sheria itakuwa nzuri lakini watu watakaa kuchukuwa hatua kupeleka malalamiko au kwenda kuchukuwa hatua kwa watu wanaofanya uharibifu.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri kwamba tutakapopitisha sheria hii kifungu hiki ajaribu kukiangalia kwa umakini katika suala zima la kutoa elimu kwa wananchi ili wananchi kufahamu wajibu wao katika masuala mazima ya uchafuzi wa kimazingira.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho cha 5(6) naomba nikisome kidogo halafu nitoe mapendekezo ya marekebisho kwa Mhe. Waziri kinasomeka kwamba:-

> "Ikiwa Mamlaka itashindwa kuchukuwa hatua kwa mujibu wa kifungu kidogo cha tano cha kifungu hiki. Mtu aliyewasilisha taarifa hizo atapeleka malalamiko yake kwa Bodi."

Mimi nilikuwa nataka tusaidiane hapa na Mwanasheria ajaribu kuangalia zaidi. Suala la kupeleka nilikuwa naomba isomeke kama itawezekana kwamba baada ya kuandika taarifa hizo watapeleka iwe taarifa hizo atawasilisha, kama itakuwa inawezeka lugha kidogo nilikuwa na mashaka ya lugha katika kifungu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika ukurasa wa 327 kifungu cha 15(3f) Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kinasomeka kwamba juu:-

> " Mjumbe yoyote wa Bodi zaidi ya Mjumbe anaingia kwa wadhifa wake atasita kuwa Mjumbe ikiwa... Sasa hiki kifungu (f) kinasema kwamba".
>
> "Atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila ya kutoa sababu ya msingi kwa Katibu wa Bodi".

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakuwa napata mashaka kidogo, kwa sababu tunaweza tukamnyima mtu haki yake pasipokuwa na sababu; kwa sababu ukiandika kwamba kama atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila ya kutoa sababu ya msingi, sasa kama mtu anaumwa na maradhi yake yako tete au fahamu zake ziko mashakani mtu huyu atakuwa na uwezo gani wa kutoa taarifa, na inawezekana vikao vitatu vitamaliza, vinne vitamaliza lakini bado hajawa na uwezo wa kutoa taarifa kwamba yeye sasa hivi ni mgonjwa na hali yake si nzuri.

Sasa mimi nilikuwa nataka nisaidie tu kwamba kisomeke kwamba "kama atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila ya sababu ya msingi" nafikiri hili linatosha. Kuliko kusema kwamba atatoa taarifa na wakati mwengine hali yake ya kiafya hawezi kutoa taarifa.

Sasa nafikiri yangetafutwa mazingira mengine ya kuandikwa kwamba atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila ya sababu ya msingi, nafikiri ingetosheleza kusema hivyo na nafikiri ingekuwa imeleta maana halisi kuliko hivi ambavyo inasomeka. Inaweza ikaleta utata kwa wale watu ambao watakuwa wanaumwa na hawawezi kutoa taarifa juu ya mardhi yao.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyengine ambayo nilikuwa nataka niizungumzie ni ukurasa wa 332. Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu (30h) hii inasomeka ni:-

> "Muundo wa kamati, sasa miongoni mwa wajumbe kutakuwa na mjumbe mwengine yeyote kutoka taasisi nyengine yoyote atakaeonekana anafaa".

Mimi nilikuwa nataka nimsaidie Mhe. Waziri tusiseme yeyote anayeonekana anafaa. Mimi nilitaka tusaidie tu, tumuengeze Sheha wa Shehia husika kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa yuko karibu kwa katika yale masuala mazima ya lile eneo husika, ambalo litakuwa kama linachimbwa mchanga au linachimbwa mawe kwa hivyo yeye atakuwa karibu kujua namna halisi.

Kwa hivyo, Sheha wa Shehia husika mimi nafikiri tungemuingiza katika kifungu hiki badala ya kuweka mjumbe yeyote. Kwa nini niseme hivyo Mhe. Mwenyekiti.

Nasemaa hivi kwa sababu kwamba mara nyingi tunapotoa vibali vya kuchimba michanga ule muda wa kumaliza kuchimbwa mchanga kutoka shimo moja kwenda shimo jengine la uchimbaji wa mchanga, wananchi wengi wanatumia ile *loophole* ya lile shimo ambalo linachimbwa mchanga kuendelea kuchimba pasipo na ruhusa, na kwa sababu kwamba ruhusa imeshamaliza. Sasa na siku nyengine eneo jengine ambalo limeruhusiwa jipya linakuwa labda liko mbali zaidi. Sasa mara nyingi watu huwa wanajipenyeza katika lile shamba la zamani kuendelea kuchimba bila ya utaratibu. Sasa kama Sheha tutamuingiza katika kifungu hichi, atakuwa mwepesi wa kusaidia kutoa taarifa kwa wale watu ambao wanaendelea kuchimba mchanga katika eneo ambalo limeshapigwa marufuku, kuliko kumuingiza Mjumbe yeyote, tukaweza kutafuta mjumbe yeyote anayefaa katika maeneo mbali, lakini atusaidie kutoa taarifa pale ambapo linapotokezea moja ama jengine.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ninataka nilizungumzie ni kutoka ukurasa wa 332 mpaka 333 kifungu cha 33 (3) (a). Imeainisha mtu na naomba ninukuu kifungu cha 33 (3) kinasema; "Mtu atakayepewa kibali kwa ajili ya uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka ataweka dhamana ya kimazingira kwa taasisi inayosimamia maliasili zisizorejesheka kwa kuzingatia yafuatayo:-

a) Ukubwa wa eneo litakalochimbwa,

b) Athari zitakazojitokeza, na

c) Gharama za hatua za uendelezaji.

Sasa hapa mimi nafikiri nilitaka nimuulize Mhe. Waziri kutafuta namna ya kuongeza kifungu ambacho kitaainisha kuweka mipaka ya lile eneo ambalo ameruhusika yule kuchimba mchanga katika eneo lake. Kwa nini niseme hivyo Mhe. Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu mara nyingi inajitokeza migogoro kwa wananchi baina ya shamba na shamba, unajua mipaka yetu ya mashamba yetu ipo katika hali ya kienyeji.

Kwa hivyo, mtu atapewa kibali cha kuchimba mchanga eneo lako, lakini wananchi wetu ndiyo wananchi, wao wanatafuta wepesi wa mahitaji yao. Sasa mtu lile shamba ambalo lililoruhusiwa kuchimba mchanga linawezekana likawa halina mchanga mzuri, lakini shamba la jirani ambalo halikupewa kibali la mpakani lina mchanga mzuri. Kwa makusudi tu au uharibu tu watu wakaacha kuchimba shamba lililotolewa kibali wakaingia katika eneo la jirani la yule mtu ambaye hakupewa kibali cha kuchimba na wakaleta migongano na migogoro baina ya mwenye shamba na mwenye shamba.

Kwa hivyo, tutafute namna ya kuongeza kifungu kwamba yale maeneo ambayo yanaruhusika kupewa kibali cha kuchimba mchanga, basi pia kuwe na alama za kuweka mipaka ili wanaokwenda kuchukua huduma zile, wajue kwamba mwisho wa kuchimba katika eneo hili ni hapa kuliko kuliachia huria katika mazingira ya kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo ninataka kulizungumzia kwenye mchango wangu katika Mswada huu ni ukurasa huu wa 334 katika kifungu cha 36, kinasema;

> "Katazo la mchanga wa ufukwe na fungu".

Mhe. Mwenyekiti, naomba nivisome vifungu hivi, kina kifungu kidogo cha kwanza na cha pili.Kifungu 36 (1), kinasema;

> "Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba, kukusanya, kuondoa, kusafirisha au kuuza mchanga kutoka kwenye ufukwe au fungu la mchanga kwa madhumuni ya kibiashara au matumizi mengine yanayolingana na hayo".

Kifungu 36 (2), kinasema;

> "Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi milioni ishirini au kifungo kwa muda usiopungua mwaka mmoja na usiozidi miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja".

Mhe. Mwenyekiti, mimi hofu yangu katika kifungu hichi kwa sababu kimezungumzia masuala ya mchanga wa ufukwe na mara nyingi fukwe zinatumiwa na wawekezaji, wawekezaji mara nyingi wanakuwa na uwezo mkubwa. Nina funzo moja ambalo nimeliona katika fukwe za Uroa, kuna hoteli kule tumewahi kutembelea wakati tupo Kamati ile ya Viongozi Wakuu wa Serikali, tuliliona tatizo la hoteli ambalo mwenye hoteli ameingia mpaka katika fukwe, ameacha zile mita 10 za kisheria na amejenga kuta la mawe, lakini mara baada ya kujenga kuta la mawe, ameuchukua mchanga wa baharini, yaani ameichimba bahari amekuja kujaza katika eneo ambalo yeye anataka kujiongezea, yaani amejiongezea ardhi.

Sasa ardhi kaongeza vipi, amejenga kuta baharini, amekwenda mbele karibu na bahari na zile mita za kisheria amezipita, halafu ameuchimba mchanga wa bahari ameutia ndani. Sasa hawa watu wana uwezo mkubwa.

Sasa hofu yangu shilingi milioni mbili kwa tajiri ambaye anataka kuekeza pahala ambapo atachukua mita mia moja kwa mita hamsini, yeye haitowezekana kuilipa Serikali si chini ya mabilioni ya pesa. Sasa haoni taabu kuja kutolewa faini ya shilingi milioni mbili kwa eneo ambalo yeye ambalo lingeweza kumugharimu si chini ya mamilioni ya pesa.

Mhe. Mwenyekiti, hofu yangu hapa adhabu hii ni ndogo hususan kwa maeneo haya ambayo yamezungumzwa hapa. Sasa Mhe. Waziri angeangalia namna ya kuzidisha adhabu ya faini ili iwe fundisho na katazo kwa wale watu ambao wachukua katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango huo kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani na nimshukuru tena Mhe. Waziri ambaye ninamuamini kwa utendaji wake wa kazi, sina mashaka na Mswada, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti,nakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante anayefuata sasa ni Mhe. Mohammed Haji Khalid na baadae Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, ajitayarishe. Waheshimiwa Wajumbe bado naendelea kupokea maombi ya wachangiaji.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kupata nafasi ya kutoa mawazo yangu mafupi kwenye Mswada huu uliopo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha wazima na tukaja hapa katika shughuli zetu za kawaida. Pia, nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa jinsi alivyojipanga na kuandaa Mswada huu ambao pindipo ukipita na sheria ikipita tunaweza kulinda, kutunza na kuhifadhi mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, mazingira ni jambo kubwa na ili nchi iwe katika hali nzuri tuna wajibu wa kuyalinda mazingira, kuyatunza na kuyahifadhi. Zanzibar ni kisiwa, hivyo, kinakabiliana na misukosuko mbali mbali ya kimazingira. Ipo ile tunayosababisha sisi wanadamu na ipo ile ya kimaumbile. Ipo ile ambayo tunasababisha bila ya kujua na tunayosababisha kwa makusudi.

Mhe. Mwenyekiti, dunia inaendelea. Zanzibar ni miongoni mwa nchi za dunia na mwanadamu siku zote anatoka hatua moja kuingia katika hatua nyengine ya kimaendeleo. Lakini pia, maendeleo yana gharama zake na maendeleo baadhi ya wakati yanasababisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Maendeleo kama hayakupangwa vyema, kama hayakuratibiwa vizuri badala ya kuwa ni maendeleo hatimaye yanachafua na kuharibu mazingira.

Kwa mfano, sisi tunahitaji nyumba nzuri na bora za kuishi, lakini kama hatukujenga kwa mpango, tukajenga ovyo ovyo, baada ya kupata pahala pazuri pa kukaa, lakini ule ujenzi wetu itakuwa ni sababu ya kuchafua au kuharibu mazingira na mandhari ya visiwa vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika ujenzi unahitaji mawe na mchanga. Kama hatukuchimba kwa maelekezo ya watu wa mazingira, kama hatukukuchukua mchanga pamoja na mawe baada ya kujenga nyumba nzuri, lakini tunajenga nyumba na hatimaye tunachafua pahala pengine. Kwa hivyo, maendeleo katika nchi mbali mbali hata hapa petu ni sababu moja ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, mwanadamu anahitaji kubadilika kutoka enzi ya *stone age* kuja hapa tulipo hapa leo. Watu tumebadilika, wengi zamani walikuwa wanasafiri masafa marefu kwa miguu, sasa watu wanatembea kwa gari na vyombo vyengine, ni mabaliko. Watu walikuwa wanachota maji visimani kwa kutumia ndoo wanavuta hivi, ukaja utaratibu wakawa wanatumia roda.

Sasa watu wanatia mashine katika visima kuvuta maji. Kwa sababu siku zote mwanadamu anatafuta njia rahisi ya kufanya kazi, ndio maendeleo katika njia ya kufanya kazi. Lakini baadhi ya wakati njia hizi rahisi huwa zinaharibu mazingira. Kwa mfano, tuchukue watu wanaokata miti. Kwa sababu mtu anapofanya kazi ndio kitaalamu, yote katika njia rahisi, kuna msumeno huu wa moto. Huu ni msumeno ambao unamrahisishia mkata mti kuweza kukata mti kwa urahisi, badala ya kutumia ule msumeno wa kawaida kwa kuvutiana ambao pengine unaweza ukachukua nusu saa au saa moja, tofauti na msumeno wa moto ambao anatumia dakika kumi mti umeanguka.

Mhe. Mwenyekiti, sasa dhana ni kuwa anarahisisha mahitaji yake. Lakini imeonekana kwa kutumia chombo kile inasababisha uchafuzi wa mazingira. Hapa huyu anakwazika kwa sababu kutumia chombo kile anachafua au kuharibu mazingira. Lakini *philosophy* ya mwanadamu siku zote anatafuta njia rahisi ya kufanyia kazi kwa muda mfupi na aweze kufanya kazi kubwa, ndiyo maana mkulima badala ya kutumia jembe la mkono akaleta lile *tractor* ili kuraisisha ile kazi yake. Lakini mara nyengine ndiyo ninasema hizo nyengine zinasababisha uchafuzi au uharibifu wa mazingira.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama huu msumemo wa moto pengine kama watu wanamiliki kinyume na taratibu, wawekewe utaratibu wa kumiliki ili wajulikane nani anamiliki na ikitokezea matatizo wale ambao wanajulikana iweze kufuata, kwa sababu ni moja katika njia inayowarahisishia watu hao kufanya kazi kama walivyo watu wengine. Sikusudii kusema uruhusiwe moja kwa moja, lakini ninaonesha ile dhana ya mwanadamu kutoka kufanya kazi kubwa kwa wakati mkubwa, kuweza kufanya kazi ile kubwa kwa wakati mdogo ambayo ndiyo falsafa ya kidunia ilivyo. Watu wakitoka Unguja kwenda Pemba kwa mtumbwi, leo wanakwenda kwa *speed boat*.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 323 kifungu cha 5 ambacho mwenzangu kakigusia kidogo lakini na mimi nitakigusia katika uwono wangu vile vile. Kifungu hichi cha 5 kwenye ukurasa huu wa 323 kinazungumzia kuwa kwenye kifungu cha (4) "Kila mtu ana wajibu wa kutoa taarifa kwa Mamlaka juu ya mpango au shughuli yoyote inaweza kusababisha uharibu au uchafuzi wa mazingira".

Kifungu hichi ni kizuri Mhe. Mwenyekiti, lakini je, ni kila mtu anajua kuwa hichi kinaharibu au kinachafua mazingira. kwa hivyo, lazima kutolewe taaluma ili hawa watu wajue nikifanya hivi ninaharibu au kuchafua mazingira, ili mtu wa taarifa kama hajatoa taarifa amuelimishe yule mtu anaonekana kuwa anachafua haya mazingira kwa kitendo hichi unachofanya unachafua au kuharibu mazingira. Kwa hivyo, hivi usifanye, pale atakuwa mkaidi ndiye achukue hatua ya kutoa taarifa kwa mamlaka inayohusika.

Kifungu cha 5 cha sheria hii kinasema;

> "Mamlaka itawajibika kuzifanyia kazi taarifa zilizowasilishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki".

Sasa baada ya mtu kutoa taarifa Mamlaka husika ilikuwa ifanyie kazi mojawapo ya kufanyia kazi kama ni jambo la kufuatilia, wafuatilie kuhakikisha je, hii taarifa tuliyopewa ni kweli kama ni kweli kuchukua ni kumwita, kumuelimisha na kumuelekeza yule ambaye karipotiwa kwao.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 6 kinasema;

> "Ili kufikia lengo la Sheria hii, kila mtu atatekeleza wajibu aliopewa chini ya Sheria hii kwa kuzingatia misingi ifuatayo".

Mhe. Mwenyekiti, niingie katika kifungu cha 8 cha ukurasa huo huo wa 323, kinasema kuwa;

> "Wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Mazingira watakuwa ni Wametajwa hapo Katibu Mkuu na Mkurugenzi na wote waliotajwa".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, Kamati hii ya Ushauri ya Mazingira inaonesha hii ni ya kitaifa kwa sababu ina viongozi wakubwa watupu; Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa taasisi mbali mbali zinazohusiana na mazingira. Sasa Kamati kama hii ningependekeza iteremke chini katika ngazi ya Shehia, kwa sababu huko chini ndiko kwenye watu ambao wengi wetu hatuna uelewano wa uhifadhi au uchafuzi wa mazingira.

Kwa hivyo, Kamati hizi ziundwe chini na wapewe na taaluma namna ya kuweza kuhifadhi na kulinda mazingira yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tunachimba mchanga bila ya kujua tunaharibu, tunachimba mawe, kukata miti iliyooko baharini na bahari inakuja juu. Yote haya ni madhara ambayo yanasababishwa na mwanadamu na kwa kuwa mwanadamu anafanya haya yote katika kutafuta maisha yake, taaluma ya kutosha itabidi itolewe ili Kamati hizi za ngazi ya chini ya Shehia ziweze kuwaelekeza na kuwafanya watu wasikate miti ovyo, wasitie moto ovyo katika mashamba yao na wahifadhi mazingira yanayotuzunguka.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nitazame kidogo katika kifungu cha 15. Kifungu hichi kinazungumzia Bodi. "Kutakuwa na Bodi ya Mamlaka ambayo itasimamia kazi ya Mamlaka kwa mujibu wa sheria". Wametajwa wajumbe, Bodi itakuwa Wajumbe:-

a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais; na

b) Mkurugenzi Mkuu;

Sasa huyu Mkurugenzi Mkuu, maana kachomoza tu hapa, huku nyuma sijamuona mtu aliyetajwa katika cheo hiki atakuwa ni Mkurugenzi Mkuu. Ningeomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, anioneshe au anisaidie kumuona Mkurugenzi Mkuu pahala ambapo katokea.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, niingie katika kifungu cha 16. Wajumbe wote wa Bodi zaidi ya:- Kifungu (2); "Mjumbe yeyote wa Bodi zaidi ya mjumbe anayeingia kwa wadhifa wake atakuwa mjumbe kwa kipindi cha miaka mitatu na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kisichozidi kimoja".

Hilo siyo tatizo kwamba mjumbe yeyote ambaye hakuingia kwa wadhifa wake na wanaoingia katika wadhifa wao wametajwa pale. Kwa hivyo, watakaa kwa miaka mitatu, lakini wadhifa wake atakaa kulingana pale wadhifa wake nadhani utakapomalizika.

Lakini inaendelea kifungu (3);

> "Mjumbe yeyote wa Bodi zaidi ya mjumbe anayeingia kwa wadhifa wake atasita kuwa mjumbe ikiwa...ina maana masharti haya yote mjumbe ambaye anaingia kwa wadhifa wake yeye hayamkumbi".

Kwa mfano, kama wataandika barua kwa waziri kujiuzulu kwa sababu ni mjumbe anaingia kwa wadhifa wake itakuwa kujibu kwake hakukudhibiti. Kama akifariki ataendelea kuwa mjumbe, kwa sababu katengwa kwa sababu anaingia kwa wadhifa wake. Nahisi haya masharti au hii lugha iliyotumika Mhe. Mwenyekiti ingerekebishwa, kwa sababu hawa wanaonesha wanaingia kwa wadhifa wao. Kwa sababu kama mjumbe kaingia kwa wadhifa wake hata akifa anaendelea kuwa mjumbe kwa mujibu wa sentensi ilivyo, inaonesha hata kama atakuwa yeye ni mjumbe, hata kama atajiuzulu yeye ni mjumbe.

Kwa hivyo, ningeomba hii lugha tu hapa ifanyiwe marekebisho ili iende sawa. Lakini mimi sio mwanasheria, mimi nazungumza katika lugha ya kawaida ya kiswahili, pengine kisheria ni sahihi. Kwa hivyo, ningependa kupata maelekezo ya kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, nizame kidogo katika kifungu cha 20 katika ukurasa wa 328 hiki ni kidogo tu, kimezungumzia uwakili wa serikali wa wizara inayohusika na mazingira atakuwa Katibu wa Bodi. Sasa huyu Katibu wa Bodi katoka nje ya ile bodi yenyewe, kwa sababu kwenye muundo wa bodi, yeye hakutajwa kuwa atakuwemo, lakini kachomoza tu kuwa yeye ni Katibu wa Bodi. Kwa hivyo, ni vyema na yeye angeingizwa akawa kama ni mjumbe wa hii bodi badala ya kuchomoza tu kama ni Katibu wa Bodi.

Mhe. Mwenyekiti, niende kidogo katika ukurasa wa 330 kwenye kifungu cha 24 kinachozungumzia tahadhari ya kimazingira, naomba nikisome kidogo pale nilipokusudia.

Kifungu cha 24(3), kinasema;

> "Mtu yeyote ambaye atakwenda kinyume na masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, atatenda kosa maana yake akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni 10,000,000 na isiyozidi shilingi milioni 100,000,000 au kifungo kwa muda usiopungua miaka 5 na isiyozidi miaka 5".

Lakini hapa nichukulie kuwa imekosewa, kuwa isiyopungua na isiyozidi imejirudia, lakini nadhani isiyozidi miaka 15 au adhabu zote kwa pamoja. Hapa nataka kuonesha tu kwamba isiyozidi miaka 5 na isiyopungua miaka 5. Isiyopungua miaka 5 ufutwe ibakie isiyozidi miaka 15.

Pamoja na adhabu itakayotolewa kwa mujibu wa kifungu hiki Mahakama itaamuru malipo ya fidia na gharama za kurejesha eneo lililoharibiwa zitakazotolewa na mamlaka ambazo zitalipwa na mtu aliyesababisha uchafuzi wa mazingira. Hapa nilihisi kwa kifungu hiki kimetoa hukumu hakikuacha Mahakama itowe hukumu. Aliyefanya uharibifu angelifika tu Mahakamani na Mahakama ndio ikaamua ifanye nini, lakini tayari hapa kifungu kitakuwa kinamuagiza Hakimu afanye nini.

Kwa hivyo, naona kama kifungu hiki kimechukua mamlaka ambayo sio ya kwake.
Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, mimi sina tatizo na mswada huu na naomba nimalizie hapo ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia mswada huu leo hii. Lakini kabla ya hapo niseme kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa katika Baraza hili nikiwa mzima wa afya.

Baada ya hapo nimpongeze Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad, pamoja na waziri, wakiwemo na watendaji wake kwa kutuletea mswada huu wa mazingira katika Baraza letu hili la Wawakilishi. Niseme kwamba mswada huu ni mzuri na unahitaji kufanyiwa kazi, ingawaje mswada huu ulichelewa kuletwa kufutwa sheria ile ya mwaka 1996, lakini kuna haja sasa hivi mswada huu kuufanyia kazi ili uweze kufanyakazi zake. Niwaombe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuuchangie mswada huu na kuuchambua na hatimaye mswada huu kuupitisha, ili kuweza kuwa sheria kamili.

Mhe. Mwenyekiti, niseme sasa hivi kuna haja ya serikali kuwa makini kulisimamia suala hili la mazingira au suala hili la maafa. Kwanza kusimamia ukataji wa mikoko na uchimbaji wa michango hasa sehemu za baharini na sehemu zilizozungukwa na bahari, hili ni suala zuri la kulisimamia ili kuweza kuwaelimisha wananchi wetu kuhusu suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kutoa elimu kwa wananchi, kwa sababu watu wetu chini huko hawaelewi wengine nini maana ya mazingira na wengine hawaelewi nini ukataji wa mikoko na wengine hawaelewi nini athari za uchimbaji wa mchanga. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri baada ya kupitishwa sheria hii na kufanyakazi ili waweze kuwaelimisha wananchi wetu na kuweza kufanyakazi kwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye mswada katika ukurasa wa 223 kwenye kifungu cha 8(1) ambacho kinasema;

> "Wajumbe wengine wasiozidi wawili wanaweza kualikwa endapo waziri ataona inafaa".

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na wajumbe wote hawa waliotajwa, lakini wajumbe hawa waliotajwa wawili hapa niseme kwamba pamoja na mapendekezo hayo Mhe. Waziri ningeomba apendekeze kati ya Masheikh au Sheikh mmoja au daktari mmoja waliopo zaidi sehemu za vijijini, kwa sababu hawa ni watu ambao wanawasaidia sana wananchi na ni watu ambao wana maelekezo zaidi kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 225 kifungu cha 13 kinasema; kwamba kwa madhumuni ya usimamizi wa mazingira Mkurugenzi wa Mazingira atakuwa na kazi zifuatazo:-

Kazi zenyewe hizo hapo (a)(b)(c)(d) na (e), lakini mimi niko katika kifungu cha (a), kuandaa na kutoa ripoti ya hali halisi ya kimazingira kwa Zanzibar na kuwasilisha kwa waziri katika kila kipindi cha miaka mitano.

Hapa Mhe. Waziri nataka aje anieleweshe ripoti hiyo ni ya kila miaka mitano au ripoti hiyo ni ya kila mwaka, kwa sababu naona kuwasilisha ripoti baada ya miaka mitano miaka itakuwa mingi na ripoti ile haitaweza kujulikana na siku nyengine matokeo huweza kutokea kabla ya miaka mitano, yanaweza kutokea mwaka mmoja au mwezi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anifahamishe.

Lakini pia, Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzi awe na sifa ya uhasibu, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, atakapowasilisha ripoti hizo ikiwa Mkurugenzi hana sifa za uhasibu itakuwa ni kazi bure.

Mhe. Mwenyekiti, nije kifungu cha 15(2)(a) kinasema kwamba, Mwenyekiti. Aah! *No*, samahani Mhe. Mwenyekiti. Nije katika kifungu cha 15(d), kinachosema kwamba;

> "Wajumbe wengine wanne ambao watateuliwa na waziri kati ya hao wanne, mmoja wao ni kutoka taasisi binafsi na wawili wawe wanawake".

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba nampongeza Mhe. Waziri kwa kuthamini sana wanawake na kuithamini sana *gender*, kwa sababu hili ni wazo zuri na pahala popote pale ikiwa hapana mwanamke Mhe. Mwenyekiti, inakuwa ni vigumu. Lakini pia, niseme katika uteuzi wake wa hawa watu wawili waliobakia nipendekeze, aidha awateuwe mwanamke au mwanamme lakini awe mzee ambaye ana sifa katika bodi na pia ana uwezo wa kuifanyia kazi bodi.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 326 kifungu cha 16. Mhe. Mwenyekiti, samahani kidogo imenitatiza. Hii inasema kwamba "Mjumbe wa bodi ataweza kujiuzulu" sijaiona bado, lakini nategemea kwamba naifahamu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niseme mjumbe huyu atakapojiuzulu ni lazima ijulikane kwamba mjumbe huyu kajiuzulu kwa sababu gani. Kwa sababu siku nyengine mtu anaweza kujiuzulu na hatimaye pengine ikawa ana kosa katika bodi alilolifanya au pengine kuna sababu nyengine ambazo zimeshatokezea.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na hili pia atueleze kwa sababu mjumbe anapotaka kujiuzulu, aidha ikiwa haumwi au hana matatizo kwa kujiuzulu tupu inakuwa haiwezekani ni lazima aeleze sababu za kujiuzulu na bodi vile vile nayo ifanye uchunguzi wa sababu hiyo ya kujiuzulu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 331, Sehemu ya Tano, inayosema;

> "Kutakuwa na wataalamu wasiopungua wawili kwenye fani tofauti ya uzoefu wa mahusiano wa mabadiliko ya tabianchi".

Mhe. Mwenyekiti, pia, niseme hapa panahitaji elimu ya kuwaelimisha wananchi wetu, kwa sababu wengine hawajui mabadiliko ya tabianchi. Kwa hivyo, ningeomba Mswada huu utakapopitishwa, vile vile, ufanye kazi kwa wananchi wetu kuwaelezea maana ya mabadiliko ya tabianchi.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, kwenye Sehemu ya Sita, usimamizi wenye uwiano ukanda wa pwani.

Samahani Mhe. Mwenyekiti, nimekosea kidogo. Nije kwenye Sehemu ya Kumi na Mbili, inayosema, uhifadhi wa *bioanuwai* na usimamizi wa vyanzo vya maji.

Mhe. Mwenyekiti, na hapa pia namuomba Mhe. Waziri itakapopitishwa sheria hii na kufanyakazi, vile vile, atowe elimu kwa wananchi wetu na kutoa maana ya *bioanuwai,* kwa sababu watu wetu hawaelewi maana yake na wanahitaji kupatiwa elimu hiyo ili waweze kukaa vizuri na wasiweze kuharibu hicho kilichokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Sehemu ya Kumi na Sita, ukurasa wa 342. Mhe. Mwenyekiti, nije Sehemu ya Kumi na Sita, ukurasa wa 347, katika kifungu cha 4(a) kinachosema kuingia katika jengo chombo cha majini, angani, nchi kavu au sehemu nyengine yoyote itakayotuhumiwa kwa madhumuni ya kutekeleza sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, nitowe pendekezo hapa niseme kwamba kuingia katika jengo chombo cha baharini, angani, nchi kavu au sehemu nyengine yoyote itakayotuhumiwa kwa madhumuni ya utekelezaji wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho niseme kwamba naiomba serikali izingatie sheria hii ya sasa kuhusu suala la uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, kwani ni moja ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira ni uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri alizingatie sana hili suala la uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, kwa sababu hiki ni kitu kimoja wapo chenye uharibifu wa mazingira. Baada ya hapo niseme ahsante sana nakushukuru.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi nikachangia machache kwenye Mswada huu ambao ni Mswada muhimu kwetu sisi pamoja na wananchi wote kwa ujumla, kwa sababu Mswada huu unamuhusu kila mtu.

Kwanza nichukuwe fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake, akiwemo Katibu Mkuu wangu wa zamani Dr. Shajak, niwapongeze sana pamoja na Wakurugenzi wake wote kwa kazi nzito ambayo wamefanya ya kutuletea Mswada huu leo na niwaombe wenzangu kama kawaida tuujadili na tuuchangie kisha tuupitishe.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu kama ulivyoeleza kwamba madhumuni yake ni kuanzisha sheria ambayo kabla ya hapo kulikuwa kuna sheria ya usimamizi wa mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu namba 2 ya mwaka 1996 na badala yake kuweka masharti bora ya uhifadhi, kulinda na kusimamia mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu kwamba huu Mswada ni mzuri na ni Mswada mrefu sana ambao una vifungu 87 kwa ufupi hapa ni vifungu 87, ambavyo vina sura karibuni 10 na sita kwa kweli nimpongeze tena Mhe. Waziri na mimi nafikiri nitumie fursa hii ingawaje Kanuni imesema kwamba jana tumesomewa vifungu vya Kanuni, lakini na mimi niseme wajina wangu kafanya kazi nzito na ngumu na siku zote jina hili linakuwa na msimamo.

Vile vile, ni jina ambalo saa nyengine linakuwa linapata mitihani mizito, lakini kwa uwezo wa *Allah,* Mwenyezi Mungu atatusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niende na ukurasa wa 320 mpaka 322 ambao ulikuwa na ufafanuzi na niende na ufafanuzi ambao unasema *bioanuwai* hata kulitamka kidogo linanipa ukakasi, lakini *bioanuwai* maana yake ni

viumbe hai vyote ukijumuisha, wanyama, ndege na viumbe hai wengine wasioonekana kwa macho wanapatikana kwenye mazingira ya nchi kavu na majini yote hiyo ndio *bioanuwai*.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni elimu tosha ambayo tumeipata wengi tulikuwa hatujui *bioanuwai* ni nini, lakini leo imeshatwambia kwamba ni vitu vyote vile *living things* na *non-living things* vyote vinakuwa katika moja wapo. *Subject* yangu ambayo nilikuwa nikiipenda sana na kwa bahati mbaya nikawa sikuweza kuendelea shule, lakini kwa kweli nilikuwa naipenda sana *subject* hii na leo niseme kwamba kwa miaka mitano hii nimepata mambo mengi katika kuweko humu ingawaje haijafika hiyo miaka mitano hivi sasa ni miaka minne. Lakini nimepata kusoma mambo mengi na kujikumbushia mambo mengi.

Kwa sababu watu wanasema elimu haina mwisho, lakini elimu haina mwisho isije ikawa ile khadithi ya mtoto aliyeamka mapema kwa sababu anaambiwa elimu haina mwisho, akaamka mapema siku hiyo, anaulizwa kwa nini umeamka mapema, akasema nakimbilia badia za mwalimu kwa sababu elimu haina mwisho.

Kwa hivyo, lazima tuzingatie kwamba elimu haina mwisho, lakini bado tunaweza kujifunza na tusifuate tu kwa sababu elimu haina mwisho, lakini ina mwanzo na lazima kitu chochote ukipate bado kingali maji, wanasema hata udongo ubakize upatize ungali maji. Sisi wanadamu kila tunapokuwa basi tunapoteza nguvu hatuwi na nguvu pale pale, tunapoteza vile vile fahamu pia zinapungua.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, niseme hivyo na nikienda tena kwenye Mswada huu nasema kwamba sheria hii jukumu la kulinda mazingira ni kwamba kila mmoja wetu ana wajibu wa kulinda mazingira kwa manufaa ya vizazi viliopo na vizazi vijavyo, kama kila mtu atakuwa na wajibu wa kulinda mazingira, basi nafikiria ni jambo la msingi kabisa.

Kwa sababu mazingira ni uhai wetu ukichafua mazingira kwa aina yoyote ile basi umeshajinyima mwenyewe uhai wako, sijui kama hutokuwa mtu wa ajabu kwa sababu kama huyu mtu anajiua mwenyewe basi sijui kuwa kama atakuwa na akili timamu au tumtie katika fungu gani mtu huyo bila ya shaka atakuwa kachanganyikiwa. Kwa hivyo, niwaombe wenzangu kwamba kila mmoja wetu tujue kwamba atuna jukumu la kulinda mazingira.

Vile vile, niseme kwamba Sehemu ya Tatu ambayo inasema kwenye *marginal note* uanzishaji wa Kamati ya ushauri wa mazingira mimi niunge mkono tu kuanzishwa chombo hichi ambacho ni muhimu, ni lazima unapoandaa sheria basi kuwa na Kamati kama hizi kwa mujibu wa ile taasisi husika.

Mhe. Mwenyekiti, kazi za Kamati vile vile nimeziona katika ukurasa wa 324 ambayo humo humo kuna mikutano ya asili na akidi ya Kamati za ushauri wa mazingira, uwezo wa Waziri ni lazima kwenye taasisi kama hizi Waziri naye ana nafasi yake katika jambo lile husika.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona vile vile kwenye Mkurugenzi kifungu cha 12(1), kutakuwa na Mkurugenzi wa Mazingira ambaye atateuliwa na Rais au pawe na Mwenyekiti ambaye anakuwa ni msimamizi.

Lakini vile vile, nimeona namna ya huyu Mkurugenzi ili aweze kuteuliwa kuwa Mkurugenzi kwa mujibu wa kifungu kidogo Namba 1 ya kifungu hichi ni lazima awe na sifa zifuatazo:

1) Kiwango cha elimu kisichopungua Shahada ya Kwanza au inayolingana nayo katika kinachotambulika na Serikali, kati ya moja ya miongoni mwa fani hizo.

2) Fani ya usimamizi wa mazingira, uhandisi, mkolojia sayansi ya bahari, Sheria ya Mazingira, sayansi ya mazingi, mabadiliko ya tabia ya nchi, usimamizi wa maliasili, maendeleo endelevu na fani yengine yoyote inayohusiana na usimamizi wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, naona hizi fani ni nyingi sijui kama nimuulize Mhe. Waziri kwamba mtu mmoja anatakiwa awe nazo zote hizi au labda katika moja ya hizi naomba na kwa sababu Mswada najua Mhe. Mwenyekiti, Miswada ni mingi na kusoma vile vile inatakiwa uwe makini sana na vile vile kwa sababu hatujajiandaa vizuri kusema kweli na ndio maana nikawa nauliza hilo kwa sababu nilivyousoma *deep* sana labda ningefahamu, lakini kwa kupitia juu juu ningeomba labda Mhe. Waziri atakapokuja anifahamishe juu ya fani hizi.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu ni mzuri na vile vile ninavyoona katika Mswada huu ni lazima Mhe. Waziri kuna taasisi nyengine itabidi ashirikiane nazo, tuseme ardhi atakuwa ni Waziri wa ardhi na yeye anahusika hapo, Waziri wa Habari kupitia kile kitengo cha mambo ya kale na taasisi nyengine nyengine bila ya kushirikiana na hao, ingawaje kwenye sheria kwenye zile Kamati zile nimeona kwamba kuna watu karibuni wa aina hiyo.

Lakini kuna maeneo kama yale ya kihistoria tumeziona hata kwenye kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwamba kuna maeneo kwa mfano Mkamandume mpaka lile bango lenyewe sasa limeshakuwa hai hoi, limekuwa hoi.

Kwa hivyo, maeneo kama yale yanatuingizia fedha nyingi za Serikali kupitia watalii, lakini inaonekana hata uhifadhi haupo na hiyo ni kupoteza historia kubwa ya nchi yetu, kwani historia tunayo, lakini nia ni nzuri na sehemu zinavutia ambazo zitatusaidia kwa kutuingizia fedha nyingi tu na kutuondoshea matatizo mengi ambayo nchi yetu kutokana na hali yanatukwaza kutokana na kutokupata fedha za kutosha. Tumeona maeneo hayo karibuni tulikuwa kwenye Kamati ya *PAC* tulikwenda mpaka Mkumbuu ambako tumeona kwamba kuna urithi mzuri tu na una thamani kubwa, lakini mpaka sasa haijashughulikiwa ipasavyo.

Vile vile, tumeona uingiaji wa bahari katika maeneo na kuna eneo tumeambiwa tokea *century* ya tano nafikiri kama sikosei tayari kulikuwa na makaburi huko na kulikuwa na mji na sasa hivi haupo umeshachukuliwa na bahari kusema kweli, kwa hivyo, pale maeneo ambayo yaliyobakia basi ni vizuri Serikali kupitia Wizara yako Mhe. Waziri kwa uwajibikaji wetu na kwa lengo lile lile la uwajibikaji mzuri, basi maeneo haya si vibaya pia kama Wizara yako pamoja na watendaji wako kwenda kuyaona yale maeneo ya historia ambayo kwetu ni *heritage* kusema kweli na pale tumeona historia kubwa ambayo mambo ya *akiologie* ambayo kunakuwa na mambo mengi ya kihistoria ambayo watafiti mbali mbali kutoka ndani na nje ya nchi yetu huwa wanakwenda kutafuta.

Na mimi nasema ni *very interesting* kwa sababu mtafiti anakwenda kutizama pale anajua kwamba kuna vitu ambavyo vimetokea tokea kwenye *century* ya tano, anasema hapa kwamba kakuta maiti, anasema huyu maiti alikuwa ni hivi na hivi. Kwa hivyo, hata zile rangi za vile vitu pia vinakuwa vinavutia mtu kujua historia hapa kwamba mwaka fulani, huyu alikuwa ni maiti au mtu wa miaka fulani, maeneo haya yawe yanahifadhiwa ili kwa kuleta historia na vile vile kuleta mapato katika nchi yetu.

Mhe. Waziri, huu Mswada ni mzuri tena ni mrefu sana kama walivyokwisha kusema wenzangu tena ni muhimu sana, vile vile, niseme kwamba hii kutupa taka za hatari kwenye Sehemu ya Kumi ya uzuiaji wa uchafuzi wa usimamizi wa taka. Mhe. Waziri katika katazo la uchafuzi kifungu cha 51(1) kinasema;

> "Marufuku kwa mtu yeyote kuchafua au kumruhusu mtu mwengine kufanya kitendo kinachosababisa uchafuzi wa mazingira kwa kukiuka viwango vyovyote vya kimazingira vilivyowekwa na Sheria yote inayotumika".

Mhe.Waziri, mimi leo nimepata kujua kwamba pale saa nyengine inapoanzishwa taasisi ikaambiwa kwamba ina haki ya kushitaki na kushitakiwa, kweli ni vizuri kuweka kwa sababu una haki ya kumshitaki Waziri wa Afya kwa kuchafua mazingira endapo kwamba atatupa taka taka zake mahali ambapo tuseme baharini, basi na yeye atakuwa na haki ya kushitakiwa na taasisi nyengine.

Kwa hivyo, hapa niseme kwamba hiki kifungu na mimi nakitilia mkazo, jana wenzangu walisema hapa kwamba niliona kama labda tunaleta ubishi kwamba itakuwaje mtu ashitakiwe au apige mtu labda asishitakiwe, lakini kwa kweli tunajenga mazingira yetu wenyewe au tunafanya vile kwa sababu ya kukimbiza kile kitu ambacho kinafanyika, kila mtu atakuwa na woga sasa wa kufanya kile ambacho tunakikataza.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri, nipongeze sana kifungu hiki na sasa ndio nimejua kwamba kweli kuna haja mtu yeyote yule ambaye atafanya hata Wizara yenyewe kama nini, basi ishitakiwe kama imefanya kosa lile.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kifungu cha 65(1) uhifadhi wa vyanzo vya maji, unasema kwamba ni marufuku mtu yeyote kuharibu na kuchafua kwa namna yoyote, hapa kwanza napenda si namna yoyote ni mtu tu ndio tunaweza kusema mtu yeyote, lakini hapa iwe namna yoyote kiswahili ni lugha yangu nasema siku zote kiswahili kinanipa tabu, lakini si kwa sababu najua kiingereza ata, kiswahili kinanipa tabu namna ya kutafsiri na ndio lugha ambayo kiswahili

kilikuwa kinanipa tabu sana skuli, ilikuwa maksi zangu sivuki kwenye 35. Lakini Sayansi hii nilikuwa napata 80, 90 pamoja na hesabu.

Mhe. Mwenyekiti, hayo ni mambo ambayo nimeyaona, lakini kuna Sehemu ya 13 nimesema usimamizi wa mabadiliko ya tabianchi, taasisi kwenye kifungu cha 66 kinasema;

"Taasisi za maana ya kusimamia mabadiliko ya tabia ya nchi".

Halafu kifungu 66 kinasema;

> "Wizara inayohusika na mazingira ndio itakuwa taasisi yenye dhamana ya kuratibu masuala yote yanayohusu mabadiliko ya tabianchi, tunaona namna gani sasa hali inavyokuwa tunapokata miti, hali ya viwanda ambayo sasa hivi tunajihatarishia maisha yetu sisi wenyewe".

Kwa kweli tumeshafika katika hali ambayo ulimwengu huu kwamba joto sasa hivi limeshazidi na linaifanya sasa zile barafu kuyayuka na kuzidi kwa maji ya bahari. Kwa hivyo, tusifanye mchezo hata kidogo kukata kata miti ovyo, kuchimba michanga hiyo, kukata mawe au kuchimba mawe kwa sababu yote hayo ni moja ya uchafuzi wa mazingira.

Tunajua kwamba wengine ni sehemu yao ya kipato, lakini saa nyengine inaweza ikasababishia vile vile kuna kware nyingi tu za uchimbaji wa mchanga pamoja na mawe na hizi ndio zile mali zisizohamishika, nilikuwa najiuliza mali zisizohamishika ni zipi, lakini kwenye Mswada wako humu umetuelezea kwamba mali zisizorejesheka na hizi hazirejesheki kweli.

Lakini tutumie *carrier* hii ili tuone kwamba wote tunawajibika kuondosha tatizo hili kwani ukikata mti basi unatakiwa upande mti na kwa sababu ukisema unaukata mti wewe mwenyewe unategemea utapata wapi hewa na tunabadilishana sisi na miti, tunatoa *carbondioxide,* mwalimu atanisaidia hapa na tunavuta *oxygen* tunabadilishana na ile miti, kwa hivyo, tukikata miti ina maana tunajihatarishia maisha yetu sisi wenyewe.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, niseme kama tutakata miti kwa wingi basi hata ile lishe bora tutakuwa hatuna. Kwani hata miti nayo ili kufanya uzalishaji wa mauwa lazima kupatikane chakula cha kutosha kutoka chini ya ardhi, maji, kama tutakata miti ovyo basi hata mvua zitakuwa hazipo na maisha kwa kweli yatakuwa hayapo. Kwa hivyo, hii sheria yenyewe ni nzito na ni nzuri na ni lazima tuijadili, tuiboreshe na kisha tuipitishe.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya 14, kuna vifungu vya fedha, kama kawaida kifungu hiki huwa napenda sana kwenye sehemu hii kukichangia kwa sababu ndio fani yangu. Kifungu cha 70 ambacho kinasema fedha za Mamlaka, sasa Mamlaka itakuwa na voti yake kwa fedha zote zitakazopitishwa na Baraza la Wawakilishi na fedha nyengine kutoka vyanzo vyengine vya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, hii voti*,* mimi nilisema voti labda ile ya kupiga kura. Kwa sababu hakuna neno voti kwa kiswahili, kwamba ni labda hapa tubadilishe kuwa na kasma au kifungu, baada ya kusema voti.

Mhe. Mwenyekiti, humu sijaona sijui kamba nime *overlook,* lakini viel vile sijaona kwamba fedha hizi, ingawaje imekuwa ni kitu cha kawaida, lakini kuna siku Mkurugenzi atasema mimi sijaandikiwa kwamba nikaguliwa na nani na wala hamna ruhusa ya kunikagua, kwa sababu kwenye sheria hamna, sasa utakujaje na sheria ambayo haikuelezea hayo. Kwa hivyo, hiki napenda humu itiwe, kawaida watu wanasema kitu cha kawaida kinakuwa kuna sheria. Lakini hata hivyo lazima zitiwe.

Mhe. Mwenyekiti, tuseme kwamba katika Mswada huu nimefarijika sana na baada ya hayo niseme kwamba naunga mkono Mswada huu Mzuri, upite vizuri na kwa niaba ya wananchi wangu wengi walionipa kura zao na wale waliokuwa hawakunipa kwa niaba yao, naunga mkono Mswada huu mia kwa mia.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nitoe shukurani zangu za dhati kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kwa ufupi kabisa Mswada huu muhimu ambao ni Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa Ajili ya Maendeleo Andelevu Nam. 2 ya Mwaka 1996 na Kuweka Badala yake Masharti Bora ya Kuhifadhi, Kulinda na Kusimamia Mazingira Zanzibar na Mambo mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuchangia niseme kuwa mimi naipongeza Wizara kwa kuleta Mswada huu ambao moja kwa moja unagusa maisha ya binaadamu na viumbe vyake. Lakini masikitiko yangu makubwa na kabla ya masikitiko hayo pia nitoe pongezi za dhati kwa wataalamu waliotayarisha Mswada huu kwa sababu ni Mswada wa kitaalamu, kama tutaweza kuufanyia kazi ipasavyo kwa maslahi ya Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu ulikuwa upewe muda tuweze kuutafakari na kuuchangia zaidi ili ueleweke kwa kila mwananchi wakati kila mwananchi anatakiwa kuyalinda hayo mazingira ajue vilivyo na sisi ndio watumishi wao. Kuletwa kwa haraka haraka mimi inanisikitisha sana, kwa sababu lengo lililokusudiwa halitofikia kama lilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kama tunavyojua umuhimu wa mazingira ambao umuhimu huo kiutalamu umetolewa katika Mswada huu ikiwa ni mambo yote yanayomzunguka binaadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji na kila kitu kilichomo ndani yake chenye uhai na kisichokuwa na uhai na maingiliano na mahusiano ya vitu hivyo na mazingira yao pamoja na mahusiano na maingiliano ya vitu hivyo na binaadamu.

Mhe. Mwenyekiti, hayo ni maneno tu ambayo yameandikwa lakini ni maneno makubwa sana. Mwenyezi Mungu alivyoumba ardhi hii aliumba na viumbe vyake. Viumbe ni tofauti na vitu vilivyokuwa havina uhai. Viumbe vyenye uhai vina mbinu zake za kuishi na vinategemeana. Ndio maana kila palipo na uhai, penye miti panakuwa na wanyama na viumbe vyengine na maisha ya hapo ndiyo yapo. Kwenye maji kunakuwa na wanyama wanaoishi na viumbe vyengine na pia uko uhai uko kwa kutegemea na vile vile ndio ilivyo kwenye hewa.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo mambo yalivyowekwa ndivyo maisha yanavyokwenda na ikitokezea kwa bahati mbaya uchafuzi za mazingira ukitokea ikawa asilia moja ya uhai inatoweka, kwa hivyo, mfumo wa maisha unabadilika na athari yake huwa inajitosheleza. Sasa kuletwa Mswada huu kuona kuwa vile hali ilivyo inakuwa ni endelevu. Ndio maana mimi nikasema kuwa napongeza sana isipokuwa tu Mswada huu umetolewa kiharaka haraka sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mswada kuna neno linaitwa "ikolojia" na limetafsiriwa vizuri tu, kuwa ni eneo lenye mfumo mmoja wa kimazingira ambalo ndani yake vimo viumbe vyenye uhai na visivyo na uhai vinavyotegemeana pamoja na mazingira yao. Kutegemeana hili ni suala muhimu sana. Sasa tukisema kuhusu uchafuzi wa mazingira maana yake baada ya maelezo haya niliyotanguliza ni kuingia kichafuzi, yaani *pollutant* kwenye mazingira kwa kiwango ambacho kinaweza kuathiri mfumo wa *kiikolojia, bioanuai* au kusababisha mabadiliko mabaya ya mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naanza kuchangia baada ya kutoa maelezo hayo kama ifuatavyo. Tunajua katika dunia hii kuna binaadamu, nchi na nchi zinazotafautiana kiuhalisia katika mazingira yao, kwa kuweza wao kujiendeleza. Kuna nchi tajiri na kuna nchi masikini, lakini kwa vyovyote binaadamu anahitaji kuishi. Sasa kinachomfanya binaadamu aweze kuishi ni ardhi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikizungumza ardhi nakusudia pamoja na hewa na maji, isije ikaonekana ardhi kavu tu. Kuna wengine ni wakulima, kuna wengine ni wavuvi na kuna wengine wanaendesha maisha yao kutokana na hali halisi ilivyo.Wengine kazi yao ni kukata mawe na kusomba mawe na kuuza kuendesha maisha. Wengine kazi zao ni kuchota mchanga au kuchimba mchanga na kuuza kuwendeshea maisha yao. Wengine kazi zao ni udereva, wanaendesha mpaka magari mabovu yanatoa hewa chafu katika hewa lakini ndio wanaendesha maisha yao.

Kwa hivyo, kutokana na kazi za kibinaadamu za kumuendeshea maisha, siku zote kunakuwa na uharibifu mkubwa wa kimazingira na bila ya kuwepo na uharibifu huo, maisha yatakuwa hayapo. Sasa basi kuiweka nchi hii katika hali hasa ya kuweza kuhifadhi mazingira yake kama Mswada unavyoeleza, kunahitaji kuwepo na mfumo maalum. Kwa sababu hili ni jambo la kitaifa sio la Kiwizara kama tunavyoliona, limeletwa na Wizara kwa sababu ndio Wizara husika ya haya mambo.

Tuangalie hivi sasa binaadamu ili aweze kuishi ni lazima ajenge, hakuna utaratibu wa kukuza upandaji wa miti katika nchi hii. Watu wanakata miti mingi sana kwa kujenga. Miti wanaipunguza, ni viumbe hai na wanaharibu mazingira kwa upande mmoja, kwa mfano miti inajifanyia chakula chake katika utaalamu Mwenyezi Mungu ameuweka, lakini mwisho wake kunatoka hewa inayoitwa *oxygen* katika kufanya hicho chake, tunatumia sisi ili tuweze kuishi kwenda kwetu kula kwetu na kuishi kwetu tunategemea hewa hiyo.

Katika kuivuta hewa hiyo na sisi vile vile tunatoa hewa mkaa (*carbondioxide)* ambayo miti inaitumia kwa kufanya chakula chao. Kwa hivyo, kuna maingiliano makubwa sana baina ya viumbe, wanyama na miti katika maisha yao, bila ya miti wanyamba hawawezi wakaishi na kinyume chake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, kukata miti ovyo ni kuleta athari kimaisha katika jamii, hivyo, ni kuchafua mazingira. Lakini Zanzibar hakuna mpango wa kuotesha miti kwa wingi kama wanavyofanya watu wengine katika nchi zao ili ukiondoa miti hii mengine ipo tayari inachukua nafasi zake, matokeo yake miti inakatwa, athari inajitokeza na zaido ya hivyo miti pia inasaidia kurutubisha ardhi, ardhi inakuwa kavu, miti ya zamani haipo, hivi sasa vyanzo za maji vimekauka, idadi ya watu inaongezeka.

Kwa hivyo, kwa hili tu ni mfano kuwa kunahitaji kufanyiwa kazi kubwa sana ili Mswada huu huweze kwenda wenye nia safi ya kuokoa maisha ya viumbe.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuna watu wanajenga nyumba za tope mpaka leo kutokana na umasikini wetu. Lakini kuna watu wanajenga majumba ya tofali, matofali yanayofanywa kwa kutumia saruji na matofali yananayopatikana kwa kuikata ardhi yaani jiwe, kama utatumia saruji ni lazima uchimbe mchanga. Yapo majumba makubwa na mengi yanayoendelea kujengwa, uchimbaji wa mchanga ni mkubwa mno.

Unapoondoa kitu cha mali ya sili isiyorejesheka maana yake pale umeharibu mazingira. Wengine kwa bahati mbaya hasa kwetu kule Pemba tunaikata ardhi hasa na kufanya mashimo makubwa na kubadilisha mfumo wa maisha na huku pia ni kuchafua mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo, umeletwa Mswada huu wa kuhifadhi mazingira na wakati mazingira yanaharibiwa kiasi ambacho nimekieleza. Je, ni mambo gani mbadala yamewekwa kwa wananchi waweze kuendesha maisha yao katika mfumo nilioueleza na wasiweze kufanya hizo shughuli zao za kimaisha ambazo zinasababisha uchafuzi wa mazingira katika hali niliyoitaja. Hiyo ni sehemu moja tu.

Tuende kwenye bahari, nchi yetu ni visiwa. Watu wengi wanaishi kwenye bahari kwa kupata chakula chao. Kuna wale wavuvu, ambao katika bahari kila eneo kama ilivyozungumzwa ikolojia. Kuna viumbe wanaishi kwa kutegemeana, hapana samaki mkubwa palipokuwa hapana samaki mdogo. Hapana samaki mdogo palipokuwa hapana majani. Hawawezi wakaongezeka samaki kama hakuna mazalio.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa sababu ya maisha ya binaadamu, kuna watu mpaka leo na kwa sababu hawana uwezo wanatumia nyavu ambazo hazitakiwi kutumika, wanavua samaki waliokuwa pia hawatakiwi wavuliwe, uzazi wa samaki unapungua kwa uvuvi haramu na kama ilivyo nchi kavu hata bahari nayo inakauka. Wachilia mbali wale wanaochimba mawe tunaita matumbawe kwa kujengea huku ardhini. Haya mambo yanafanyika kila siku, mazingira yanaharibiwa na sisi tumefanya Mswada huu muhimu sana wa kuhifadhi mazingira.

Je, tumewapangia vipi watu hawa waweze kuishi katika maisha yao ya kujituma. Lakini maisha yanayoendelea kwa uchafuzi wa mazingira kupita kiasi kama nilivyoeleza, mpango gani tumewapangia ili maisha yao yaende na huu Mswada uweze kufanya kazi ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, kwenye hewa ambapo hewa ni lazima tuipate ambao tuweze kuishi, kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira. Mambo mengine yamo katika uwezo wetu na mambo mengine ni kwa sababu ya maendeleo ya nchi za wenzetu zilizoendelea. Tumeingiliwa na tabia ya nchi, tabia ya nchi hii imesababisha kuongezeka kwa hewa mkaa na dawa yake ni kupanda miti kwa wingi.

Hewa mkaa hii imesababisha na kuongezeka kwa joto duniani, mabarafu kuyayuka na maji kuongezeka, kima chake kuzidi na kuleta athari kubwa kutokana na hali ya ardhi ilivyo na hii yetu iliyokuwa haina milima mikubwa kuingia mpaka katika sehemu ambazo wananchi wanaendesha maisha yao.

Kwa hivyo, kila siku tunafikwa na tatizo hili, hili halimo katika mamlaka yetu. Sijui serikali kwa kupitia Wizara inamahusiano gani na dunia wanaofanya shughuli zao za maendeleo, lakini athari ikawa kubwa ili kuona *at list* tunapata fidia ya kuweza kujiimarisha kupambana nayo, kwa sababu hatuna uwezo wa kuyafanya Mataifa makubwa yasifanye shughuli zao za maendeleo kutokana na hali ya dunia ilivyo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, hii safari ni ndefu, tusiiyone kuwa ni rahisi, inataka matayarisho na matayarisho yenyewe ni gharama na ya kitaalamu ili Zanzibar ambayo ndiyo tunayoishi ibakie katika hiyo hadhi Mhe. Waziri kwa makusudi aliyokusudia kwa kuona athari yake ili nchi hii isalimike kimaisha. Hilo ni moja.

Mhe. Mwenyekiti, kunakuwa kunazungumzwa zungumzwa kuhusu uchimbaji wa mafuta na gesi, unaweza kuchafua mazingira kama tutakuwa hatuna uangalifu wa kutosha. Hilo ni kweli tumeona katika nchi za wenzetu zinazoendelea safari moja ilipasuka bomba la mafuta viumbe baharini walivyoathirika ni wengi sana, tunajua mafuta ni mepesi kuliko maji, mafuta yanabakia juu ya maji na viumbe vinavyoishi katika bahari vinapata athari, vinakufa bure kwa sababu ya mafuta.

Ni kweli ni hatari sana uchimbaji wa mafuta unataka utaalam hasa mafuta yanayochimbwa kwenye bahari. Kwa vile Zanzibar inazungumzwa kuwa ina vitalu vyenye mafuta na gasi nyingi sana na tunaelekea katika uchimbaji wa mafuta Zanzibar na Mungu ajalie awe ni ya Wazanzibari na huu ni utajiri utakaotufanya sisi kuweza kuziba mapengo ya ufukara tulionao.

Lakini mimi niulize, kutokana na hali ilivyo kama patachimbwa mafuta hapa Zanzibar imedhatiti kiasi gani kiutaalam ili kuona kuwa athari haitakuja kutokezea kiasi ambacho hatuwezi kuimudu ikawa kuchimba ni majuto kwetu sisi badala ya kupata faida.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho katika Mswada huu kuna kifungu cha 34 ambacho naomba kidogo nipate maelezo. Kifungu hiki kinaeleza kama ifuatavyo:

> "Kuwa mtu aliyepewa kibali cha uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka atakuwa na jukumu la kuendeleza eneo lililochimbwa na halafu kuna mambo mengine yanafuata huko chini".

Mhe. Mwenyekiti, sasa tuseme kama mtu kachimba mchanga baharini hivyo eneo lile litarejesheka vipi, yaani mchanga ushachukuliwa na ni maliasili iliyorejesheka, si patabakia shimo tu na maji yataendelea usoni! Hivyo, mtu ukenda kukata mwamba kule Vitongoji na kutengeneza matofali kwa ajili ya kujengea, shimo lile la mwamba si la udongo alifanye fanye vipi ili alirejeshe au arejeshe vipi ili ionekane kuwa hicho kirejeshwaji kinatoka wapi katika kisiwa hiki kidogo ikiwa hakwenda akabomoa huku kwa kujenga huku.

Hivyo, mtu kenda kuchimba mawe baharini arejeshe vipi hali pale na halafu kuna *fine* na nini na kadhalika kama suala hili halikutekelezeka ipasavyo, kwa hivyo, naomba nipate maelezo hasa hizi shughuli zikianza baada ya kupitishwa mswada huu, zitakuwa katika mkakati gani wa utekelezwaji ipasavyo ile athari isijitokeze kutokana na kuwa mimi nikiona mambo mengine hayawezekani.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho, ninaloomba kuzungumza ni kuwa mswada huu ambao mimi naunga mkono sana ni mzuri, lakini Mhe. Waziri kwa sababu ya mswada huu umetoka haraka haraka lakini yeye kauona tokea zamani atueleze zile njia alizopanga kupambana na uharibifu huu wa mazingira ambao uliendelea na nina hakika ni vigumu kuweza kupanga usiendelee kutokana na hali ya maisha yetu yalivyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nashukuru.

**Mhe. Farida Amour Mohammed:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi kutoa mchango wangu mdogo. Kabla ya kutoa mchango naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndie aliyetupa uzima na afya njema tukakutana leo katika Baraza lako hili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea mswada huu muhimu sana kwa maslahi ya nchi yetu, ingawaje huu mswada umechelewa kiasi fulani, lakini *Inshaalla* Mungu ajaalie tupate hekima nzuri za wananchi wetu ili kutekeleza mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba niseme naunga mkono mswada huu asilimia mia moja pamoja na wanawake wa Wilaya ya Wete Mkoa Kaskazini Pemba kwa umuhimu wake kwa mustakbali wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mazingira linahitaji mikakati na umakini wa Serikali yote hauishii katika kutunga sheria tu. Nasema hivyo kwa sababu unapodhibiti uharibifu wa mazingira, unabadilisha mazoea ya mfumo ya wananchi wetu, sasa kwa Serikali kabla ya kukurupuka tu na kutunga sheria, kwanza inabidi nimuulize Mhe. Waziri suala dogo hapa. Serikali imejiandaaje na kuondoa mazoea hayo ya wananchi kwa sababu unapotaka kubadilisha hili kuna wananchi wana mazoea ya mambo wanayofanya si ya kawaida.

Sasa lazima Serikali kwanza ijiandae hapa katika kuondoa mazoea hayo ya kutafuta maisha ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe mfano katika hilo, nikija kwenye utupaji wa taka, utupaji wa taka ni mazoea ya wananchi wetu wanapomaliza kusafisha maeneo yao hasa kule vijijini wanatupa taka tu katika maeneo tofauti, maeneo yaliyokuwa hayana uhakika kuwa nitupe wapi na wapi. Sasa matokeo ya mazoea hayo miji yetu inachafuka sana na inakuwa michafu kupindukia, sasa hapa ndio maana nikasema Mhe. Waziri kuuliza Serikali imejipangaje katika kuondoa haya mazoea ya wananchi wetu ya kawaida wanayoyafanya katika mazingira yao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nimuulize Mhe. Waziri tatizo hili la sheria hii imezingatia vipi na Serikali yetu imejiandaaje hili suala lililozunguka taasisi kadhaa za Serikali, je, patakuwa na umakini hapa. Kwa sababu sheria hii inavyokuja kutokana na mazingira inabidi kuna taasisi tofauti zinazoshirikiana katika kufanya haya maeneno kuwa safi. Sasa sijui Serikali itakuwa imejipanga vipi katika hali kama hii.

Mhe. Mwenyekiti, katika mifano yangu pia naomba nitoe mfano katika umwagaji wa maji machafu. Umwagaji wa maji machafu katika maeneo yetu sana yanaachiwa kutoka nje na kusababisha udhia mkubwa katika maeneo husika. Tunavyokaa ndani ya mitaa yetu tunamwaga maji na maji yenyewe hayana maeneo maalum ya kwenda, sio wengi waliokuwa na uwezo wa kuweka sehemu maalum za kufikia yale maji machafu na huleta kero kwa watu wengine. Je, kwenye miji yetu ipo miundombinu inayokusanya maji machafu kutoka kila nyuma na kupelekea sehemu husika?

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii Mhe. Waziri tatizo limezingatiwa, nikija kwenye upigaji wa mkaa, tatizo jengine kubwa ni nishati ya kupikia Wazanzibari asilimia kubwa sana katika utafiti wa sensa 2012 inaonekana ni zaidi ya asilimia 70 wanatumia nishati ya mkaa kwa ajili ya kupikia pamoja kuni.

Mhe. Mwenyekiti, na katika hili si watu wengi walio na uwezo wa kutumia umeme na gasi kwa sababu ya maisha ya watu wetu wengi. Hivyo, utekelezaji wa sheria hii utapata tabu sana ikiwa katika nchi yetu kila uchao gasi na mafuta na umeme inazidi kuongezeka bei.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa lazima Serikali ijipange vizuri sana kushusha bei hii ya umeme na gasi ili kupata kufanikisha mswada wetu huu uende vizuri. Kinyume na hivyo, itakuwa ni tatizo, watu wetu wengi ni maskini hawana uwezo wa kutumia gasi na umeme na umeme ulivyo ghali. Sasa hili litakuwa ni tatizo kubwa, itakuwa bado tunaendelea kukata miti kwa ajili ya kuhuisha maisha yao, lakini huku tukiharibu mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu bei ya umeme ni kubwa kama nilivyozungumza na watu wanashindwa kutumia umeme na gasi basi hapa nitaomba nitoe angalau ushauri wangu kidogo kwa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, suala la upandaji wa miti naomba lipewe kipa umbele na lizingatiwe katika kila maeneo na baadae Idara ya Misitu kila Wilaya iwe na vitalu vya viti inayostawi katika Wilaya husika na mashamba hayo yanapandwa miti na kutunzwa. Kwa sababu kuna baadhi ya maeneo hufanya hiyo kazi ya kupanda miti, lakini baada ya kwishapanda ile miti haina utunzaji.

Sasa bila ya kutunzwa inakuwa ni kazi bure, tunafanya kazi ya kupanda miti lakini haishughulikiwi.
Mhe. Mwenyekiti, halafu shughuli za Idara ya Misitu zinafanana sana na kwa ufanisi ya usimamizi wa mipango ya Idara hizi ziunganishwe pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, sasa la mwisho kabisa kwa sababu ya umaskini na hali ngumu ya maisha ya wananchi wetu ndio wanaosababisha kufanya kazi hii ya kukata miti na kukata matofali kwa ajili ya kujenga na kupata rizki zao. Sasa naiomba sana Serikali ilifikirie sana suala hili na kulipa uzito wa hali ya juu na kubwa zaidi naomba Serikali kupitia Wizara hii na Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais itoe elimu kubwa sana hasa vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea kutunga sheria tu tukasema tutoe na adhabu na nini watu wanapokiuka hizi sheria bila ya kuzingatia umuhimu na kuwaona wananchi wetu walivyo na hali zao ngumu za maisha halafu bila ya kuwa na elimu, kwa sababu mtu yeyote anapopewa elimu atafahamu. Lakini kwa kukaa tu ikawa mtu anaambiwa kutakuwa na sheria hii na hii ukifanya hili utafungwa basi lazima kwanza watu wapewe elimu kubwa halafu waelezwe nini faida na hasara ya kukata miti.

Kwa sababu sisi tunaona nifuraha tunakata kuni, tunapika, tunapata maisha na kusaidia vizazi vyetu, lakini hajui ile athari inayotokea baadae. Sasa naomba sana suala elimu lizingatiwe.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Ofisi yake kwa kutoona muhali katika kudhibiti matumizi ya misumeno ya moto. Naomba sana suala hili liendelee tusirudi katika hili kwani misumeno ya moto inatuathiri sana. Lakini katika hilo kwa sababu misumeno ya moto ndio inafanya kazi hiyo inatumika katika mazingira mengine kuwe na vibali maalum kwa sehemu maalum watakaoruhusiwa kutumia ile misumeno ya moto, sio kuchukuliwa misumeno ile ikakatiwa katiwa tu vitu ovyo ovyo baadae tukapata taathira ndani ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo, machache nakushukuru.

**Mhe. Abdi Mosi Kombo:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na mimi kwa kunipa fursa ya kuchangia katika mswada huu wa kuweka sheria mpya ya mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitachangia katika kifungu 25, ukurasa wa 331, Kitengo cha Mazingira na Tabia Nchi. Kutokana na hali ya mazingira ya nchi yetu, kwanza nchi yetu ni nchi ya kisiwa na wananchi wake wanahitaji sana utumiaji huo huo unaotaka kutumiwa sheria ya mazingira.

Kwanza, katika nchi ni nchi ambayo imezungukwa na bahari pande zote nne na kila mwaka bahari inapanda juu na bahari hiyo hiyo katika sehemu za fukwe ndimo mnamochimbwa mchanga kwa watumiaji mchanga.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile mswada wetu huu unazungumza juu ya sheria ya kuhifadhi mazingira, kwanza kama walivyochangia wajumbe wenzangu kabla ya kutumiwa sheria hii, wananchi wanahitaji kupewa mafunzo na elimu ya utunzaji wa mazingira baadae ndani ya nchi yetu wananchi wengi huwa wanajenga ujenzi ambao wa kiholela. Wengi wanajenga katika sehemu za fukwe ambamo ndimo mnamoharibika sana katika sehemu za mazingira.

Kwa hivyo, wizara husika inafaa kutoa elimu ya ujenzi juu ya kuhifadhi mazingira. Kwa sababu nchi yetu hivi sasa inamalizika sana kwa ujenzi holela, ujenzi ambao hauna mazingira mazuri, kwa hivyo, wizara naiomba itoe elimu hata kwa kujenga hayo majumba ambayo yatakuwa na mazingira mazuri kwa mwanaadamu.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika hii hii uwekaji wa mazingira safi, nchi yetu hivi sasa kipindi cha nyuma Serikali ilijitahidi sana kupanda miti, lakini Serikali imeshindwa kuihudumia miti, hivi sasa nchi yetu haina miti, ukipita sehemu nyingi hivi sasa kuna jua kali tu, hamna miti, hewa mbaya na chafu, kwa vile hii inasababisha uchafuzi wa mazingira. Kwa hivyo, ningeiomba Serikali kupitia Wizara hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais ili ihakikishe kila mwananchi anapatiwa miti ya kupanda angalau kila mwananchi apate ekari mbili mbili za miti.

La pili, barabara zetu hizi za mijini hasa ukitoka Darajani na sehemu nyengine hamna miti, utakuta jua kali tupu, kwa hivyo, ukosefu wa miti inakuwa na uchafuzi wa mazingira vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, tukenda katika uchafuzi wa mazingira kwa sababu mazingira yana upeo mkubwa sana hata msongamano wa magari ni uchafuzi wa mazingira, magari hayana *parking* nzuri ni uchafuzi wa mazingira.

Kwa hivyo, Serikali kupitia wizara hii ihakikishe kwamba hata yale magari ukenda pale Darajani mazingira machafu ya magari wanaadamu hawana pakupita uzuri, gari zinawekwa vibaya, *parkings* zake chafu ni uchafuzi wa mazingira. Kwa hivyo, mazingira hata mwanaadamu peke yake ana mazingira, mbali ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, naiomba Serikali kwamba itoe elimu ya kutosha isiwe mtu amechafua mazingira anakwenda kufungwa bila ya elimu, mtu anachimba mchanga anakwenda kufungwa sasa atachimba wapi na nchi yetu ndio hii, wananchi wote wanatumia mchanga na kuni. Kwa hivyo, Serikali ijitahidi kutoa elimu ya kutosha juu

ya uchafuzi wa mazingira na Serikali iweke sehemu kwa mfano utupaji wa taka ovyo, inatungwa sheria lakini wapi mwananchi akaweke taka, hapana.

Kwa hivyo, Serikali ijipange kuweka sehemu hasa za kuwekea taka, magari ya kuchukulia taka yawepo, zana za kuchukulia taka hakuna za kutosha katika nchi yetu. Kwa hivyo, naiomba Serikali kupitia Wizara hii ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais ijitahidi sana, kwanza kuweka usafi wa mazingira, yale magari ya kuchulia taka yawepo ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, nikimalizia kwamba naiomba kwanza naipongeza wizara hii kwa kutuletea mswada huu, lakini naiomba wizara ijitahidi kutoa elimu kwa wananchi kuhusu habari ya mazingira. Nashukuru Mwenyekiti.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kunipa nafasi hii kuchangia mswada ulio mbele yetu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu Nam. 2 ya 1996 na kuweka badala yake masharti bora ya kuhifadhi, kulinda na kusimamia mazingira Zanzibar, na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, wachangiaji wengi wamesema mswada huu ni mzuri, na mimi nasema ni mzuri lakini hakuna jema lisilokuwa na kasoro. Mswada huu ni mzuri lakini ukiangalia lazima iwe tumejipanga vizuri. Kwa hiyo, Mhe. Farida hapa alichangia ilikuwa kwanza tuwape elimu wananchi wetu ili kufikia hayo maendeleo endelevu, lakini kwa kuvamia tu kwa hivyo inavyoendelea basi tutakuwa na hatari kubwa mbele yetu juu ya hao wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ukizingatia katika neno mazingira lina maana pana sana, na kama lina maana pana sana limeenea sehemu zote ukiwepo juu ardhini na baharini. Lakini mimi niseme tu kwa sababu binadamu baadhi yao wanatafuta rizki zao kwa kuharibu hayo mazingira na ndio yaliyozungumka kabisa. Ukiangalia kama wachambaji mchanga lazima afanye kuharibu mazingira, wakata miti na ni mahitaji ya kila siku anahitaji mwanadamu, haya hayaepukiki. Kwa mantiki hiyo hata serikali yenyewe inaharibu mazingira.

Kwa mfano, nikienda kule kwa Mhe. Subeit kule katika mambo ya miundombinu basi wamechimba kule kwa sababu ya matengenezo ya barabara, lakini hayo mashimo yamekithiri mpaka kupita kiasi. Kile kimo walichopewa wachimbe basi wamezidi zaidi, hapo nayo ni serikali ipo katika mtiririmko wa kuharibu mazingira. Kwa hivyo, tusimuangalie tu mwananchi wa kawaida na sisi serikali vile vile tujirekebishe katika uchafuzi wa mazingira.

Lakini mimi nasema sheria hii itakapopita basi asionewe mwananchi wa chini tu, mtu yeyote lazima imguse pamoja na sheria hii ichague lakini kila mtu imguse.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu imezungumzwa hapa katika mswada huu, katika ukurasa wa 327 katika kifungu cha 18 (2) inasema Mwenyekiti anaweza kuitisha kikao maalum wakati wowote itakapohitajika. Mimi hapa napendekeza Mwenyekiti kwa kushauriana na Mkurugenzi Mkuu anaweza kuitisha kikao maalum wakati wowote inapohitajika. Naomba pendekezo langu hilo linapofaa lichukuliwe.

Lakini Mheshimiwa ni kwamba katika kuendelea na mchango katika kifungu cha 18 (1) uanzishwe ukanda maalum wa pwani wa Zanzibar, nasema katika kuanzishwa ukanda maalum wa pwani wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, hii niiweke wazi kwamba ukanda huu uwekwe vizuri katika malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu 28 (2) ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya shughuli yoyote katika eneo la ukanda maalum wa pwani bila ya ruhusa ya mamlaka. Inasema hivyo kufanya chochote kinaweza kufanywa katika ukanda huo wa pwani bila ya ruhusua ya mamlaka. Ni kweli lakini mimi nasema wavuvi wanaopita hawendi kwenye mamlaka na wanaweza kufanya mambo mengine kule bila kufika kwenye mamlaka. Kwa hivyo, tunaomba hiki kifungu kifanyiwe marekebisho makubwa hiki, heri ya hivyo basi kwanza kwa mantiki hii kingeongeza magereza. Ukiangalia sheria hii inavyotupa tungeongeza magereza kwa sababu watu wengi kama itasimamia vizuri na maelezo yanayowekwa katika vifungu hivi, basi watu wengi watakuwa wamefungwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tukiangalia ukanda wa pwani kuna mambo mengi yaliyowekwa, huu ukanda wa uchumi upo toka zamani labda ulikuwa si wa kisheria. Ukanda huu tukiangalia una Minay Bay, Linka, Tunka, Mji Mkongwe kwa Pemba kule, huu ni ukanda wa uchumi uliowekwa lakini sijui kama ulikuwepo kisheria au watu walijipangia tu na sasa hivi unataka kuwepo kisheria. Kama upo kisheria lazima tuzingatie mambo ya msingi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hiki cha 24 (3) angalia adhabu iliyowekwa. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia adhabu iliyowekwa naomba ninukuu kwa ruhusa yako.

> "Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki kidogo cha (2) cha kifungu hiki ametenda kosa na akapatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na isiyozidi shilingi milioni mia moja au kifungo kwa muda usiopungua miaka mitano na isiyozidi miaka kumi na tano au adhabu zote mbili kwa pamoja".

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia adhabu hii iliyowekwa wavuvi wetu ni wavuvi masikini na ni wavuvi wadogo wadogo hawana uwezo wa kwenda mpaka mbali, isipokuwa wanakuwa katika ukanda wa pwani. Leo mtu tangu anazaliwa anafanya mavuvi pamoja na familia yake milioni tano hajawahi kuziona, leo unasema akipata na kosa hili atafungwa miaka mitano, atatolewa faini ya shilingi milioni tano na isiyozidi milioni kumi au adhabu zote mbili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema hukumu na adhabu hii inaweza kuwa chanzo cha uonevu kwa watu wenye kipato cha chini, na wavuvi wadogo wadogo ambao hawana pengine pakwenda kufanya shughuli zao za uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi lakini sana naomba Mhe. Waziri wetu katika mswada huu akiangalie sana kifungu hiki, kama nilivyozungumza kama amekusidia hiki kufanya kazi na ikapata usimamizi mzuri, basi utaweka jela watu wengi lakini hiki kifungu hiki kitakuwa hakitekelezeki. Namuomba Mhe. Waziri afanye marekebisho sana kifungu hiki na kukiweka sawa juu ya hivyo utapambana nayo haya, angalia hivi sasa mpaka leo sheria hii haijapitishwa tunaanza kuichangia hapa, lakini huko Marumbi na Chwaka mpaka leo ni vita vitupu. Je, leo mkija kufanya ikapita hii si matatizo? Haya ni matatizo makubwa na tutakuwa hatuwatendei haki wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, hili tukiliangalia lazima tuliangalie kwa upeo tusiandike tu maneno wakati na sisi wenyewe yanatugusa. Mimi nadhani hakuna hata mtu mmoja asiyeharibu mazingira, lakini unaharibu mazingira kiasi gani jiulize, lakini hata sisi waheshimiwa hakuna mtu asiyeharibu mazingira, kwamba sisi tutajenga tukafanye na mambo mengineyo. Mimi naunga Mhe. Abdi Mossi kama alivyochangia ile hamasa ya kuhamasisha kama mtu kata mti panda mti ni vizuri zaidi, lakini hata serikali haina uwezo wa kwenda kufanya marekebisho ya kufukia yale mashimo waliyoyashimba ndio maana nasema hata serikali nayo inachangia katika kuharibu mazingira nimetoa mfano kule Micheweni hilo uliangalie sana.

Lakini kwamba haitoshi katika kifungu cha 30 muundo wa kamati ya pamoja na usimazi wa mali ya asili zisizorejesheka. Mheshimiwa kumeundwa kamati hii wametajwa hapa namba (a) naomba niinukuu.

a) "Mkuu wa Wilaya ambapo ombi la uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka limefanywa ambye atakuwa Mamlaka;
b) Mkurugenzi Mkuu wa Mahakama;
c) Mkurugenzi anayehusika na masuala ya ardhi na usajili;
d) Mkurugenzi anayehusika na masuala ya mipango miji na vijiji;
e) Mkurugenzi anayehusika na masuala ya maliasili zisizorejesheka ambaye atakuwa Katibu wa Kamati na;
f) Mkurugenzi anayehusika na masuala ya nishati;
g) Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ambapo ombi la uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka limewasilishwa na;
h) Mjumbe mwengine yeyote kutoka taasisi nyengine yoyote atakayoonekana anafaa".

Mhe. Mwenyekiti, sasa niko hapa kifungu (h) napendekeza hapa mjumbe mwengine yeyote anayetoka asasi za kiraia atakayeonekana anafaa. Naomba Mheshimiwa hii iingizwe kwa sababu huko chini ndio kwenye mambo kuliko huku juu, hapa wote wakubwa wameshapangwa lakini na hili ipendekezwe kama mjumbe yeyote anayetoka katika asasi za kiraia anaonekana anafaa aingizwe katika sehemu hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema mchango wangu hautakuwa mkubwa na Mhe. Mwenyekiti, kanipendelea tu alikuwa tayari ameshafunga mamlaka yake pale, lakini *inshaallah* naomba ile sehemu niliyosema wajumbe warekebishwe yafanye ili kwa maslahi ya nchi yetu. Ahsante sana nakushukuru Mwenyekiti.

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwanza kumshukuru yule aliyetuumba kutujaalia uhai na uzima wa afya leo hii tukawa tupo katika jengo hili ili kuweza kuyajadili na kuyapitia yale ambayo yatatupa mwelekeo kwa kuweza kuiongoza nchi yetu kwa amani na usalama.

Kwa upande wangu pia nitoe shukurani zangu za dhati kuishukuru serikali kupitia ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuweza kutuletea Mswada huu wa Sheria, ambao mswada huu ni kielelezo kwa kila mwananchi wa nchi hii na wale wageni waliopo katika nchi hii ili kuweza kuipa uhai Zanzibar kuendelea kuishi viumbe vinavyoonekana na vile visivyoonekana.

Mhe. Mwenyekiti, huu mswada unasema kwamba ni Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu Nam 2 ya mwaka 1996 na kuweka badala yake masharti bora ya kuhifadhi, kulinda na kusimamia mazingira Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.
Mhe. Mwenyekiti, kumetolewa tafsiri mbali mbali ya maneno hapa kuhusu masuala mazima ya mazingira. Mimi nakubaliana nayo Mhe. Mwenyekiti na ni kweli kwamba mazingira ndio uhai wa viumbe vyote vilivyopo hapa duniani, kila kiumbe kinahitaji kuwa na mazingira yake inategemea kiumbe hicho kiko katika eneo gani la ardhini au la angani. Kwa hivyo, kiumbe hicho kinahitaji kupata mazingira ambayo kinaweza kikaishi kwa muda wake wote huo kilichopangiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mazingira ndio maendeleo, maendeleo hayatopatikana kama hatuna mazingira. Lakini kupatikana kwa maendeleo ndiko kuchafuka kwa mazingira. Sasa kama tunavyopata maendeleo kutachafuka kwa mazingira ni lazima wataalamu waweke viwango ambavyo vitasababisha uchukuaji wa yale ambayo yataleta maendeleo hayatokwenda mno chini ili kukaja kukachafuka zaidi kwa mazingira hayo. Kama tunavyojua kwamba ardhi ni sehemu iliyo chini yake kuna kina kikubwa cha maji, na kutokana kwamba nchi yetu ni visiwa ama mambo mawili yanaweza yakatokea ama maji ya bahari au maji baridi. Kwa hivyo, kama suala ni hili la kuchafua mazingira huku kwa kupata maendeleo hatukuweka kiwango cha kwenda *deep*, basi ni kweli mazingira ya nchi yetu yanaweza yakachafuka haraka sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya dibaji hiyo mchango wangu mimi utaanza sehemu ya pili katika majukumu ya jumla ya kimazingira. Katika majukumu ya kulinda mazingira kifungu cha 3 kinasema kwamba kila mtu ana wajibu wa kulinda mazingira kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

Mhe. Mwenyekiti, hii sentensi imetubana kwamba ukitaja kila mtu, huyo mtu akiwa ni Rais, akiwa ni Katibu Mkuu Kiongozi, akiwa ni waziri, akiwa ni mtu wa chini kabisa ndiye kila mtu. Kwa hivyo, kuwe na wajibu huu wa kulinda mazingira, kwa hivyo hii ni haki ya wajibu ya watu wote hapa nchini, kulisimamia hili na kuyalinda haya mazingira. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mazingira ndio maisha, kwenye mazingira ndio kwenye maisha. Kwa hivyo, ni lazima vitu viwili hivi vinakwenda sambamba, lakini ili tuweze kuishi na ili tuweze kuyahifadhi mazingira maisha yetu ili yaboreke ni lazima twende katika *stage* maalum, huo ni ulazima twende katika *stage* maalum ili mazingira yetu yasiweze kuchafuka haraka sana.

Kwa hivyo, hapa Mhe. Mwenyekiti nasema kwamba panahitaji taaluma, panahitaji elimu ya lazima, panahitaji wananchi wetu kupewa dozi kila aina ya sekta, kila aina ya watu kila mamlaka kulifanyia kazi suala zima hili la mazingira. Kama wananchi watapata elimu basi uharibifu huu utapungua kidogo sana kwa sababu mazingira ndio maisha. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti hili sio suala la kulifumbia macho ni suala la lazima la wananchi wetu kupewa taaluma hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 4 kinasema kwamba kila mtu analazimika kuhakikisha kwamba mipango ya shughuli za maendeleo zinatekelezwa kwa kuzingatia usimamizi endelevu. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hatuwezi kuendelea kama hatukuyatumia mazingira yetu inavyopaswa. Mhe. Mwenyekiti, napigiwa makofi lakini naomba muda wangu niumalizie kwa jioni, inshaallah. Ahsante (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano yenu ambayo mmetuonesha na jioni tukijaaliwa Mhe. Rufai utamaliza dakika zako kumi zilizobakia baadae Mhe. Waziri ataendelea na majumuisho. Kwa hiyo, tutasitisha shughuli zetu hadi hapo saa kumi na moja barabara ili tuweze kuja kuendelea, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe mufike kwa wakati. Ahsanteni.

*(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MUONGOZO**

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa dhati, tuna nia njema ya kuendelea na Baraza lakini kama tunavyofahamu leo nchi yetu ina mtikisiko mkubwa kwa kufa Mshauri wa Rais kwa mambo ya utalii Zanzibar na marehemu amefika na mazingira ya Baraza kwa kweli hata kama majadiliano yataendelea itakuwa tunawaambia watu wa nje, lakini sio wa ndani. Haiwezekani kuendesha Baraza tukiwa na watu sita. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe, kwa mujibu wa taarifa yako ambayo umeitoa taarifa ya kuhudhunisha na kusikitisha, lakini ni mambo ambayo Mwenyezi Mungu ameyapanga kwetu sote. Tusisahau kwa mujibu wa taratibu zetu tulizojiwekea ikiwa kwamba kutatokea jambo kama hilo kwa mtu ambaye yumo ndani humu inakuwa taratibu kama hizo ambazo umezizungumzia Mhe. Mjumbe zinaweza zikachukua mkondo wake. Lakini kwa sababu yule mtu alikuwepo na sasa hivi yuko nje zile haki na fursa ambazo zinatumika humu kwa ajili ya Wajumbe wa Baraza hili kwa wakati huu yeye hatoweza kufaidika nazo.

Kwa msingi huo, pamoja na mahudhurio ambayo umeyaona bado si ya kuridhisha sana, lakini kwa sababu kikao kilianza toka asubuhi na sasa hivi ni muendelezo tu wa kikao hiki tunao uwezo wa kuendelea tukapata maoni ya mjumbe ambaye anataka kutoa maoni yake na baadae Mhe. Waziri akaweza kuendelea na taratibu zake. Ikiwa kama wajumbe watakuwa hawakutimia ili kuweza kupitisha vifungu na mambo mengine hapo tutatumia taratibu zilizopo katika kanuni kufikia muwafaka na mustakabali unaopaswa hasa. Ahsante sana.

**UTARATIBU**

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kutumia kanuni ya 72 kifungu kidogo cha kwanza kinachosema kwamba, Kiwango cha Vikao. Kanuni inasema kwamba: "Kiwango cha vikao vyote vya Baraza itakuwa ni nusu ya wajumbe wote".

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na sababu ambazo umesema kwa sababu mjumbe aliyekaa ametumia msiba kama ni *excuse* mimi natumia Kanuni hii ya 72 ambayo inasema: "Vikao vyote vitakuwa ni nusu ya wajumbe wote". Mhe. Mwenyekiti hatuko hata robo ya wajumbe wote. Naomba muongozo wako.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe nimepata hoja yako ya Kanuni ya 72(1) ambayo umeitumia, lakini ukiendelea Kanuni ya 72(2) mara kabla ya uamuzi wowote kufanyika ikiwa mjumbe yeyote aliyehudhuria atapinga kwa kudai kwamba mbali na Spika, wajumbe waliopo ni chini ya nusu ya wajumbe wote basi kama Spika atathibitisha kuwa wajumbe waliopo ni chini ya nusu ya wajumbe wote atasimamisha shughuli kwa muda wa dakika tano, huku mhudumu kwa maelekezo ya katibu atapiga kengele kwa vituo, yaani sio mfululizo. Kwa utaratibu huo, kitakachofanyika kwa sasa ni hili suala labda la kuweza kuakhirisha kikao hiki kwa muda wa dakika tano ili wajumbe waweze kuitwa pale walipo na baadae tuangalie nini kitakachoendelea baada ya hatua hiyo.

Kwa hiyo, kwa utaratibu huo basi, naomba kuakhirisha kikao hiki kwa muda wa dakika tano ili wajumbe waweze kuitwa walipo na baadae tuendelee na utaratibu. Ahsante.

*(Saa 11:5 jioni Baraza liliakhirishwa kwa muda wa dakika tano)*

*(Saa 11: 10 Baraza lilirudia)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante, sasa tunamkaribisha Mheshimiwa Rufai Said Rufai aendelee na majadiliano au kuchangia.

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Mhe. Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia jioni hii kunipa hali nzuri ya afya na kupata uwezo wa kuja kumalizia katika Mswada huu ambao asubuhi nilikuwa nazungumzia katika kifungu cha nne (4) ambacho kinasema: "Kila mtu analazimika kuhakikisha kwamba mipango na shughuli za maendeleo zinatekelezwa kwa kuzingatia usimamizi endelevu kwa mazingira bora".

Mhe. Mwenyekiti, hiki ni miongoni mwa kifungu adhimu ambacho kinaweza kuyaendeleza mazingira yakawa katika hali nzuri na kunusuru wimbi lile la kuharibu mazingira kama kwamba sheria hii itasimamiwa ipasavyo. Nataka niseme kwamba kifungu ni kizuri lakini hatutofikia maendeleo endelevu kama usimamizi utakuwa mbovu. Kufanya kazi kwa sheria sio kubakia katika karatasi, kufanya kazi kwa sheria kunahitaji usimamizi ulio bora. Kwa hivyo, hiki kifungu kizuri lakini la msingi ni kukisimamia ili kiweze kufanya kazi zake kama vile inavyopaswa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kifungu cha 13, kazi za mkurugenzi wa mazingira katika kifungu (f) kinasema kwamba: "Kuandaa na kutoa ripoti ya hali halisi ya kimazingira kwa Zanzibar na kuwasilishwa kwa waziri katika kila kipindi cha miaka mitano".

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki mimi kidogo nimekifanyia wasiwasi, muda wa matayarisho wa ripoti umekuwa mrefu mno, ukiangalia kwamba nchi yetu kila miaka mitano tunafanya uchaguzi. Inawezekana waziri akapokea taarifa ima mwaka wa mwanzo au wa pili wa kuteuliwa kwake katika wizara hiyo, lakini taarifa nyengine inayokuja ikaja ikakutiwa na waziri mwengine wa awamu nyengine. Kwa hivyo, ripoti zitakuwa hazitoki vizuri na wananchi hawapati kujua mazingira yao yakoje kutokana na muda huu kuwa mrefu mno.

Kwa hivyo, mimi ningeliomba sana kifungu hiki kifanyiwe marekebisho baada ya kutoa ripoti kwa muda wa miaka mitano basi angalau ndani ya miaka mitano tupate ripoti kwa muda wa miaka miwili na nusu, ili ndani ya miaka mitano wizara hii au mkurugenzi aweze kutoa ripoti zake kwa waziri ili wananchi wapate kufaidika na taarifa za kimazingira zilizomo katika nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu (i) kinasema kwamba: "kuendeleza utoaji wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine kwa mujibu wa majukumu yake".

Mhe. Mwenyekiti, hii ni kazi moja kubwa aliyopewa Mhe. Mkurugenzi ya utoaji wa elimu. Mheshimiwa tusidhani kwamba kila mmoja anafahamu nini mazingira, hiki ni kitu kigumu na japokuwa utaona kwamba mazingira ni kitu kinachomzunguka kila mtu lakini sivyo ilivyo katika ufahamu. Kwa hivyo, kupatikana kwa elimu itainusuru sana nchi na itaisaidia sana nchi ili wananchi waepukane na kufanya uharibifu wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, kitu elimu ni lazima, ni lazima, ni lazima; tukifanya hivyo itakuwa tumepiga hatua ya kuinusuru nchi kuingia katika dimbwi la uharibifu wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea kuna kifungu cha 22 hapa ambacho kinazungumza kazi za mamlaka. Mamlaka hii ina kazi nyingi iliyopangiwa na sheria hii na hizi kazi kwa kweli zimepangika vizuri. Lakini la msingi bado nasisitiza ni ufuatiliaji si hoja kupanga, tupange lakini hatima yake ufuatilie.

Kwa hivyo, katika kifungu cha (d) kinasema kwamba:

> "Kufanya ufuatiliaji wa kimazingira ambao utasaidia kuendeleza usimamizi bora na uhifadhi wa mazingira".

Mhe. Mwenyekiti, jambo lolote lile linapokosa ufuatiliaji juu ya uzuri wake ulionao basi jambo hilo litakuwa ni baya katika hayo yaliyokuwa ni mabaya na itakuwa kwamba ni wazuri wa kuandaa mipango, lakini tuna tatizo la ufuatiliaji wa mipango yetu. Kwa hivyo, kama sheria hii mamlaka itafanya wajibu wake wa ufuatiliaji tunaweza kuinusuru nchi kuendelea katika mambo ya uharibifu wa mazingira. Lakini na katika kifungu cha (g) kinasema kwamba: "kuendeleza utoaji wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine kuhusiana na majukumu ya mamlaka".

Mhe. Mwenyekiti, kuusoma mswada huu kila eneo linasisitiza utoaji wa elimu, kila eneo linasisitiza utoaji wa elimu. Kwa sababu, si watu wengi walio na uelewa wa suala zima la mazingira. Sasa kama kifungu kipo basi ni lazima wahusika wa utoaji wa elimu wafanye wajibu wao kuhakikisha kwamba wamewaelimisha wananchi.

Kifungu (h) kinasema kwamba: "kutekeleza kanuni na kuhakikisha uzingatiaji wa viwango, miongozo na amri kuhusiana na mazingira". Suala la kanuni katika sheria zetu nyingi hapa Zanzibar mara nyingi walio na majukumu ya kutunga kanuni hawalipangi suala hili. Hata juzi hapa tumeshuhudia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais sheria imetungwa toka mwaka 2003 lakini mpaka juzi tunasomewa hapa kwamba kanuni imo katika matayarisho ya mwisho mwisho, mwaka 2003 hadi leo tuko mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, sasa sheria yoyote iliyokuwa haina kanuni inakuwa na uzito wa utekelezaji, wanapata tabu wanaosimamia sheria ile. Kwa hivyo, kama vifungu vinavyosema waziri anayehusika ahakikishe ametekeleza utayarishaji ule wa kanuni ili wale wanaohusika na kusimamia sheria waweze kupata unafuu na mabadiliko yaliyomo katika sheria ile ili kuweza kufuatilia lile suala ambalo linahitajika upande wao.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 23(d) kinasema kwamba: "Kuweka na kutoza ada na malipo kwa watoaji vyeti, vibali au ruhusa za huduma za kimazingira zitakazotolewa na mamlaka". Hapa ndio penye matatizo zaidi, utoaji huu wa ruhusa kwa kweli taasisi nyingi kila eneo wanatoa ruhusa, vyeti vimekuwa vingi, wasimamizi wamekuwa wengi na hali ikiwa hivyo hata mapato yanaweza yakapotea kirahisi. Ni vyema kukawa na utaratibu unaosimamiwa na taasisi husika masuala yote ya vyeti, ruhusa nyenginezo, vibali, ikawa serikali inajua jukumu hili limetupiwa wizara gani; kulikoni kwamba kila taasisi inatoa ruhusa. Hapa na wale wanaokwepa ndipo wanapopata kufanya yale ambayo ya kuitia hasara serikali.

Mhe. Mwenyekiti, katika matembezi ya kamati zako imebainika wazi katika Halmashauri moja kwamba maendeleo yao ya halmashauri kwa kweli Halmashauri ya Wilaya hiyo maendeleo yao ni upatikanaji wa uchimbaji wa mawe. Lakini kutokana na kwamba kila mtu anatoa ruhusa magari yanayobeba mawe wanapotakiwa na Halmashauri hiyo husika kutoa mapato wanapewa barua kwamba sisi tuna ruhusa ima ya sisi viongozi wakubwa, mimi nina ruhusa ya kiongozi fulani, ruhusa ya kiongozi fulani; imefika Halmashauri ile inakosa mapato katika ukusanyaji wa mawe. Kwa hivyo, hili ni miongoni mwa kuifanya serikali ikose hatua za maendeleo, lakini ikiwa serikali itaweka kituo maalum, watu maalum, taasisi maalum, basi tunaweza kupunguza wale wanaokwepa ulipaji huo wa ada.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika kifungu cha 33 kinasema kwamba, kuna kibali cha maliasili zisizorejesheka. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba, kuondosha, kusafirisha au kuuza maliasili zisizorejesheka bila ya kibali kutoka taasisi inayosimamia maliasili zisizorejesheka.

Mhe. Mwenyekiti, umarufuku huu bado narudia kusema, umarufuku huu hautopatikana n autaendelea kubaki katika kumbukumbu kama tutakuwa na usimamizi usiofaa. Sheria hii si wengi hivi sasa unaosikia katika wananchi wetu kwamba kuna sheria inasema hivyo, ni wachache mno unaowasikia hilo na hawa wenye shughuli hizi za kuchimba na kuondosha hawana habari hiyo, wao wapo wanaendelea na kazi zao. Kama hatutasimamia inavyopaswa basi Zanzibar iko hatarini.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuchimba na kuondosha tumeshashuhudia katika miundombinu ya maendeleo ya barabara katika nchi yetu, kumechimbwa mahandaki mpaka maji ya chumvi yakaanza kuja juu. Hayo nina ushahidi nayo katika maeneo mbali mbali wakati wa ujengaji wa barabara mwaka 1990 - 1992, Ambasha, Shengejuu; *Moro beach* iliyokuwepo pale palichimbwa mpaka maji ya bahari yakaja juu, Micheweni palichimbwa mpaka maji ya bahari yakaja juu, Konde maeneo ya kwendea Makangale palichimbwa mpaka ile ardhi yake ikawa iko ya umajimaji.

Kwa hivyo, kwa taarifa tulizonazo kwamba Zanzibar ni miongoni mwa visiwa vidogo na visiwa hivi vinasemekana kwamba viko chini ya bahari, yaani bahari iko juu kulikoni visiwa vyenyewe. Kutokana na kuyakaribisha maji ya bahari kwa uchimbaji wa kina kirefu basi kuna uwezekano maji ya bahari hayo yakaanza kuja kuvamia nchi yetu na hatima yake ikawa ndio mwisho wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuyanusuru hayo ni lazima mamlaka iweke kiwango cha uchimbaji wa *material* haya yanayojengewa barabara ili kuhakikisha kwamba tumeyanusuru mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia kifungu cha 77.

**Mwenyekiti:** Zingatia muda.

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Ahsante. Makosa yanayohusiana nje ya Mahakama. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana wizara kuweka kifungu hiki, huku ni kupunguza mrundiko wa kesi Mahakamani. Mhe. Hassan hapa asubuhi amesema kwamba, kwa ilivyo hii sheria basi tuandae magereza ya kuwaweka wananchi wetu, kwa nini? Kwa sababu mambo tuliyonayo ni mambo yaliyozoeleka kila mtu anafanya vile anavyoona katika eneo lake hakuna kibali, hakuna mambo mengine. Lakini kuweka kifungu hiki kinaweza kikasaidia na kutokana naWazanzibari hulka zao zilivyo wengi hawapendi usumbufu, hawapendi kuhangaishwa ,kwa hivyo watuwanapomaliziana bila kufikishwa Mahakamani ni njia moja ambayo itafanya mamlaka hii iweze kupata mapato kwa haraka na wananchi wetu waepukane na matatizo na Mahakama kuifanya kwamba isirundike kesi za aina kama hii kwa kutumia njia hii.

Pia, nitoe pongezi zaidi kwamba ni lazima hivi inavyosema sheria ifanyiwe kazi kama ilivyoelekeza isiwe kitu alichokichukua muhusika akapigwa faini ya papo kwa papo zaidi na lile tokeo, hapo itakuwa hatukuisimamia sheria wala hatukuwafanyia haki wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na muda wako na unaniangalia na kunihimiza kila mara nashukuru mimi nasema kwamba naunga mkono sheria hii kwa asilimia mia moja.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na amani katika nchi yetu na kuweza kuendelea na kazi za ujenzi wa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kuweza kufanya majumuisho baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu katika kuuchangia mswada huu.
Ni imani yangu kuwa leo baada ya muda sio mrefu Baraza lako tukufu litahitisha kazi ya kutunga ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ambayo itakuwan ndiyo tegemeo kubwa la kuwa na mazingira endelevu Visiwani Zanzibar, hasa kwa vile tutakuwa na chombo chenye nguvu kisheria ambacho naamini kwa kiasi kikubwa kitapunguza uharibifu na uchafuzi wa Mazingira katika visiwa vya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Serikali inayoongozwa na Mwenyekiti mahiri Mhe. Hamza Hasssan Juma Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kwamtipura kwa msaada wao mkubwa wakati wa kuupitia mswada huu. Kwa hakika maoni na michango yao imesaidia kufanya mswada huu kuwa bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, aidha naomba nichukuwe nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa wote waliopata nafasi ya kuchangia mswada huu. Hakika michango yao na maoni yao yalikuwa ni mazuri yenye kulenga katika kufanikisha madhumuni ya mswada huu.

Nawashukuru pia Waheshimiwa waliokuwa hawakupata nafasi ya kuchangia lakini walikuwa makini kusikiliza majadiliano na michango iliyokuwa inatolewa. Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imepokea pongezi zote zilizotolewa kutoka na kuwasilishwa kwa mswada huu.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kuunga mkono na kuona umuhimu wa kuletwa kwa mswada huu. Pia maoni na ushauri wote uliotolewa yanayohusiana na usimamizi na uhifadhi wa mazingira tumeyapokea na tutayafanyia kazi ipasavyo kadri hali itakavyoturuhusu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani na utangulizi huo naomba sasa niwatambue Washimiwa Wajumbe wote waliochangia mswada huu ambao wamezungumza.

| | |
|---|---|
| Mhe. Hamza Hassan Juma | Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa kitaifa ambaye pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura. |
| Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Mwakilishi wa Jimbo la Kitope |
| Mhe. Ali Salum Ali | Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani |

| | |
|---|---|
| Mhe. Mohammed Haji Khalid | Mwakilishi wa Jimbo la Mtambile |
| Mhe. Mwajuma Faki Mdachi | Mwakilishi wa Nafasi Maalum za Wanawake |
| Mhe. Fatma Mbarouk Said | Mwakilishi wa Jimbo la Amani |
| Mhe. Salum Abdalla Hamad | Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe |
| Mhe. Farida Amour | Mwakilishi wa Nafasi za Wanawake |
| Mhe. Abdi Mossi Kombo | Mwakilishi wa Jimbo la Matemwe |
| Mhe. Hassan Hamad Omar | Mwakilishi wa Jimbo la Kojani |
| Mhe. Rufai Said Rufai | Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe |

Mhe. Mwenyekiti, nachukuwa fursa hii sasa kutoa ufafanuzi juu ya ushauri na hoja mbali mbali zilizotolewa na Wajumbe kama ifuatavyo:-

Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais inakubaliana na Bango Kitita la marekebisho ya Mswada huu liliwasilishwa na Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa asilimia 99%.

Hata hivyo, katika vifungu vifuatavyo ofisi yetu ina maoni mengine, kifungu cha 32(1) katika kifungu hiki nakubaliana na marekebisho ya kuongezea maneno "zaidi ya" baina ya neno itakuwa na neno nusu. Ila nusu isiongezwe kwa kuwa tayari katika kifungu neneo hilo lipo na katika kifungu cha 59(1) kwenye kifungu hiki neno "Usafirishaji" linatakiwa kuwa "kusafirisha". Katika kifungu cha 71(1)(c) ambacho kinafutwa kifungu hichi sicho kinachofutwa kifungu hicho hakipo tunakubaliana na maoni ya kamati lakini hicho ni kifungu cha 71(2)(c) na sio 71(1)(c).

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na marekebisho ya kamati kuna marekebisho madogo madogo ambayo yamefanywa na ofisi yangu kama inavyoonekana kwenye jaduweli ya marekebisho ambayo nina hakika imegawiwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kugusia hoja mbali mbali kama zilivyowasilishwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako na nitaanza kwa kumzungumza Mhe. Makame Mshimba ambaye yeye kwa kweli alitupa ushauri juu ya namna bora ya kuweza kuitekeleza sheria hii. Tunampongeza sana kwa maoni ambayo ametupa na tunaahidi kwamba sisi tutayachukuwa na tutaweza kuyafanyia kazi.

Mhe. Ali Salum, alikuwa na hoja mbili tatu ambazo zilikuwa zinataka ufafanuzi. Katika kifungu cha 5 (6). Tunakubaliana na ushauri wa Mhe. Ali Salum kwa kulibadilisha neneo "atapeleka" na baada yake kuweka neno "atawasilisha" kwa ajili ya kiswahili kuwa kizuri zaidi.

Katika kifungu cha 16(3)(f) tunamuarifu Mheshimiwa kwamba akubaliane na mawazo yetu katika kipindi hiki kwa kuwa ni muhimu lakini tumeona bora tubakishe kifungu kama kilivyo kwa sababu hivi ndivyo utaratibu wa kisheria unavyotaka kwamba mtu yoyote ambaye hawezi kuhudhuria kwenye vikao akiwa ni mtumishi ni lazima atoe taarifa.

Mhe. Ali Salum hapa panazungumziwa vikao vitatu mfululizo na vikao hivi huwa ni mizi tisa kwa vikao vitatu mfululizo maana yake miezi tisa. Sasa ni lazima kwa kweli Mjumbe huyu aweze kupeleka taarifa na ninafahamu hoja yako kwamba pengine ni mgonjwa hawezi kufika yeye mwenyewe kutoa taarifa. Taarifa hii siyo lazima aipeleke yeye mwenyewe *physically* lakini anaweza kuandika barua.

Mhe. Mwenyekiti, naomba utulivu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Rufai kule tusaidie ili Mhe. Waziri anapotoa majibu tuweze kusikia na wewe uliuliza mambo mengi sana, tunaombwa tumsikilize.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru katika kifungu hiki cha 16(3)(f) tunamuomba Mheshimiwa atukubalie kibakie kama kilivyo kwa sababu taarifa hii si lazima aipeleke yeye mwenyewe anaweza kuwa kweli ni mgonjwa hawezi kufika pengine hayuko ndani ya nchi yuko kwenye matibabu lakini taarifa hii inaweza kupelekwa maandishi au hata ndugu na jamaa wanaweza kupeleka taarifa hiyo huo ndio utaratibu wa kazi unavyotaka. kwa hivyo, naomba atukubalie kifungu hicho kibakie kama kilivyo.

Mhe. Ali Salum pia katika kifungu cha 30(h) kwenye Mjumbe mwengine kutoka taasisi yoyote alisema anaona bora hapo tuweze kumuingiza Mhe. Sheha katika nafasi hii. Lakini tunaomba atukubalie kwamba kibakie kama kilivyo kwa sababu tukiandika tukimuandika Mhe. Sheha inabana kabisa nafasi ile kuweza kumualika mtu mwengine. Mwenyekiti, kama atakavyoweza inafaa ni nani amualike kwa siku hiyo kutokana na ile madhumuni ya kikao chenyewe inakwenda kuzungumza nini itampa fursa zaidi Mwenyekiti kumualika mtu mwengine yoyote, lakini tukiweka Sheha moja kwa moja imeshafunga mlango na hataweza kumuweka kama mjumbe ila Sheha anaweza kualikwa kama ni mualikwa wa kikao lakini sio kama Mjumbe.

Kifungu cha 33(3) Mheshimiwa alisema kuna migogoro mingi ya ardhi kwa watu wanaochimba mchanga na ni vyema maeneo yakaainishwa kwa kuweka mipaka. Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hicho kimeeleza kwamba katika mambo yaliyozingatiwa ni miongoni mwa eneo ukubwa wa eneo linalochimbwa kitu ambacho kinajumuisha pia mipaka ya eneo lenyewe. Mhe. Mwenyekiti, hilo limezingatiwa ndani ya sheria hiyo.

Kifungu cha 36 katika kifungu hiki nakubaliana na ushari wake kwa kuongeza adhabu kwa kosa linalohusiana na uchukuwaji wa fukwe na fungu, hivyo tunaweka kuanzia milioni mbili hadi kufikia milioni hamsini kutegemea na wingi wa uhamishwaji wa mchanga wenyewe kwa sababu hawa watakuwa wanatumia mchanga wa fukwe kwa ajili ya kufanyia biashara kitu ambacho tayari kimekatazwa na sheria hii.

Mhe. Mohammed Haji Khalid aliomba vile vile tunakubaliana na ushauri wake lakini katika kifungu hiki cha nane Wajumbe waliowekwa wote ni wataalamu na kazi ya kamati hii ya Ushauri kazi yake ni kumshauri Mhe. Waziri katika masuala haya ya mazingira na Mabadiliko ya Tabia ya Nchi. Kwa hiyo, ni vyema tunaomba atukubalie kwamba Kamati hii ibakie kama ilivyo kwa sababu kamati hii ni kamati ya wataalamu.

Kifungu cha 15 Mheshimiwa alisema ameona Mkurugenzi Mkuu lakini hakuona wapi Mkurugenzi Mkuu ameanzishwa au ametokea wapi. Naomba tu Mheshimiwa uangalie kwenye mswada kifungu cha 21 (1)(a) cha mswada huu kinaelezea vipi anapatikana Mkurugenzi Mkuu ambaye anakuwa Mjumbe katika hiyo ambayo wewe umeizungumza.

Katika kifungu cha 16(b) napenda kumjibu Mheshimiwa kwamba hapa tunakubaliana na ushauri wake kwa kurekebisha kifungu na baada yake kusomeka Mjumbe yoyote atasita kuwa Mjumbe ikiwa kuongeza hayo maneno.

Kifungu cha 20 katika kifungu Mheshimiwa Katibu wa Bodi hakutajwa katika orodha ya Wajumbe wa Bodi kwa sababu yeye si Mjumbe Mteule yeye anaingia katika nafasi yake na kwa kazi zake maalum wakati akiwa hana kura ya maamuzi kama walivyo Wajumbe wengine.

Kifungu cha 24(3) tumeuchukuwa ushauri wako Mheshimiwa na tayari tumezingatia katika marekebisho katika jaduweli ya marekebisho ambayo tumeiwasilisha kwa Waheshimiwa Wajumbe.

Kifungu cha 24(4) Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki ni kwamba kinasimamia majukumu ya awali aliyotakiwa kuyafanya katika kifungu cha 24(2) endapo hatowajibika na hilo nndipo atakapopewa adhabu kwa mujibu wa

kifungu cha 24 (3) na adhabu hizi zote ni Mahakama ndizo zenye uwezo wa kuamua kwa kufuata sheria hii sio maamla yenyewe. Mamlaka ina sheria na Mahakama itatumia sheria hii katika kufanya maamuzi hayo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na yeye amechangia mengi tumepokea ushauri wako hata hivyo kama itawekwa alivyopendekeza Mhe. Mwajuma Faki Mdachi kwamba tumuingize daktari au Sheha basi kifungu hicho cha 23(1) kinaweza kuziba nafasi ni bora tukiache kama kilivyo na kama nilivyoongea kwa Mhe. Ali Salum kwamba Mwenyekiti anangalia kwa siku ile nani atamuhitaji kuweza kuingiza katika mkutano huo.

Kifungu cha 13(f) katika kuandaa ripoti ya kimazingira, ripoti hii ya kimazingira Waheshimiwa Wajumbe inayozungumzwa hapa ni ripoti ya hali halisi ya mazingira ambayo ni ripoti inayozungumzia mienendo ya kimazingira kwa kipindi si chini ya miaka 5 au zaidi ambayo itaweza kukupa picha halisi ya mabadiliko ya kimazingira katika eneo husika.

Waheshimiwa Wajumbe ambao wamelizungumzia hili zile ripoti za kila mwaka zile ni ripoti nyengine za kiutendaji na mambo ambayo yanajitokeza siku hadi siku. Ripoti hii ni maalum ni ya kitaalamu na inafaandikwa baada ya kufanyika utafiti. Kwa hiyo, kinahitaji kipindi kirefu kuangalia labda hali ya mvua inavyokwenda kipindi cha joto, kipindi cha baridi na mambo kama hayo ili uweze akutayarisha ripoti hii. Kwa hiyo, ripoti hii muda wake kwa uchache ni miaka mitano, lakini nchi yengine wanaitoa hata baada ya miaka kumi wengine miaka 7.

Katika kufungu cha 16 (a) Mheshimiwa hapa kilichokusudiwa ni kumuandikia waziri ni pamoja na kutoa sababu za msingi zilizompelekea kujiuzulu.

Kifungu cha 84(2) tunaomba kibakie kama kilivyo kwa sababu asibabaishwe na neno Majini, majini yetu sisi ni maana ya ndani ya maji tukilichukuwa neno baharini kuna sehemu nyengine si bahari lakini yako maji na kuna vyombo vinapita ndani ya maji hayo. Kwa hiyo, tunaomba atukubalie tubakishe neno letu kama lilivyo la majini na tusitumie neno bahari pengine kwa Zanzibar tu hapo unaweza kuona ni bahari lakini kuna maeneo ambayo si bahari ni mito au maziwa ambayo vyombo pia vinapita.

Mhe. Fatma Said wa Jimbo la Amani amezungumzia kuhusu kifungu cha 70, amezungumzia mengi sana tunamshukuru kwa mchangio wake. Lakini ameomba litumike neno baada ya neno *Vote* katika kuzungumzia fedha za mamlaka na kidogo tumepata ukakasi katika kulitumia neno hilo la fungu kwa sababu tayari fungu tumelitumia ndani ya tafsiri ya sheria hii kukusudia mafungu yale ya mchanga ya baharini. Kwa hiyo, baada yake tunaweka neno kasma naomba utukubalie ili kuondoa utatanishi wa neno *Vote* katika mswada huu.

Mheshimiwam pia amezungumzia juu ya kutokuona hali nzima inayozungumzia fedha kuhusu makadirio na ukaguzi wa mahesabu za fedha za mamlaka. Mheshimiwa tunakushukuru kwa ushauri wako huo tunaviongeza vifungu hivyo viwili vitaengezwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu vitakuwemo, kifungu ambacho kitaelezea makadirio na vile vile kifungu ambacho kitaelezea ukaguzi wa hesabu hivyo vitaengezwa katika kufungu kile cha 70 kinachozungumzia fedha za mamlaka.

Mhe. Salum Abdalla Hamad nae namshukuru sana kwanza kwa elimu na utaalamu mkubwa kwa jinsi alivyoanza kuiongelea hoja yake na naamini wananchi watakuwa wamefaidika sana kwamba tafsiri ya mazingira pekeyake ni neno moja kubwa pana na ndio maisha yenyewe bila ya mazingira hakuna maisha. Nafikiri hilo ni jambo muhimu sana ambalo tumelitoa katika taaluma ambayo ulikuwa unaelezea katika tanbihi ya kuanza mchangio wako.

Sasa kwa mujibu wa kifungu cha 34 Mhe. Salum Abdalla kinachotolewa na sheria hii havihusiki na uchimbaji wa mchanga katika bahari kwa sababu sheria hii imepiga marufuku uchimbaji wa mchanga katika fukwe ama katika mafungu ya baharini sio mchanga wa baharini katika mafungu yaliko baharini.

Mhe. Hassan Hamad Omar kifungu cha 18 (2) tunakubaliana na ushauri wake juu ya mwenyekiti wa Bodi kushauriana na Mkurugenzi Mkuu pale anapotaka kuitisha mikutano. Katika kifungu cha 28 Mheshimiwa naomba

urejee tafsiri kuhusiana na neno Ukanda Maalum wa Pwani. Lakini kwa manufaa zaidi ni ningeomba nikisome hicho kifungu alikuwa anaogopa kwa jinsi alivyoweka kifungu cha 28 anasema anakiona kinaweza kikawaadhibu wavuvi kama kinavyosema hapa kama ni marufuku 28(2) ni marufuku kwa mtu yoyote kufanya shughuli yoyote katika eneo la ukanda maalum wa pwani bila ya ruhusa ya mamlaka.

Mheshimiwa naomba nikurejeshe tu kwenye tafsiri ya Ukanda Maalum ya Pwani ukiangalia kwenye sheria maana yake ni eneo la masafa kati ya mita 30 hadi 1 kuelekea ardhini linalopimwa kuanzia alama ya mwisho inayofikiwa na maji kujaa. Masafa ya mita 30 hadi 100 inategemea na aina ya ukanda husika. Kwa hiyo, usiwe na wasi wasi na mashaka yoyote kwamba wavuvi wanashikwa ndani ya sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 30 tumepokea ushauri wako kama unavyopendekezwa lakini tunaomba ibakie kama ilivyo ili isifunge nafasi ya kuweza kumuingiza mjumbe mwengine yoyote kwa sababu hiyo inata mu *include* pia mjumbe ambaye atatokana na taasisi za kiraia.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na suala ambalo alilizungumza Mhe. Mwenyekiti wa kamati lakini vile vile Mhe. Ali Salum nalo lina umuhimu wake kuhusiana na taka za Hospitali. Napenda kuwajulisha kwamba Wajumbe katika mswada wetu huu kuna kifungu cha adhabu za ujumla, hivyo ikiwa haikuwekwa adhabu hapo katika kifungu za ujumla kifungu cha 80 kinaweza kutumika kutoa adhabu kwa kosa hilo na jengine ambalo halikuwekewa adhabu katika sheria hii. Ni kweli hapana sheria pale pale lakini ziko adhabu katika kifungu cha 80 na hizo si tu zina muhusu mtu au taasisi ambayo ya binafsi lakini pia inaihusu Taasisi ya Serikali.

Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe muwe mnaangalia zile tafsiri za maneno ndani ya mswada wenyewe. Tafsiri ya neno mtu imejumuisha yote hayo. Kwa hiyo, naomba mturidhie kwamba bado ni wajibu wa taasisi au mtu yoyote kuhakikisha kwamba taka hizi za Hospitali zinatupwa kwa utaratibu unaofaa na asipofanya hivyo zipo sheria ambazo zinaweza kumshughulikia katika kifungu cha 80.

Mhe. Abdi Mosi Kombo Mheshimiwa wa Jimbo la Mtambwe aliulizia pia je kuna mahusiano gani ya dunia kwa ajili ya mabadiliko ya Tabia ya Nchi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa mabadiliko ya tabia ya nchi na itafiki ya kyoto. Kupitia vyombo hivyo Serikali imekuwa inashiriki mikutano mbali mbali inayoandaliwa na vyombo hivyo na imekuwa inapata misaada ya kutekeleza programu za mabadiliko ya tabia ya nchi. Sambamba na hilo Serikali imezindua mkakati wa mabadiliko ya tabia ya nchi ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi ambazo zinajitokeza ndani ya visiwa vyetu.

Pia alikuwa na suala, je, Serikali imejipanga vipi kuzuia athari za uchimbaji wa mafuta. Tunaeleza kwamba kwa kufuata Mswada huu, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi umedhibitiwa kisheria ili kupunguza na kuondoa athari za kimazingira ambazo zinazoweza kujitokeza, lakini sambamba na hili Serikali hivi karibuni itazindua sera ya mafuta na gesi ambayo baadae itafuatiwa na sheria yake;Sheria ya Mafuta ya Gesi. Mambo yote hayo ni kuhakikisha kwamba uchimbaji wa mafuta na gesi inshallah utakuwa salama bila ya kuiathiri jamii na mazingira yetu.

Mheshimiwa pia alisema mchang ukichukuliwa baharini, urejeshaji wa mashimoni nao ukoje. Kwa mujibu wa Mswada wa Sheria hii ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba, kukusanya, kuondoa, kusafirisha au kuuza mchanga kutoka kwenye fukwe au fungu ambapo ni sehemu muhimu wa mchanga wa baharini unapopatikana. Hivyo ni jukumu letu sote kusimamia utekelezaji wa sheria hii ili kuhakikisha tunahifadhi mazingira yetu.

Mheshimiwa alikuwa na masuala mengi, aliuliza pia njia gani zimepangwa kuhakikisha kwamba Mswada huu unatekelezwa. Mhe. Mwenyekiti, kwa hakika suala la elimu ambalo limechangiwa ninashukuru na Waheshimiwa Wajumbe karibu wote ambao wamesimama kuzungumzia juu ya Mswada ni la umuhimu sana na ndani ya Mswada wetu huu kuna kamati ambazo kazi yake ni kutoa elimu kuanzia ngazi za Shehia. Zinaundwa kwa mujibu wa sheria na moja ya majukumu yao ni kutoa elimu kwa raia, lakini naomba vile vile sisi tuliomo humu ndani ambao tunawawakilisha wananchi hilo pia ni sehemu ya jukumu letu, pale tunapokwenda kufanya mikutano yetu ndani ya Shehia mbali mbali tulichukue suala la mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi nalo tulielezee kwa wananchi wetu

na pale wanapotaka msaada siku hiyo kama una mkutano tukupatie wataalamu kutoka Afisi yetu ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwenda kuzungumzia suala la mazingira, tutakupatia ili mkutano huo uweze kufana na wananchi waweze kupata taaluma hiyo. *(Makofi)*

Ninawasihi sana kwamba hiyo pia ni sehemu ya majukumu yetu, sisi kwa upande wetu Serikali tunajitahidi sana na tutaendelea na hatuchoki. Moja ya kati ya kazi za Mkurugenzi wa Mazingira basi ni kutoa elimu, tutaiona imo ya Mswada huu. Kwa hivyo ninashukuru kwamba na nyinyi munaliona hilo kwamba sheria hii kuwa ni mpya, ikishakuwekwa saini sheria hii tutafanya mafunzo maalum kwa wadau wote lakini vile vile kwa wananchi kupitia vyombo mbali mbali vya habari kuwaelimisha juu ya uwepo wa sheria hii. Kwa sababu sheria hii ni kubwa na imekusanya mambo mengi ndani yake na sasa inakusudia kuweka adhabu kali kwa wale ambao wanaharibu mazingira kwa makusudi. Kwa hivyo sheria itawadhibiti, tutatoa taaluma hiyo na nitaomba Waheshimiwa Wajumbe tuendelee kusaidiana.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimezungumza mengi lakini siwezi kuyamaliza yale yote ambayo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wameyazungumza leo hii, niwashukuru sana na niseme mengi tunayachukua kwa ajili ya kuyafanyia kazi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya ufafanuzi na kwa heshima kubwa sana naomba Waheshimiwa Wajumbe wote waukubali Mswada huu ili uweze kuwa sheria na mfumo bora wa kitaasisi wa usimamizi wa mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu kwa faida yetu na kwa faida ya kizazi kijacho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima sana naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu baada ya kifungu.

**KAMTI YA KUTUNGA SHERIA**

**MSWADA WA SHERIA WA KUFUTA SHERIA YA USIMAMIZI KWA AJILI YA MAENDELEO ENDELEVU NAMBA 2 YA MWAKA 1996 NA KUWEKA BADALA YAKE MASHARTI BORA YA KUHIFADHI, KULINDA NA KUSIMAMIA MAZINGIRA ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

**SEHEMU YA KWANZA**

**UTANGULIZI**

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 Ufafanuzi

**SEHEMU YA PILI**
**MAJUKUMU YA JUMLA YA KIMAZINGIRA**

Kifungu 3 Jukumu la kulinda mazingira
Kifungu 4 Usimamizi wa mazingira katika mipango ya maendeleo
Kifungu 5 Haji na wajibu wa kuwa na mazingira bora safi na salama
Kifungu 6 Misingi ya usimamizi wa mazingira

**SEHEMU YA TATU**
**UTAWALA NA MUUNDO WA TAASISI**

Kifungu 7 Uanzishaji wa Kamati ya Ushauri wa Mazingira
Kifungu 8 Muundo wa Kamati ya Ushauri wa Mazingira

Kifungu 9 Kazi za Kamati ya Ushauri wa Mazingira
Kifungu 10 Mikutano ya akidi ya Kamati ya Ushauri na Mazingira pamoja na marekebisho yake
Kifungu 11 Uwezo na kazi za Waziri
Kifungu 12 Mkurugenzi wa Mazingira
Kifungu 13 Kazi za Mkurugenzi wa Mazingira pamoja na marekebisho yake
Kifungu 14 Uanzishaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira pamoja na marekebisho yake
Kifungu 15 Muundo wa uteuzi wa wajumbe wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 16 Muda wa kutumikia Afisi kwa wajumbe pamoja na marekebisho yake
Kifungu 17 Kazi za Bodi
Kifungu 18 Vikao vya Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 19 Maamuzi ya Bodi
Kifungu 20 Katibu wa Bodi
Kifungu 21 Uteuzi na uajiri
Kifungu 22 Kazi za Mamlaka
Kifungu 23 Uwezo wa Mamlaka pamoja na marekebisho yake

**SEHEMU YA NNE**
**TAHADHARI YA KIMAZINGIRA**

Kifungu 24 Tahadhari za kimazingira pamoja na marekebisho yake

**SEHEMU YA TANO**
**KITENGO CHA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIA YA NCHI**

Kifungu 25 Uanzishaji wa wa Kitengo cha Mazingira na Mabadiliko ya Tabia ya Nchi
Kifungu 26 Kazi za Kitengo cha Mazingira na Mabadiliko ya Tabia ya Nchi pamoja na marekebisho yake

**SEHEMU YA SITA**
**USIMAMIZI WENYE UWIANO WA UKANDA WA PWANI**

Kifungu 27 Eneo la ukanda wa pwani na Zanzibar pamoja na marekebisho yake
Kifungu 28 Uanzishaji wa ukanda maalum wa pwani

**SEHEMU YA SABA**
**USIMAMIZI WA MALI ASILI ZISIZOREJESHEKA**

Kifungu 29 Uanzishaji wa Kamati ya pamoja ya usimamizi ya mali asili zisizorejesheka
Kifungu 30 Muundo wa Kamati ya pamoja ya usimamizi wa mali asili zisizorejesheka pamoja na marekebisho yake
Kifungu 31 Kazi za Kamati ya pamoja ya usimamizi wa mali asili zisizorejesheka pamoja na marekebisho yake
Kifungu 32 Akidi ya vikao vya Kamati ya pamoja na usimamizi wa mali zisizorejesheka pamoja na marekebisho yake
Kifungu 33 Kibali cha mali asili zisizorejesheka
Kifungu 34 Jukumu la kuendeleza eneo lililochimbwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 35 Kumbukumbu za mali asili zisizorejesheka pamoja na marekebisho yake
Kifungu 36 Katazo la mchanga wa fukwe na fungu pamoja na marekebisho yake

**SEHEMU YA NANE**
**ELIMU YA MAZINGIRA NA UTAFITI**

Kifungu 37 Upatikanaji wa taarifa za kimazingira pamoja na marekebisho yake
Kifungu 38 Utafiti wa mazingira

**SEHEMU YA TISA**
**TATHMINI YA ATHARI ZA KIMAZINGIRA NA KIJAMII**

| | |
|---|---|
| Kifungu 39 | Mahitaji ya tathmini ya athari za kimazingira pamoia na marekebisho yake |
| Kifungu 40 | Vigezo vya kuzingatia shughuli zinazohitaji kufanyiwa tathimini ya athari za kimazingira |
| Kifungu 41 | Utambuzi wa kampuni na wataalamu wa kufanya tathmini ya athari za kimazingira |
| Kifungu 42 | Kusikiliza maoni ya jamii pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 43 | Ufuatiliaji |
| Kifungu 44 | Taarifa zinazohitajika |
| Kifungu 45 | Ripoti ya kimazingira pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 46 | Ukaguzi wa kimazingira |
| Kifungu 47 | Mgharimikiaji |

**SEHEMU YA KUMI**
**MKAKATI WA TATHMINI ZA MAZINGIRA**

| | |
|---|---|
| Kifungu 48 | Mkakati wa tathmini za kimazingira |
| Kifungu 49 | Majukumu ya Mkurugenzi wa Mazingira juu ya utekelezaji wa makakati wa tathmini za kimazingira pamoja na marekebisho yake |

**SEHEMU YA KUMI NA MOJA**
**UZUIAJI WA UCHAFUZI NA USIMAMIZI WA TAKA**

| | |
|---|---|
| Kifungu 50 | Viwango vya kimazingira |
| Kifungu 51 | Katazo la uchafuzi |
| Kifungu 52 | Katazo la kutupa kwenye eneo la bahari |
| Kifungu 53 | Usimamizi wa taka na maji machafu |
| Kifungu 54 | Katazo la kuharibu au kuangamiza bidhaa zisizofaa kwa matumizi pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 55 | Ufutiaji na ukaguzi |
| Kifungu 56 | Taka za hatari pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 57 | Vitu vya hatari pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 58 | |

**Mhe. Ali Salim Haji:** Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa dhati sana. Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nilizungumzia kwa kina sana suala la taka za hospitali na ninashukuru kwamba Mhe. Waziri alinisikia. Ninashukuru kwa mara nyengine tena kwamba kanijibu.

Mhe. Mwenyekiti, katika jibu lake akanipeleka kwenye kifungu cha 80. Mhe. Mwenyekiti, bado sijaridhika na majibu ya Mhe. Waziri. Ninamtaka Mhe. Waziri anipe ufafanuzi wa kina. Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kama utakisoma kinazungumzia namna ya Taasisi ya Serikali za Mitaa au Taasisi nyengine inayohusiana na taka kwa kushauriana na Wizara ya Afya itahakikisha kwamba taka zote za hospitali zinakusanywa, zinahifadhiwa, zinasafirishwa na zinateketezwa kwa utaratibu unaofaa utakaothibitishwa na mamlaka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaanza kupata wasi wasi kwamba sheria hii kuna baadhi ya watu moja kwa moja tunawalenga namna ya kuwaadhibu, ama tunawapiga faini au tutawafunga. Lakini kwa zile taka hatarishi ambazo zinahatarisha maisha ya mwanadamu sijui hofu ipo kwamba tusiwaadhibu ama kuwapiga faini ama kuwafunga, halafu tunakwenda kusema eti kifungu cha 80 kina adhabu za jumla ndizo wataingia huku.

Mhe. Mwenyekiti, mimi siyo mwanasheria lakini kama sheria mtu hujamtia hatiani imeshauri tu, maana yake zaidi imetoa ushauri wa kuhifadhi, kuchukua, kupeleka, yaani hapana kifungu, halafu uje umwambie mtu unamuhukumu kufuatana na sheria hii, wakati sheria hii haimtii hatiani kwa kosa alolitenda.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa twende kwenye *point* yako moja kwa moja.

**Mhe. Ali Salim Haji:** Mhe. Mwenyekiti, ninamuomba Mhe. Waziri anipe majibu ya kina ili niridhike katika kifungu hiki cha 58.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, ninadhani sote tumemsikia Mhe. Waziri katika majumuisho yake, of course ndiyo madhumuni ya kuwa na kifungu cha adhabu cha jumla. Maana yake kuna vifungu vyengine huviwekea adhabu zake kwenye vifungu vyake, ndiyo maana tumewekwa kifungu cha 80, kama adhabu hii haipo huku, halafu kifungu cha 80 kinatosha kumtia adhabu mtu yeyote atakayefanya makosa kwa mujibu wa kifungu cha 58.

Mimi ninadhani maelezo ya Mhe. Waziri yametosha na Mhe. Ali Salim Haji nimuombe kwenye hii hakuna haja ya mjadala, kwa sababu kifungu cha 80 kipo wazi na kinaweza kumtia adhabu mtu yeyote.

**Mhe. Ali Salim Haji:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mwanasheria. Mwanasheria ni mwanasheria lakini kifungu cha 58 hakioneshi kwamba ni kosa, angalau basi kingekuwa kinasomeka kwamba ni kosa kisheria halafu yakaendelea na hayo maneno mengine, lakini haioneshi kwamba kifungu hiki ni kosa, kifungu kinatoa ushauri tu Mhe. Mwenyekiti.

Hata adhabu yenyewe imezungumzia. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka kutoa mfano mmoja ingawa Mhe. Waziri alipokuwa anatoa majibu alisema inawezekana, watu wanasoma maandiko, maandiko yanasema ni mtu, hayasemi taasisi. Mhe. Mwenyekiti, kuna siku *dispensary* sina haja ya kuitaja ilitupa taka usiku kwenye Shehia ya Kwaalimsha, taka zilitupwa ndani ya jumba bovu lakini tulichokibaini ni *documents* ambazo tumezikuta pale sindano na madubwana mengine, lakini tulikuta *documents* zinaonesha lile jina la *dispensary* yenyewe, tukazichukua mimi na Mhe. Sheha wakati mimi nikiwa Diwani kuifuta ile *dispensary*, mwenyewe akakiri aah! mimi nilimpa mtoto apeleke, mtoto wenyewe hajulikani lakini tunajua ni taasisi. Hapa haioneshi ni taasisi, inazungumzia mtu yeyote.

Sasa mtu yeyote anaweza kutupa akawa asijulikane. Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi wa kutosha Mwanasheria anisaidie niridhike katika hili. Mtu yeyote, yaani ni mtu yeyote mtu mmoja au ni taasisi, halafu lakini kwa nini hawa wote kifungu cha 59 kinasema ni marufuku. Yaani marufuku ni kosa kwamba utakapofanya hilo umefanya kosa, lakini humu halioneshi hilo.

Hebu asome kifungu cha 59, halafu kifungu 58. Ninataka majibu ya kuridhisha Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, mimi ninadhani na Mhe. Ali Salim Haji tunazungumza lugha moja. Kwa sababu kwanza hizi taka za hospitali zina utaratibu wake wa kuzitupa, hazitakiwi kutupwa jaani kama unapotupa taka za nyumbani, zinatakiwa zitengenezewe chombo maalum na ambazo zinachomwa moto kusema kweli, ndiyo utaratibu wake wa kushughulikia hizi za hospitali. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, Mhe. Mwenyekiti, msisitizo unaowekwa hapa kwamba na hizi taka zote zichukuliwe kwa msingi huo uliowekwa hapa na kama kosa ni kutendeka maana yake kifungu cha 80 ndio kitatoa adhabu na hizi mamlaka zinafanywa kwanza na watu, kile chombo ni watu wanachokiongoza. Kwa hivyo, wale watu watakaofanya hayo makosa kifungu cha 80 tayari kipo.

Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, hakuna ubishi kwenye hili, vyenginevyo labda Mhe. Ali awe ana maelezo mengine, lakini mamlaka, serikali za mitaa au taasisi nyengine hizi zote zinaongozwa na watu na hawa watu ndio wamepewa dhamana ya kushughulikia hizi kazi, sasa wanapokwenda kinyume ndio adhabu zimewekwa huku Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kama kuna jambo linalindwa basi tuambizane. Lakini kama tunataka kutunga sheria basi tukubali kutunga sheria. Mhe. Mwenyekiti wakati Mhe. Mwanasheria ananiambia kwamba mamlaka zinazohusika zina utaratibu. Mhe. Mwenyekiti, hata wewe ni shuhuda kwamba tulipiga kelele Kamati ya Ustawi wa Jamii namna ya kutupa taka nyuma ya Mapinduzi Mpya, taka zilioneshwa mpaka kwenye *TV*, yaani watu wote walishuhudia. Lakini hakuna jambo, nasema Mhe. Mwenyekiti na mataka yalikuwa ni hatari huwezi hata kuelezea, nasema kwamba hili ni tatizo. Tunaona tabu kitu gani kutaja mtu yeyote au taasisi kwenye kifungu cha 80. Hapa kaandikwa mtu yeyote au taasisi, halafu tunaona tabu gani kutaja. Yaani tutafute lugha ya kuweka kwamba ile mamlaka itakapofanya kosa ijulikane kuwa imefanya kosa, lakini huku haionekani kama mamlaka inafanya kosa.

Kwa sababu nakubali kuwa kifungu hiki cha 80 kitaadhibu, lakini kitaadhibu nini wakati huku halioneshi kama hili ni kosa.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Mjumbe ni sahihi, lakini unaposoma sheria usisome kifungu kimoja, usome sheria kwa vifungu vyote vinavyohusika. Sasa ukisoma kifungu cha 58, pale maana yake ni kuchafua mazingira, ukikisoma hicho unataona kwamba hapo inakataza kuchafua mazingira. Sasa kama ni kuchafua mazingira kifungu cha 51, kinasema; katazo la uchafuzi na amesema kwamba ni marufuku kwa mtu yeyote kuchafua au kumruhusu mtu mwengine kufanya kitendo kinachosababisha uchafuzi wa mazingira. Sasa hiyo marufuku anayosema tayari imeshakuwepo na kama mtu atafanya hivyo basi kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu adhabu yake iko katika kifungu cha 80. Kwa hivyo, ni sahihi kwa kweli kifungu hiki cha 58 ukisome pamoja na kifungu cha 51 na ukisome pamoja na kifungu 80, lile tatizo au wasi wasi wake umeshasawazishwa hapa.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo naomba tusome kifungu cha 51 ambacho kinapiga hiyo marufuku anayotaka yeye na kifungu cha 58 kwamba anachafua mazingira, na kama ukifanya hivyo basi kifungu cha 80 kitatoa adhabu inayohusika. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru waliosimama wote ni wanasheria, mimi sio mwanasheria, lakini nataka tu tusaidiane mawazo tu Mhe. Mwenyekiti mpaka tufike pahala. Mhe. Mwenyekiti, kama kifungu cha 51(1) ndivyo kinavyozungumza kama ni marufuku kwa mtu yeyote kuchafua, au kumruhusu mtu mwengine kufanya kitendo kinachosababisha uchafuzi wa mazingira, kwa hivyo kwa viwango vyovyote vya kimazingira vilivyowekwa na sheria yoyote inayotumika, basi nafikiri ilikuwa haina haja ya mantiki ya kifungu cha 58 kuwekwa, kwa sababu tayari kimeshaainisha kwamba kimepiga marufuku uchafuzi wa mazingira na suala la hapa pia linazungumza masuala ya mazingira. Hilo ni moja.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, kilio changu huku ametajwa mtu, taka zinaweza kutupwa usiku na usimbaini mtu aliyetupa na taasisi ina wafanyakazi wengi hatujui zamu gani saa iliyotupwa taka. Kama hatukumjua mtu aliyetupa taka maana yake taasisi iliyotupa tunaweza tukaikamata kutokana na *document* kupitia vyeti au vitu vyengine, au dawa ambazo zitakuwa zina nembo ya ile taasisi yenyewe, sasa hapa tumetaja mtu peke yake, umempata sawa hukumpata taasisi kwa nini unashindwa kushtaki. Hiyo ndio hoja ya pili.

Hoja ya mwanzo aliyozungumza Mhe. Abubakar Khamis, kama kuna hoja ambayo ni kifungu cha 51, basi hana haja ya kuweka kifungu cha 58, kwa sababu kinajitosheleza kwa mtu yeyote atakayechafua mazingira. Lakini ya pili huku tunamtaja mtu *specific*, hatukutaja taasisi.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, sheria hapa kuna kitu kinachoitwa *general,* kinaelezea kwa jumla. Halafu hala kifungu cha 58 kimezungumzia *specific* kwamba ukifanya ukifanya kitu hiki na hiki, kwa sababu uchafuzi wa mazingira sio lazima haya yaliyowekwa hapa tu, lakini haya yamewekwa *specific* kwamba ukifanya makosa haya nayo ni uchafuzi wa mazingira, mbali na huo uchafuzi mwengine, kwa hivyo hili *specific* limewekwa.

Sasa unaposema kwamba kuna taasisi ambayo inaweza ikatupa taka pahala, sasa hiyo itakuwa iko kwenye suala jengine, kwa sababu humjui aliyetupa taka usiku, taka hizo za hospitali kwa mfano, au taka nyengine zozote utakuwa humjui. Kwa hivyo hapo kuna suala jengine la *investigation* mpaka ukajua na ukishakujua taasisi na mtu mwengine yeyote, zimo sheria zake au utaratibu wake humu, kama umeshajua kuwa hii ndio taasisi iliyofanya, kwa hivyo unaikamata taasisi, ukishamjua huyu ndiye mtu aliyefanya basi unamkamata yule mtu kwa mujibu wa vifungu vilivyopo.

Kwa hivyo, tunazungumzia hapa, huku amezungumzia *general* tu kuwa itakuwa ni tatizo au ni kosa kwa kuchafua mazingira. Hapa akaja *specific* akataja katika mazingira hayo ni pamoja na kufanya hivi aliyotaja katika kifungu cha 58. Kwa hivyo, hivi ni vifungu ambavyo vina- *specify* kwamba ukifanya hili nalo litakuwa ni kosa.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Kwanza Mhe. Ali angesoma tafsiri ya mtu kwenye sheria hii huyo mtu ametafsiriwa, na hayo aliyosema mamlaka sijui taasisi, yote yameelezwa kama yote hiyo ni mtu. Sasa kifungu cha 80 kimetaja huyo mtu. Sasa mimi sioni kwa nini hoja yake anasema kifungu cha 80 hakitoshi kwa sababu hakijaandika mamlaka, lakini ukisoma tafsiri ya mtu tayari imeshaeleza tafsiri yake mtu, inasema;

"Mtu inajumuisha mtu mwenyewe kikundi cha watu, jamii, taasisi ya serikali, taasisi binafsi, shirika, kampuni, kiwanda au jumuiya". Sasa ni kifungu cha 80 vile kiko. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante. Mhe. Ali Salum naomba tufike pahala tukubaliane, kwa sababu umeshasimama zaidi ya mara tatu kwa ajili ya mdahalo huu, au tufikie kwenye maamuzi ya kura. Mhe. Ali Salum.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, watu wanasema wakubwa wakisimama mdogo inabidi ukae. Naomba tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu 58 Taka za Hospitali
Kifungu 59 Utafutaji, Uchimbaji au Usafishaji wa Mafuta au Gesi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 60 Umwagikaji wa Mafuta au Uvujaji wa Gesi pamoja na marekebisho yake.

**Sehemu ya Kumi na Mbili**
**Uhifadhi wa Bioanuwai na Usimamizi wa Vyanzo vya Maji**

Kifungu 61 Kutangazwa Eneo la Hifadhi
Kifungu 62 Usimamizi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 63 Miongozo ya Uhifadhi wa Bioanuwai.
Kifungu 64 Katazo la Bioanuwai.
Kifungu 65 Uhifadhi wa Vyanzo vya Maji pamoja na marekebisho yake.

**Sehemu ya Kumi na Tatu**
**Usimamizi wa Mabadiliko ya Tabianchi**

Kifungu 66 Taasisi dhamana ya Kusimamia Mabadiliko ya Tabianchi
Kifungu 67 Uanzishwaji wa Kamati ya Mabadiliko ya Tabianchi
Kifungu 68 Muundo na Kazi za Kamati ya Uongozi ya Mabadiliko ya Tabianchi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 69 Muundo na Kazi za Kamati ya Kitaalamu ya Mabadiliko ya Tabianchi pamoja na marekebisho yake.

**Sehemu ya Kumi na Nne**
**Vifungu vya Fedha**

Kifungu 70 Fedha za Mamlaka.
Kifungu 71 Vyanzo vya Mfuko pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 72 Maamuzi ya Fedha na Mapato ya Mamlaka pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 73 Kuanzishwa kwa Mfuko wa Mazingira pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 74 Matumizi ya Fedha za Mfuko wa Mazingira.

**Sehemu ya Kumi na Tano**
**Makosa na Adhabu**

Kifungu 75 Makosa Yanayohusiana na Afisa Mwenye Mamlaka pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 76 Makosa Yanayohusiana na Kushindwa kutii Amri ya Kusitisha.
Kifungu 77 Makosa Yanayohusiana nje ya Mahakama pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 78 Makosa Yanayohusiana na Kurudia na Kuendelea Kutenda Kosa.
Kifungu 79 Makosa Yanayohusiana na Jaribio la Kutenda Kosa.
Kifungu 80 Adhabu za Jumla.
Kifungu 81 Vifungu vya Jumla Vinavyohusiana na Adhabu.

**Sehemu ya Kumi na Sita**
**Masharti Mengineyo**

Kifungu 82 Uteuzi na Uwezo wa Afisa Mwenye Mamlaka.
Kifungu 83 Kinga.
Kifungu 84 Mwendesha Mashtaka wa Mazingira pamoja na marekebisho yake.

| | |
|---|---|
| Kifungu 85 | Uwezo wa Waziri wa Kuzuwia pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 86 | Uwezo wa Kutunga Kanuni. |
| Kifungu 87 | Kufuta na Kubakiza. |

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu, na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante. Waheshimiwa Wajumbe niwahoji. Wanaoafiki wanyooshe mikono. Wasioafiki. Walioafiki wameshinda. Mhe. Waziri.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar 2015**

*(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba mswada wa sheria ya usimamizi wa mazingira Zanzibar ya mwaka 2015, usomwe kwa mara ya tatu.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe niwahoji. Wanaoafiki wanyooshe mikono. Wasioafiki. Walioafiki wameshinda. Katibu. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufanya shughuli zetu hadi tukafika katika hatua hii. Lakini vile vile niwashukuruni sana kwa namna ambavyo mmenipa mashirikiano na kuweza kufanya kazi hii nzito na kuweza kumaliza kwa salama. Kilichobaki kwa sasa ni kuchukua nafasi hii vile vile kuahirisha Baraza letu hili tukufu kutoka leo tarehe 27/01/2015 hadi kesho tarehe 28/01/2015 saa 3:00 za asubuhi, bila kuchelewa. Naomba kuahirisha.

(*Saa 12:30 jioni kikao kiliahirishwa mpaka tarehe 28/01/2015 saa 3:00 kamili za asubuhi*)